# TASHTITI KATIKA VIBONZO VYA KISIASA: UCHUNGUZI WA VIBONZO KATIKA TOVUTI YA MSANII GADO.

MBURU, KERRYANN WANJIKU

Tasnifu hii imewasilishwa kwa Shule ya Mafuzu kwa Madhumuni ya Kutosheleza Mahitaji ya Shahada ya Uzamili, katika Taaluma ya Kiswahili na Mawasiliano, ya Chuo Kikuu Cha Laikipia.

October, 2024

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Matokeo ya utafiti huu yalitokana na juhudi zangu binafsi na hayajawasilishwa na mtu mwingine kwa ajili ya kuendeleza mahitaji ya shahada yoyote ile katika Chuo Kikuu chochote kile.

Sahihi: ______________________ Tarehe: ______________________

**Mburu, Kerryann Wanjiku**

**MK22/2505/2017**

**Idhini**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Laikipia.

Sahihi: ______________________ Tarehe: ______________________

Dkt. Sheila P. Wandera-Simwa

Idara ya Usomilugha na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Laikipia

Sahihi: ______________________ Tarehe: ______________________

Prof. Nabea Wendo

Idara ya Usomilugha na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Laikipia

# HATIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili tasnifu hii kwa njia yoyote ile. Lazima idhini itolewe na mwandishi au Chuo Kikuu cha Laikipia

©*Mburu Kerryann Wanjiku 2024*

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wandani wangu Kelvin Njore na Elianalove Wangari ambao wamekuwa wenye subira katika kipindi hiki cha masomo yangu. Pili, naitabaruku kwa wazazi wangu Bw. Nicholas Mburu na Bi. Ruth Mburu ambao walinihimiza kuendeleza masomo yangu hadi kufikia kiwango hiki.

## SHUKRANI

Utafiti huu haujafanikishwa na juhudi zangu pekee yake, ila imegharimu juhudi za watu wengi. Kwa hivyo, ningependa kutoa shukrani zangu kwa watu mbalimbali walionitia moyo na kunishika mkono ili niweze kufanikiwa katika shughuli hii nzima ya usomi. Kwanza kabisa, natoa shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu ambaye alinijalia na neema, uwezo, hekima na ari ya kufanya utafiti huu.

Pili, nashukuru usimamizi wa Chuo Kikuu cha Laikipia kwa kufadhili masomo yangu ya Uzamili, na kunipa nafasi ya kupata mtaji wangu kupitia kwa Chuo Kikuu cha Laikipia. Asanteni sana, sina njia nyingine ninayoweza kuonyesha shukrani zangu ila kuomba Mola azidi kuwakirimia wema zake.

Vilevile, ningependa kumshukuru msimamizi wangu Dkt. Sheila Pamela Wandera-Simwa kwa kunitia moyo na kunielekeza kwa upendo mwingi kama jinsi mama anavyomwelekeza mwanawe. Asante sana kwa kutembea nami katika safari hii ya usomi iliyo na panda shuka nyingi. Umekuwa wa msaada kwangu na ombi langu kwako ni Jalali akubariki, akujalie na akuneemeshe katika shughuli zako zote.

Tatu, ningependa kutoa shukrani zangu kwa msimamizi wangu Prof. Wendo Nabea, kwa uelekezi wake na ushauri wake wa kiusomi. Asante Profesa kwa kunifunza jinsi ya kuwa makinifu katika kazi yangu. Nakushukuru kwani hukuniruhusu kuzembea katika shughuli nzima ya usomi. Naomba Mola akubariki mara dufu.

Pia ningependa kuwashukuru wahadhiri wengine kama vile; Prof. James Ogola, Prof. Felicia Yieke, Prof. Nicholas Kamau na Dr. Nelson Nderitu ambao walinitia moyo katika shughuli nzima ya usomi. Vilevile, shukrani za dhati ziwaendee wasomi wenzangu; Bi Lucy Mugo, Bw. James Mwangi, Bw. Nicholas Kirui, Bw. Simon Wanjohi kwa ushirika wenu na kwa juhudi za kutiana moyo katika shughuli nzima ya usomi. Asanteni sana.

Hatimaye, shukrani za dhati ziwaendee wazazi wangu Mzee Nicholas Mburu na Mama Ruth Mburu, pamoja na dada zangu kwa upendo wenu kwangu na kujitolea mhanga kuniombea katika safari yangu ya kiakademia. Kwa mpenzi wangu Kelvin Njore na mwanangu Elianalove Njore, asanteni kwa kuwa wavumilivu na wenye subira katika kipindi hiki cha usomi. Mola awabariki na awaneemeshe.

## IKISIRI

Sanaa ya uchoraji vibonzo ni taaluma ambayo imekuwepo tangu jadi na ina mvuto mkubwa kwa watafiti wengi kutokana na uwezo wake wa kusimba jumbe zisizoweza kusemwa wazi wazi. Kwa kawaida, ufasiri wa vibonzo unaweza kuzua utata kutokana na sababu kadhaa. Kwanza, hadhira inaweza kufasiri ujumbe uliopo kwenye vibonzo tofauti na alivyokusudia mchora vibonzo. Pili, katika uchoraji wa vibonzo, mchora vibonzo huchukulia kuwa hadhira yake ina ujuzi wa awali kuhusiana na kinachoangaziwa. Hivyo basi, ikiwa hadhira ya mchora vibonzo haina ujuzi wa awali kuhusiana na kinachosawiriwa, huenda hadhira lengwa isipate ujumbe kama ilivyokusudiwa. Ifahamike kuwa sifa kuu ya vibonzo vya kisiasa ni kuwa vinapaswa kuwa cheshi na vyenye tashtiti ndiposa viweze kuwasilisha masuala tata kwa njia ya kimzaha. Kutokana na hali hii, utafiti huu ulichunguza tashtiti katika vibonzo vya kisiasa vya Godfrey Mwampembwa almaarufu Gado vilivyochapishwa katika mwaka wa 2017 kwenye tovuti yake. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vya Gado, kisha kuhakiki mikakati iliyotumika katika kuendeleza maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vilivyoteuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure, Roland Barthes na baadaye kuhakikiwa na Wamitila. Mihimili ya nadharia hii ilitumika kuchambua mikakati iliyotumiwa na Gado katika vibonzo vyake kwa minajili ya kuendeleza maudhui ya kitashtiti. Utafiti huu ni wa kimaelezo na ulifanyika mtandaoni, pale ambapo mtafiti alipekua tovuti ya Gado (www.gadocartoons.com) na kuteua kimaksudi vibonzo ishirini kutokana na jumla ya vibonzo sitini vilivyokuwa vimechapishwa katika mwaka wa 2017. Uteuzi huu ulijikita katika vibonzo vilivyofungamana na madhumuni ya utafiti huu na vilitumika kama data ya utafiti wenyewe. Baadaye, mtafiti alirekodi data aliyokusanya kwa njia ya maandishi, akaitafsiri, akaisimba na kisha kuichanganua kwa njia ya maelezo. Ufafanuzi wa matokeo ya utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti, mihimili ya nadharia iliyoteuliwa na mipaka ya utafiti wenyewe. Kwa jumla, utafiti huu ulithibitisha kuwa maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vya Gado yalikuwa ya kitashtiti kwani yalilenga kuweka wazi maovu yaliyokuwa yakiendelezwa na serikali ya mwaka wa 2017. Waaidha, mtafiti aligundua kuwa mwanavibonzo Gado alitumia mbinu za lugha kama vile; kinaya, kejeli, metonimia, sitiara, analojia na mwingiliano matini kama mikakati ya kuibua kitashtiti katika vibonzo vyake. Vilevile, utafiti huu ulionyesha kuwa Gado alitumia ishara kama vile; matumizi ya rangi mbalimbali, pamoja na alama kama vile; heshtegi, mviringo na nyota, matumizi ya anwani na vipovu vya sauti kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vyake. Mwishowe, utafiti huu ulidhibitisha kuwa vibonzo vilivyochapishwa kwenye mtandao, vilidhihirisha uhuru na ukali mwingi katika usawiri wa masuala mbalimbali, jambo ambalo lilisaidia katika kufanikisha lengo kuu la tashtiti; ambalo ni ushambulizi unaochochea mabadiliko. Mwishowe, matokeo ya utafiti huu yalitarajiwa kuwanufaisha wanamawasiliano, wanasemiotiki na wasomi wa masuala ya kisiasa kwa kuwapa mtazamo mpya kuhusiana na matumizi ya maneno na ishara katika kusimba jumbe tata zinazochapishwa kwenye mtandao ambapo kuna uhuru mwingi wa kuelezea masuala tata bila kudhibitiwa.

## ABSTRACT

The art of cartooning has been around for decades, and it has received a lot of attention from researchers due to the fact that cartoons can encode messages that people might find hard to convey directly. More often than not, confusion and ambiguity may arise in the interpretation of cartoons as it is assumed that the audience has prior knowledge of what the cartoons are meant to convey. Ordinarily, political cartoons are humorous, rhetorical, and satirical. They playfully communicate controversial issues. As such, this study investigated satire in political cartoons that were published on the internet by a Kenyan cartoonist Godfrey Mwampembwa popularly known as Gado in the year 2017. The main objective of the study was to identify and examine satirical themes in Gado's political cartoons and the satirical strategies employed in conveying the said themes in the political cartoons that were selected. This research was guided by the Semiotics theory as espoused by Ferdinand De Saussure, Roland Barthes, and later reviewed by Wamitila. The researcher used the Semiotics theory as espoused by Wamitila to collect and analyze data for this research. The study employed a descriptive research design, where the researcher purposively selected twenty political cartoons from a corpus of sixty political cartoon that were published in the year 2017 by Gado. During the sampling of the twenty political cartoons, the researcher took into consideration those that were in line with the objectives of the study. The research was carried out on the internet, where the researcher downloaded and printed out selected cartoons from www.gadocartoons.com. The data from the sampled political cartoons was recorded, translated, coded, analyzed and presented with respect to the two main objectives of the research, the theory, and the scope of the study. The research findings showed that the themes portrayed in Gado's political cartoons were satirical in nature as they brought to light the ills that ailed the government that was in power in the year 2017. In addition to that, the researcher found out that Gado used stylistic devices such as; sarcasm, irony, metaphors, metonyms, analogy, and intertexuality as strategies for bringing out satire. Furthermore, the research findings showed that Gado used visual signs such as; use of different colors, symbols such as asterisks, and hashtags, use of titles and speech bubbles as satirical strategies, meant to attack specific targets with the aim of causing change in behavior. Finally, the research found out that there was more freedom and bluntness in portraying issues in political cartoons that were published on the internet. It is from this new found freedom and bluntness, that cartoonists such as Gado are able to realise the role of satire; which is to attack specific targets with the aim of causing change. In conclusion, the findings of this research were envisaged to be beneficial to communication students, semioticians, and researchers in the field of politics, where the findings would bring in a new perspective in the use of texts and signs in encoding messages that are published on the internet where there is no censorship and hence more freedom of expression and more so on issues that are deemed controversial.

**YALIYOMO**

UNGAMO NA IDHINI ........ ii
HATIMILIKI ........ iii
TABARUKU ........ iv
SHUKRANI ........ v
IKISIRI ........ vi
ABSTRACT ........ vii
YALIYOMO ........ viii
MAELEZO YA VIFUPISHO ........ xi
MAELEZO YA ISTILAHI ........ xii
**SURA YA KWANZA ........ 1**
**UTANGULIZI ........ 1**
1.1 Usuli wa Mada ........ 1
1.1.1 Tashititi. ........ 1
1.1.2 Vibonzo vya Kisiasa ........ 2
1.1.3 Vibonzo na Mtandao ........ 5
1.2 Suala la Utafiti ........ 6
1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 7
1.4 Maswali ya Utafiti ........ 7
1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 7
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 8
**SURA YA PILI ........ 10**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA ........ 10**
2.1 Utangulizi ........ 10
2.2 Mapitio ya Maandishi ........ 10
2.2.1 Maudhui katika Vibonzo vya Kisiasa ........ 10
2.2.2 Mikakati Inayoendeleza Maudhui ya Kitashtiti ........ 15
2.3 Msingi wa Nadharia ........ 19
**SURA YA TATU ........ 23**
**MBINU ZA UTAFITI ........ 23**
3.1 Utangulizi ........ 23
3.2 Muundo wa Utafiti ........ 23
3.3 Mahali pa Utafiti ........ 23

3.4 Kundi Lengwa ........ 23
3.5 Uteuzi wa Sampuli ........ 24
3.6 Ukusanyaji wa Data ........ 25
3.7 Uchanganuzi wa Data ........ 26
3.8 Uzingativu wa Maadili ........ 27
**SURA YA NNE ........ 28**
**UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA ........ 28**
4.1 Utangulizi ........ 28
4.2 Maudhui katika Vibonzo ........ 28
4.2.1 Uongozi ........ 29
4.2.2 Unyanyasaji wa Wafanyikazi ........ 43
4.2.3 Ulaghai katika Siasa ........ 47
4.2.4 Ufisadi ........ 53
4.2.5 Ukosefu wa Maadili ........ 58
4.2.6 Upendeleo ........ 62
4.2.7 Unafiki ........ 64
4.2.8 Hitimisho ........ 66
4.3 Mikakati ya Kitashtiti ........ 66
4.3.1 UKaragosi ........ 66
4.3.2 Sitiara ........ 68
4.3.3 Kejeli ........ 78
4.3.4 Kinaya ........ 83
4.3.5 Metonimia ........ 90
4.3.6 Analojia ........ 95
4.3.7 Matumizi ya Anwani, Vipovu vya Sauti na Kutaja ........ 97
4.3.8 Matumizi ya Alama ........ 101
4.3.9 Matumizi ya Rangi mbalimbali ........ 103
4.3.10 Mwingiliano Matini ........ 107
4.3.11 Hitimisho ........ 111
**SURA YA TANO ........ 112**
**MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 112**
5.1 Utangulizi ........ 112
5.2 Mahitimisho ya Tasnifu ........ 112
5.3 Matokeo ya Utafiti ........ 114

5.3.1 Uchanganuzi wa Maudhui ya Kitashtiti ........................................................ 114
5.3.2 Uhakiki wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Gado ....................... 116
5.4 Mapendekezo ........................................................................................... 117
MAREJELEO ................................................................................................ 118
VIAMBATISHO............................................................................................. 125
Kiambatisho I: Barua ya Chuo ...................................................................... 125
Kiambatisho II: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI ......................................... 126

## MAELEZO YA VIFUPISHO

**BH:** Bila Tarehe

**BM:** Boniface Mwangi

**BY:** Baba Yao

**KM:** Kalonzo Musyoka

**MS:** Mike Sonko

**MM:** Musalia Mudavadi

**PI:** Polycarp Igathe

**RO:** Raila Odinga

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Karagosi:** Neno hili lilitumika kumaanisha michoro au picha iliyopigwa chuku na ina mfanano mkubwa wa sura na mtu fulani katika ulimwengu halisi.

**Kejeli**: Neno hili linamaana ya hali yoyote inayodokeza unyume katika tukio, usemi au hali. Vilevile ni neno au tendo la kuonyesha dharau kwa mtu. Hivyo, kutokana na maelezo haya, istilahi hii ilitumika kumaanisha maneno au matendo yenye unyume ndani yake na kazi yake kuu ni kuonyesha dharau.

**Kinaya**: Neno hili limetumika kumaanisha mbinu ya lugha ambayo maana halisi ya maneno au matendo inakinzana au ni kinyume kabisa na maana inayokusudiwa. Neno hili limetumika kumaanisha kutenda mambo kinyume na matarajio. Kwa kawaida, kinaya hutumiwa kuonyesha hali ya utani, kejeli, au kebehi.

**Mikakati ya Kitashiti**: Istihali hii imetumika kumaanisha fani au mbinu za lugha kama zilizojitokeza katika vibonzo kwa minajili ya kuvifanya viwe vicheshi na vyenye kubeza.

**Modi**: Neno modi katika utafiti huu lilitumika kumaanisha matini au michoro katika vibonzo.

**Siasa**: Neno hili lilitumika kumaanisha mfumo wa shughuli, mchakato, na mipango ya kuendesha serikali au jamii. Siasa inahusiana na mbinu za kuongoza, kupanga sera, na kufanya maamuzi katika jamii au nchi. Pia inahusisha jinsi madaraka yanavyotumiwa, kugawanywa, na kupokezwa miongoni mwa watu au vikundi tofauti.

**Tashtiti:** Ni mbinu inayotumiwa na watunzi kutajia yasiyotajika kwa uwazi bila kuchukiza, kuudhi au kuchukuliwa vibaya na msomaji. Katika utafiti huu lilitumika kumaanisha ushambulizi wa watu au taasisi za kisiasa kwa minajili ya kukashifu na kukejeli matendo yao.

**Vibonzo vya kisiasa:** Neno hili lilitumika kumaanisha michoro au picha zinazowasawiri wanasiasa na kukashifu maovu wanayoyatenda pamoja na taasisi za serikali wanazosimamia.

**Wingimodi**: Istilahi hii ilitumika kumaanisha mwingiliano na mkamilishano uliopo

kati ya maneno na picha katika vibonzo vya kisiasa kwa minajili ya kupitisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

### 1.1.1 Tashititi.

Tashtiti ni taaluma au aina ya sanaa inayobeza, kukebehi na kudhihaki watu, taasisi za kijamii na za kisiasa. Ni aina ya ukosoaji ambao huwa na ufanisi mwingi. Tangu enzi za Wagiriki, tashtiti imetumika kukosoa na kubeza mabwenyenye, viongozi na taasisi zinazoendeleza maovu katika jamii. Ingawaje, inaaminika kuwa tashtiti ni modi moja ya ujielezaji iliyoibuka miaka mingi iliyopita, cha kushangaza ni kufikia sasa bado hakujakuwa na uelewano kuhusiana na maana ya dhana ya hiyo. Kwa mfano; Simpson (2003) anaeleza kuwa tashtiti ni taaluma yenye kufuata mpangilio wa njia tatu ambazo zinaweza kubadilishana. Mpangilio huu unahusisha anayetoa maneno, picha au matamshi ya kitashtiti, hadhira ya mtashtiti ambapo hadhira inaweza kuwa wasomaji, watazamaji au hata wasikilizaji, na anayetashtitiwa au kinachotashtitiwa. Wahusika wawili kati ya wahusika hao watatu huwa wameidhinishwa katika tukio la kuzorongeshwa, naye mhusika wa tatu huwa ametengwa katika tukio la kuzorongeshwa. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa anayelengwa au kinacholengwa katika mpangilio huo ndicho huwa kichocheo cha tashtiti.

Isitoshe, Simpson anadai kuwa matini za kitashtiti ni maneno au picha zisizoweza kudadavuliwa kivyake kwa kuwa zimefungamanishwa na muktadha wa hali fulani, wahusika wa diskosi na huwa zimejikita katika uelewa fulani. Hivyo, tunaweza kusema kuwa, ili hadhira iweze kuelewa ujumbe wowote wa kitashtiti, lazima wajitose katika ulingo wa matukio yaliyopo katika jamii. Vilevile, ni sharti hadhira ya vibonzo iweze kutambua muktadha uliomaanishwa na mchora kibonzo.

Tashtiti haiwezi kufaulu kivyake na mara nyingi hutumia mbinu zingine za lugha ili iweze kutambulika. Knight (2004), anadai kuwa tashtiti husawiri "ushambulizi wa ainasafu" ambapo mara nyingi huwa inafaulu kwa kujifanya kuwa kitu kingine. Kwa kawaida, tashtiti hutwaa, kumiliki na kunyonya tanzu zingine kama vile riwaya, hotuba, shairi au hata vipindi vya televisheni. Katika hali hii tashtiti huchukuliwa kama kimelea. Zaidi ya hayo, tunaweza kusema kuwa dhana ya tashtiti ni sawa na dhana ya mwigo wa kubeza, ambayo sifa yake kuu ni mwigo. Aghalabu, tashtiti na mwigo wa kubeza huchukuliwa kama visawe, lakini tofauti iliyopo ni kuwa, mwigo wa kubeza

huwa hauna utepetevu na shurutisho la kutoa makataa kama dhana ya tashtiti. Ni muhimu kufahamu kuwa sio ucheshi wote wa kisiasa hufikia vipimo vya kuwa tashtiti, vivyo hivyo ifahamike kuwa sio kila wakati mwigo wa kubeza huwa wa kitashtiti (Gray, Jones na Thompson, 2009).

Kadhalika, ni vyema kuelewa kuwa kwa muda mrefu kumekuwa na mgogoro kuhusiana na maana ya dhana tashtiti. Kuna wale wanaoshikilia kuwa tashtiti ni mtindo wa mawasiliano (Dorner na Porzelt, 2016), wengine wanadai kuwa tashtiti ni utanzu (Declercq, 2018), lakini ufafanuzi ninaokubaliana nao ni wa Stinson (2019) anayedai kuwa tashtiti ni modi na wala si utanzu na inafanya kazi kwa kushambulia mtu, taasisi, au tabia. Vilevile, tashtiti ni aina ya maandishi au ishara ambazo ni za kimaksudi na huwa na lengo maalum ambalo mara nyingi huwa kukejeli au kukebehi. Hivyo, lengo kuu la tashtiti ni "ushambulizi" wa kimaksudi wenye lengo la kusababisha mabadiliko.

Peifer na Lee (2019) wanadokeza kuwa tashtiti ni taalamu ya kuzorongesha inayochochea mabadiliko katika mfumo wa kijamii na kisiasa kwa njia ya kimzaha. Hivyo, tunaweza kuchukulia tashtiti kama uhakiki wa kisiasa wenye mzaha na unaolenga kufichua upumbavu, unafiki na masuala ya kipuzi miongoni mwa viongozi, serikali au taasisi za kiserikali. Hivyo, ili matini yoyote ile iweze kusemekana kuwa ni ya kitashtiti, ni lazima iwe na msukumo wa kuleta mabadiliko ya aina fulani katika siasa au jamii. Zaidi ya hayo, wawili hawa wanadai kuwa dhana za tashtiti na ucheshi zinachukuliwa kuwa visawe; lakini ukweli ni kuwa, dhana hizi mbili ni tofauti kwa kuwa tashtiti huwa na msukumo wa kutoa changamoto katika sera za kisiasa na za kijamii pamoja na taasisi zake. Hata hivyo, si muhali kupata matumizi ya ucheshi katika kuelezea masuala ya kisiasa, pamoja na wanasiasa au matukio ya kisiasa. Waidha, Peifer na Lee (2009) wanaonya kuwa sio ucheshi wote wa kisiasa huhitimu vipimo vya kuwa katika kategoria ya tashtiti. Hii ina maana kuwa ikiwa matini fulani hainuii kuleta mabadiliko au kutahakiki hali ilivyo, basi haifikii vipimo vya kutambulika kama tashtiti.

### 1.1.2 Vibonzo vya Kisiasa

Dhana ya vibonzo vya kisiasa kama ilivyotumika katika utafiti huu ni michoro iliyo na usawiri bayana wa mtu, watu, tukio au hali ya kisiasa ya nchi fulani. Cha msingi ni kuwa vibonzo vya kisiasa hutoa maoni fiche kuhusiana na masuala ya kisiasa kwa njia yenye kuzua ucheshi. Hata hivyo, lengo kuu la vibonzo vya kisiasa si kuzua ucheshi tu,

bali ni kutashtiti wanasiasa na kuwashawishi walengwa wa vibonzo vile kufuata mkondo wa mawazo wa mchora vibonzo. Kando na kushawishi umma, vibonzo vya kisiasa hunuia kuleta mabadiliko katika uga wa siasa na maisha ya wanajamii. Isitoshe, vibonzo vya kisiasa huwa kama hati ya kihistoria inayoelezea hali ya kisiasa ya nchi fulani katika kipindi fulani.

Sanaa ya uchoraji wa vibonzo vya kisiasa iliibuka kutokana na haja ya kuelezea masuala changamano ya kisiasa kwa njia rahisi na yenye kunata raghba za umma. Haya yanawezekana kutokana na uwezo wa vibonzo kufinya masuala changamano katika picha na maneno yanayoweza kueleweka kwa urahisi. Ventola na wenzake (2004) anadai kuwa sanaa hii ya uchoraji vibonzo ilianza katika karne ya kumi na tano kule Ufaransa. Katika karne ya kumi na saba, kulichipuka tawi la uchoraji wa vikaragosi ambalo ni tofauti kwa kiasi fulani na uchoraji wa vibonzo. Kwa mujibu wa Ventola na wenzake, tofauti iliyopo kati ya sanaa ya ukaragosi na uchoraji vibonzo ni kuwa, ukaragosi ni usawiri uliopigwa chuku wa mtu ilhali uchoraji wa vibonzo ni usawiri wenye chuku wa masuala, matukio au dhana. Kwa upande mwingine, Holysteyn (2017) anaeleza kuwa vibonzo au karagosi ni rasilimali za kijamii zinazoundwa kutokana na matukio ya kijamii na uchoraji wake huongozwa na nia zilizoafikiwa kijamii. Hii ni kumaanisha kuwa, usawiri unaotumika katika vibonzo vya kisiasa hutokana na mazingira au utamaduni wa watu fulani. Kwa mfano, mchora kibonzo akimsawiri mtu kama mwenye sura ya nguruwe, huenda hadhira ikaelewa kuwa ujumbe unaowasilishwa ni kuwa mtu yule ni mlafi na wazo hili linatokana na imani iliyoko katika jamii za kiafrika kuwa nguruwe ni mnyama mlafi.

Kwa kawaida ni vigumu kwa anayechora vibonzo hivi kubaini ikiwa hadhira yake imepata ujumbe uliopo kwenye vibonzo alivyochora kama alivyokusudia. Hali hii inaweza kuzua utata katika ufasiri wa jumbe zilizosimbwa katika vibonzo vinavyochapishwa. Ili hadhira ya mchora vibonzo iweze kupata ujumbe kama ilivyokusudiwa, ni lazima iwe na maarifa ya awali kuhusiana na kinachosawiriwa. Njia moja ya kuisaidia hadhira kuelewa kinachozungumziwa ni matumizi ya maelezo yanayoandamana na picha zilizochorwa au mfanano wa sura unaojitokeza katika vibonzo.

Kwa kawaida, vibonzo vya kisiasa huongoza maoni ya umma kuhusiana na masuala mbalimbali yanayotokea katika maisha ya kila siku ya jamii fulani. Sani na wenzake

(2012) wanadai kuwa vibonzo vya kisiasa hutumika kama chombo cha kusambaza na kuundia ajenda za kijamii kupitia kwa usawiri wa mara kwa mara wa masuala ya kisiasa na ya kijamii katika kipindi fulani. Kutokana na usawiri huu wa mara kwa mara, vibonzo vya kisiasa vya magazetini huelekeza maoni ya umma kuhusiana na suala fulani na vilevile kuwapa jambo la kuzungumzia na kuhakiki. Hili linawezekana kutokana na uwezo wa vibonzo kusimba na kufupisha masuala tata katika picha zinazoweza kueleweka.

Sanaa ya uchoraji vibonzo barani Afrika ilichupika katika miaka ya 1900 katika enzi za ukoloni. Katika eneo la Afrika Mashariki, wakoloni walikuwa na gazeti lao la vibonzo lililoitwa Kronikal. Dhima kuu ya vibonzo vilivyochapishwa kwenye gazeti hili, ilikuwa ni kuwamotisha wanajeshi wa Uingereza kwa kuwasawiri wanajeshi wa Ujerumani kama dhaifu na wanyonge. Kadhalika, Rabe (2018) anasema kuwa kibonzo cha kwanza kuchapishwa Afrika Kusini kilichapishwa kule Uingereza na kilihusu uhuru wa vyombo vya habari mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Hivyo, tunaweza kuchukulia kuwa sanaa ya uchoraji vibonzo ina historia ndefu barani Afrika.

Nchini Kenya, vibonzo vya kisiasa vimekuwepo tangu enzi za ukoloni. Sanaa hii ilianzishwa na Edward Gitau mnamo 1950 alipochapisha vibonzo vilivyojulikana kama Juha Kalulu. Katika miaka ya 1960, Gitau alihamishia kazi zake katika gazeti la Taifa. Baadaye katika miaka ya 1970, kuliibuka mchora vibonzo maarufu Terry Hirst aliyekuwa na gazeti la Joe, na inaaminika kuwa ndiye mwanzilishi wa vibonzo vya kisiasa nchini Kenya (Wanjiru, 2018). Baadaye kulizuka wanavibonzo kama vile; Phillip Ndunguru wa Tanzania, James Tumisiime wa Uganda na Frank Odoi wa Ghana waliojiunga na wanavibonzo wa hapa nchini. Watatu hawa walisifika kwa kazi zao za uchoraji wa vibonzo katika magazeti mbalimbali. Ndunguru alijiunga na gazeti la Kenya Times katika mwaka wa elfu moja mia tisa themanini na tatu na kuanzisha vibonzo vilivyoitwa Kazi bure vilivyoangazia masuala ya kijamii. Naye Tumisiime akajiunga na Daily Nation katika mwaka wa elfu moja mia tisa themanini na sita na alikuwa maarufu kwa vibonzo vilivyokuwa na mhusika maarufu aliyeitwa Bogi Benda. Kwa upande mwingine Frank Odoi alichora vibonzo vya kisiasa katika gazeti la The Nation kuanzia mwaka wa 1979. Kufikia Miaka ya 1980, vibonzo vya mwanzo kuhaririwa viliweza kuchapishwa kwenye magazeti ya kila siku. Hata hivyo, vilidhibitiwa na havingeweza kuangazia masuala tata yaliyohusiana na serikali. Licha

ya kudhibitiwa, wanavibonzo pia hawakuruhusiwa kuchora vibonzo vyovyote vile vilivyohusiana na Rais wa wakati ule Marehemu Daniel Toroitich Arap Moi. Hata hivyo, mwanavibonzo Paul 'Madd' Kalemba anasifika kwa kuwa mwanavibonzo wa kwanza kuchora kibonzo kilichohusu Rais wa wakati huo Marehemu Daniel Toroitich Arap Moi (Wanjiru, 2018).

Kwa kawaida, wanahabari huongozwa na kanuni maalumu katika utendekazi wao. Kanuni hizi, huwa za kusaidia wanahabari kujidhibiti na pia kuwa waadilifu katika kazi zao. Ulimwenguni kote wanahabari wanapaswa kupasha habari kwa njia isiyo na mapendeleo. Hata hivyo, katika bara la Afrika ambako wanahabari hawana uhuru mwingi, wanahabari hulazimika kuchapisha habari zinazopendelewa na mashirika wanayofanyia kazi na mara nyingi hawawezi kuchapisha habari zinazokashifu serikali, viongozi au taasisi za uongozi (Gathara, 2019). Hata hivyo, wanavibonzo wengi barani Afrika hukaidi mtazamo huu kupitia uchoraji vibonzo magazetini na kwenye mitandao. Kwa muda mrefu, kumekuwa na mikwaruzano kati ya wanavibonzo na baadhi ya wanasiasa katika nchi mbalimbali barani Afrika, kwa sababu ya uchapishaji wa vibonzo vinavyokashifu viongozi. Kwa mfano, katika mwaka wa 1998 Paul-Louis Nyemb Ntoogué almaarufu "Popoli" mchora vibonzo wa gazeti la Le Messager nchini Cameroon, alilazimika kuwa mkimbizi na kutorokea Afrika Kusini baada ya kuchora vibonzo vilivyokashifu uongozi wa Rais wa wakati ule Paul Biya. Haya ni baadhi ya mambo ambayo wanavibonzo wa Kiafrika hukumbana nayo katika harakati zao za kuhamasisha umma kuhusu masuala yanayotokea katika ulimwengu wa kisiasa. Ni kutokana na mikwaruzano hii, ndipo wanavibonzo wengi waliamua kuhamisha kazi zao kutoka magazetini hadi kwenye mitandao ya kijamii, ambako hakuna udhibiti kutoka kwa serikali au mashirika wanayofanyia kazi.

### 1.1.3 Vibonzo na Mtandao

Kwa muda mrefu vibonzo vya kisiasa vimetumika katika magazeti na majarida kama njia ya kuwasilisha hoja ambazo kwa kawaida ni vigumu kuwasilishwa kwa njia iliyo wazi. Kwa karne nyingi, vibonzo vilijumuisha mojawapo wa vipengele muhimu katika magazeti na majarida. Hata hivyo, kutokana na utandawazi na harakati za kutafuta uhuru wa kujieleza, baadhi ya wanavibonzo wamebadili mkondo na kuanza kuchapisha vibonzo vyao katika mitandao yao ya kibinafsi. Ifahamike kuwa wanavibonzo wa Kiafrika wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira yenye uhasama na udhibiti

mkubwa kutoka kwa serikali, pamoja na mashirika ya magazeti nchini. Kutokana na hali hii, wengi wao wamemudu hali ya kujidhibiti wenyewe. Hata hivyo, kwa wale ambao kazi zao zinaonekana kana kwamba zinawashutumu wanasiasa na matajiri nchini, wanavibonzo hawa hujipata kwenye mashaka ya kufunguliwa mashtaka na kufungwa gerezani. Udhibiti na uhasama huu, umepelekea wanavibonzo wengi kubadili modi ya kuchapisha vibonzo vyao kutoka magazetini; ambapo kuna udhibiti mkubwa hadi mtandaoni ambapo kuna uhuru mkubwa wa kujieleza (Eko, 2015).

Kutokana na udhibiti uliopo katika magazeti, baadhi ya wanavibonzo wametafuta njia mbadala ya kuelezea masuala ambayo kwa kawaida ni vigumu kuyaeleza wazi wazi. Kwa mfano, mwanavibonzo maarufu Gado, licha ya kuwa na tajriba ya miaka mingi katika sanaa ya uchoraji vibonzo, alijipata katika mkwaruzano na serikali, kwa sababu ya vibonzo alivyochapisha. Hali hii ilipelekea kupigwa marufuku kwa baadhi ya vibonzo alivyochapisha katika magazeti ya hapa nchini na hatimaye kuachishwa kazi katika gazeti la Daily Nation. Kutokana na hali ya kukandamizwa na kunyimwa haki ya kujieleza kama mwanahabari, Gado alianzisha tovuti yake (ww.gadocartoons.com) ambapo ana uhuru wa kuchapisha vibonzo vyake bila woga wa kufutwa kazi au vibonzo vyake kupigwa marufuku. Uhamisho huu kutoka magazetini hadi kwenye mitandao ndio uliompa mtafiti mshawasha wa kuchunguza mikakati ya kitashtiti inayotumika katika vibonzo vya mtandaoni na ikiwa mikakati inayotumika katika mtandao ni tofauti na ile ya magazetini na kwa njia ipi. Kando na hayo, mtafiti alinuia kuchunguza ikiwa mikakati ya kitashtiti iliyotumika katika vibonzo vilivyochapishwa kwenye mtandao, vilisaidia katika kuongeza makali na uhuru katika uangaziaji wa masuala mbalimbali.

Hivyo basi, utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa maudhui ya kitashtiti pamoja na mikakati iliyotumika kuendeleza maudhui hayo ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa vilivyochapishwa kwenye mtandao. Kwa vile kuna vibonzo vingi vinavyochapishwa mtandaoni kila siku, utafiti huu ulijikita katika vibonzo vilivyochapishwa na mchora vibonzo Godfrey Mwampembwa almaarufu Gado katika tovuti yake www.gadocartoons.com katika mwaka wa 2017.

## 1.2 Suala la Utafiti

Watafiti wengi wa awali walioshughulikia vibonzo vya kisiasa walizingatia masuala kama vile; wingimodi katika vibonzo vya kisiasa, maudhui yanayojitokeza katika vibonzo, dhamira ya mchora vibonzo vya kisiasa, umuhimu wa vibonzo vya kisiasa na

hata jinsi ucheshi unavyojitokeza katika vibonzo hivi. Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa suala la vibonzo vya kisiasa si geni katika uwanja wa utafiti. Hata hivyo, katika karne hii ya utandawazi na hasa kuanzia mwaka wa 2005, wanavibonzo kama vile Gado, Eric Gammz Igah na Paul Maddo aghalabu hutumia mitandao yao ya kibinafsi kuchapisha baadhi ya vibonzo ambavyo vilikuwa vimepigwa marufuku katika mashirika ya magazeti waliyofanyia kazi. Kwa kawaida, wanahabari hufanya kazi kwa kuzingatia kanuni za shirika wanalofanyia kazi. Hivyo, ni vigumu kwao kusawiri masuala yanayoikumba nchi kwa njia iliyo wazi kutokana na hali ya kudhibitiwa na mashirika wanayofanyia kazi. Kutokana na hali hii, ni dhahiri kuwa uhamisho wa sanaa ya uchoraji vibonzo vya kisiasa kutoka magazetini hadi kwenye mitandao ya kijamii na tovuti za kibinafsi, umepelekea wanavibonzo kuongeza makali katika uangaziaji wa masuala mbalimbali ya kisiasa kwa kuwa, hamna udhibiti mkubwa katika mitandao yao ya kibinafsi. Uhuru huu mpya unawawezesha kuangazia maswala kwa njia iliyo wazi na huru. Ni kutokana na hali hii, mtafiti alipata mshawasha wa kuchunguza jinsi uhuru huu mpya pamoja na kuongezeka kwa makali katika usawiri wa maswala ya kisiasa nchini kunavyoendeleza maudhui ya kitashtiti, pamoja na mikakati inayotumiwa na wanavibonzo, hasa Gado kuendeleza maudhui hayo ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa vinavyochapishwa kwenye mitandao ya kijamii na tovuti za watu binafsi.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

1. Kuchanganua maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyochapishwa mtandaoni katika mwaka wa 2017
2. Kuhakiki mikakati iliyotumika katika kuendeleza maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyochapishwa mtandaoni katika mwaka wa 2017

## 1.4 Maswali ya Utafiti

1. Je, ni maudhui yepi ya kitashtiti yaliyopo katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyochapishwa mtandaoni katika mwaka wa 2017
2. Je, ni mikakati ipi iliyotumika katika kuendeleza maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyochapishwa mtandaoni katika mwaka wa 2017?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Mtafiti alipata motisha wa kutafitia mada hii kutokana na baadhi ya vibonzo vya kisiasa kuhamishwa kutoka magazetini hadi kwenye mitandao ya kibinafsi. Uhamisho huu,

umepelekea kuwepo kwa uhuru mwingi wa kujieleza miongoni mwa wanavibonzo. Kutokana na hali hii, wanavibonzo wameongeza makali katika mbinu wanazotumia kueleza masuala yenye ubishi yanayohusiana na siasa. Kutokana na umaarufu wa vibonzo vya kisiasa hatuwezi kusema kuwa tumeyajaza mapengo yote ya kiutafiti yanayohusiana na suala hili. Hivyo basi, utafiti huu ulinuia kuongeza maarifa na kuziba pengo lililopo la ukosefu wa tahakiki tosha katika nyanja za semiotiki, wingimodi, tashtiti na uhamiaji wa vibonzo katika uwanda wa mitandao kwa kuangazia mada mpya katika tanzu ya diskosi ambayo bado haijatafitiwa kwa kina.

Matokeo ya utafiti huu, yatasaidia watafiti wengine kutambua kuwa maudhui yanayojitokeza katika vibonzo vya kisiasa, aghalabu huwa ya kuweka wazi maovu yanayojitokeza katika mazingira ya msanii, na dhima kuu ya maudhui haya ni kutashtiti watu, tabia fulani au taasisi mbalimbali. Pili, utafiti utaongeza maarifa kuhusiana na suala la uhamiaji wa vibonzo katika mitandao ya kijamii na tovuti za kibinafsi pamoja na sababu zinazopelekea uhamiaji huu. Vilevile, utafiti huu utasaidia katika kuelewa wingimodi katika vibonzo na jinsi wingimodi huchangia katika kukuza mikakati tofauti ya kitashtiti inayosimba maudhui yanayohusiana na jamii au mazingira ya mchora vibonzo. Hali kadhalika, mtafiti alinuia kutoa mchango katika usomi wa vibonzo kwa kutoa mwelekeo wa kinadharia kwa utanzu wa vibonzo kupitia uchambuzi wa kisemiotiki kwa minajili ya kubainisha na kuelewa mikakati inayotumika katika uchoraji vibonzo ili kuvifanya viwe vya kitashtiti.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika vibonzo vya kisiasa vilivyochorwa na Godfrey Mwampembwa au kwa jina lake la lakabu Gado vilivyochapishwa katika tovuti yake ya www.gadocartoons.com katika mwaka wa 2017 na hasa vilivyohusu nchi ya Kenya. Katika mwaka wa 2017, Gado alikuwa amechapisha jumla ya vibonzo sitini katika tovuti yake na kutokana na jumla hii, mtafiti aliteua kimakusudi vibonzo ishirini vilivyounda data ya utafiti huu. Kuna sababu kadha wa kadha zilizompelekea mtafiti kujikita katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyochapishwa kwenye tovuti yake ya kibinafsi.

Kwanza kabisa, ni kwa sababu Gado alikiuka mfumo wa kudhibitiwa na kuanza kuchapisha vibonzo vilivyopigwa marufuku katika tovuti yake wa kibinafsi. Ni kutokana na hali hii, mtafiti alikisia kuwa angepata vibonzo vyenye makali na ambavyo

havikuwa vimedhibitiwa na taasisi za serikali au hata vyombo vya habari. Pili, mtafiti aliteua kimakusudi vibonzo ishirini kutokana na sampuli pana ya vibonzo sitini kwa kuwa alichukulia kuwa vibonzo ishirini vilivyopangwa kulingana na maudhui mbalimbali vingeunda data pana na toshelevu ya kufaidi utafiti huu. Isitoshe, katika uteuzi wa vibonzo hivi ishirini, mtafiti alijikita katika vibonzo vilivyofungamana na madhumuni ya utafiti huu na vile vilivyohusu nchi ya Kenya.

Sababu ya tatu iliyompelekea mtafiti kuchagua vibonzo vya Gado ni kwa sababu ana tajriba ya miaka ishirini na saba katika sanaa ya uchoraji vibonzo vya kisiasa na hivyo ilichukuliwa kuwa kazi zake zina weledi unaotokana na miaka mingi ya usawiri wa masuala ya kisiasa nchini Kenya na ulimwenguni. Hali kadhalika, mtafiti alichagua kipindi cha mwaka wa 2017 kwa kuwa alikisia kuwa angepata data pana na toshelevu kwa kuwa katika kipindi hiki kulikuwa na uchaguzi mkuu baada ya mfumo wa serikali za kaunti kuanzishwa katika mwaka wa 2013. Hivyo, mtafiti alichukulia kuwa angepata data changamano kutokana na hali na matukio changamano yaliyokuwa yakitokea katika mazingira ya kisiasa nchini Kenya. Vilevile, utafiti huu ulijikita katika nadharia ya Semiotiki ambayo ilichukuliwa kuwa faafu katika uchanganuzi wa masuala ya lugha na ishara katika vibonzo vilivyoteuliwa kwa minajili ya utafiti huu.

Hali kadhalika, kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika vibonzo vilivyochapishwa kwenye tovuti ya Gado katika mwaka wa 2017 na hasa vilivyohusu nchi ya Kenya, mwelekeo huu ulizuia uwezo wa kuchunguza jinsi mikakati ya kitashtitti ya Gado imebadilika kwa muda au katika kipindi fulani. Hivyo, hitimisho lililotolewa huenda lisionyeshe mitindo ya muda mrefu au mabadiliko katika mtindo wake. Kando na hayo, uchambuzi wa vibonzo huhusisha kiwango fulani cha maoni ya kibinafsi, kwani ucheshi, kejeli, na ukosoaji wa kisiasa katika vibonzo zinaweza kutafsiriwa kwa njia tofauti na hadhira mbalimbali. Ingawa juhudi zilifanywa kuhakikisha usawa wa maoni, uchambuzi huu huenda uliakisi upendeleo wa mtazamo wa mtafiti mwenyewe.

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inajumuisha mapitio ya maandishi ya tafiti za awali zilizohusiana na kukaribiana na utafiti huu. Sura hii ilishughulikia yaliyoandikwa kuhusiana na vibonzo, maudhui yanayojitokeza katika vibonzo vya kisiasa, tashtiti na mikakati ya lugha inayoibua tashtiti. Lengo kuu la udurusu huu, lilikuwa ni kuonyesha mshabaha na tofauti iliyopo kati ya utafiti huu na tafiti zingine za awali na hatimaye kujaza pengo la kiusomi. Sehemu ya pili ya sura hii ilijishughulisha na maelezo kuhusiana na nadharia ya Semiotiki pamoja na mihimili yake. Zaidi ya hayo, ni katika sehemu hii mtafiti alionyesha umuhimu wa nguzo mbalimbali za nadharia ya Semiotiki katika utafiti huu na jinsi nguzo hizo zilivyomsaidia mtafiti katika uchanganuzi wa data iliyoteuliwa.

### 2.2 Mapitio ya Maandishi

Mapitio ya maandishi yalipangwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Kwanza, mtafiti alitahakiki kazi zilizohusu maudhui katika vibonzo vya kisiasa. Katika sehemu iliyofuata, mtafiti alichanganua kazi zilizohusu mikakati iliyotumika kuendeleza maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa. Kazi zilizopitiwa ni za kimataifa, kimaeneo, kikanda na pia za humu nchini kwa sababu vibonzo hutumika kote ulimwenguni.

#### 2.2.1 Maudhui katika Vibonzo vya Kisiasa

Maudhui kwa jumla ni jumbe shamiria, masuala au mawazo yanayojitokeza katika mawasiliano ya aina yoyote ile. Aghalabu maudhui huwa yamefungamanishwa na falsafa ya msanii, mazingira anamoishi msanii na utamaduni wa jamii yake. Nkumbo (2019) anaeleza kuwa maudhui ni jumla ya mambo yanayofafanuliwa na kujitokeza katika mawasiliano ya aina yoyote ile. Kwa kawaida, maudhui hujumuisha dhamira, mtazamo, msimamo, ujumbe au falsafa ya msanii anayewasilisha kazi ile. Zaidi ya hayo, ni kwamba maudhui ya kazi yoyote ile ya kisanii ni zao la hali ya jamii ya msanii, kwa kuwa vibonzo vya kisiasa ni zao la kisanii, huwa vimebeba jumbe kuhusiana na mazingira ya msanii anayevichora na pia huonyesha msimamo wake kuhusiana na suala analosawiri.

Kwa mujibu wa Dugalich (2018) vibonzo vya kisiasa hujikita kwenye muktadha fulani. Vibonzo hivi huwa vinaakisi hali halisi na masuala yanayojitokeza katika jamii. Ni

muhimu kufahamu kuwa, vibonzo pia huchangia katika diskosi ya umma, na huwasaidia wasomaji katika kuelewa na kutoa uamuzi kuhusu miingiliano changamano inayofanya kazi katika mifumo ya kisiasa na ya kijamii. Kutokana na hali hii, vibonzo vya kisiasa hutumika kama vyombo muhimu vya kusambaza jumbe mbalimbali pamoja na kuelekeza majadiliano yanayohusiana na masuala ya kijamii. Mtafiti alikubaliana na mawazo ya Dugalich kwa kuwa vibonzo vilivyotumika katika utafiti huu, vilisheheni masuala yaliyokuwa yanatendeka nchini Kenya katika mwaka wa 2017. Isitoshe, vibonzo hivi vilichangia diskosi ya umma kutokana na usawiri wake wa viongozi mbalimbali wa nchi ya Kenya na ofisi walizoshikilia. Kutokana na usawiri huo, majadiliano kuhusiana na masuala yaliyokumba jamii ya nchi ya Kenya yalijitokeza katika utafiti huu.

Ni muhimu kuelewa kuwa vibonzo vya kisiasa ni aina ya sanaa na kama sanaa zote zingine, vibonzo huwa vimefungamanishwa na maoni ya anayevichora. Hess na Northrop (2011) wanasisitiza kuwa mchora vibonzo aliyebobea ni yule anayeweza kufungamanisha sanaa anayoifanya na maoni au mawazo yake kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, wanaeleza kuwa vibonzo vya kisiasa aghalabu huwa vyenye hisia hasi, ubeuzi na vyenye kuhakiki. Lengo kuu la mchora vibonzo ni kuchochea fikira za hadhira yake katika kuunga mkono mkondo wa mawazo yake. Uhakiki wa wazi na kweli unapaswa kuwa kigezo muhimu cha kumwongoza mchora vibonzo yeyote yule. Kutokana na maelezo ya Hess na Northrop, mtafiti aliweza kutambua maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo alivyoteua kwa kutambua na kutathmini maoni yaliyosimbwa katika vibonzo vile.

Kwa kawaida, kuna mambo ya kimsingi yanayojitokeza katika vibonzo vya kisiasa nayo ni kama vile; masuala ya kisiasa, udokezi wa kitamaduni, hali zinazokumba jamii fulani na hulka za watu binafsi. Medhurst na Desousa (1982) walionyesha jinsi vibonzo vya kisiasa vilivyotumika katika kampeni za urais nchini Marekani katika miaka ya 1980. Walidai kuwa maudhui yaliyoshamiri katika kipindi hiki cha kampeni yalijitokeza katika njia nne. Kwanza, matukio ya kisiasa yaliyokuwa yakitendeka. Pili, vibonzo vilivyofungamanishwa na hulka za wanasiasa waliokuwa wanawania urais kwa kupigwa chuku kwa sifa zao za kisaikolojia au za kimwili. Tatu, matukio yaliyotokea katika kipindi cha kampeni na mwisho, udokezi wa kitamaduni uliojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa. Utafiti huu wa Medhurst na Desousa ulitoa mwongozo

mwafaka katika kutambua maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vya Gado vilivyochapishwa kwenye tovuti yake mintarafu ya masuala yale manne ya kimsingi yanayojitokeza katika vibonzo vya kisiasa.

Kwa upande mwingine, vibonzo vya kisiasa vinaweza kutumika kama mbinu ya mawasiliano ya kisiasa (Onakpa, 2014). Katika uchunguzi wake, Onakpa alidai kuwa vibonzo vya kisiasa hutumika kama silaha madhubuti inayoangazia masuala ya kisiasa. Hali hii inatokana na uwezo wake wa kujenga taswira zinazodumu akilini mwa wasomaji wake. Matokeo ya utafiti wake yalithibitisha kuwa vibonzo vya kisiasa hutumika katika kuunda ajenda zinazotawala mazungumzo na maoni ya wananchi. Utafiti wa Onakpa ulikuwa muhimu katika utafiti huu, kwa kuwa ulitoa mwongozo mwafaka kuhusiana na utambuzi wa maudhui yanayojitokeza kwenye vibonzo, kwa kutambua ajenda zinazotokana na vibonzo vilivyochorwa. Hata hivyo, utafiti wa Onakpa ulitofautiana na utafiti huu kwa kuwa ulijikita katika kuchunguza jinsi vibonzo vya kisiasa huunda ajenda zinazoshamiri katika mawasiliano ya umma, ilhali utafiti huu, ulibainisha na kuchunguza maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vya kisiasa vya Gado. Kadhalika, mtafiti alifanya uhakiki wa kisemiotiki kwa minajili ya kutambua mikakati ya kitashtiti iliyotumika katika vibonzo vya Gado.

Dweich na Wenzake (2022) aliangazia jinsi itikadi za kijamii na kisiasa huundwa kupitia vibonzo vya magazeti. Katika utafiti wake, Dweich na wenzake walihakiki jinsi itikadi na lugha katika vibonzo vya kisiasa vya Nigeria husawiri watu wa Nigeria kama wenye kutilia maanani itikadi za vikundi kuliko maslahi ya kitaifa. Matokeo ya utafiti huo, yalionyesha ushamiri wa ukabila kutokana na ukosefu wa itikadi za pamoja zinazoongoza nchi ya Nigeria. Utafiti wa Dweich na wenzake ni tofauti na utafiti huu, kwani E kudhihirisha itikadi katika jamii fulani na hatimaye kuweka wazi maudhui yaliyoshamiri katika jamii hiyo. Hata hivyo, utafiti huu ulichunguza mikakati ya kitashtiti ambayo hujitokeza katika vibonzo vya kisiasa vinavyochapishwa mtandaoni ili kuchangia diskosi ya vibonzo kwa kuangazia uhamiaji wa vibonzo vya kisiasa kutoka mfumo wa uchapishaji wa magazetini hadi kwenye mtandao.

Kando na hayo, vibonzo vya kisiasa vimetumika katika kuunda na kukuza utambulisho wa watu fulani kama alivyothibitisha Najjar (2007) alipohakiki vibonzo vya mwanavibonzo maarufu kutoka Palestina, Naji al-Ali. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha jinsi vibonzo vya kisiasa vinavyotumika katika kuunda utambulisho wa

watu kupitia sifa bainifu kama vile; mavazi yao, umbo la miili yao, tabia na utamaduni wao. Hivyo, maudhui tawala katika utafiti huo wa Najjar ni utamaduni wa wakimbizi wa Kipalestina. Ingawa, mawazo ya Najjar yanatoa mwongozo mwafaka katika utafiti huu, tofauti iliyojitokeza kati ya utafiti wa Najjar na utafiti huu, ni kuwa Najjar alijikita katika kuchunguza utambulisho wa watu fulani kwa kuhakiki maisha na utamaduni wao ilhali utafiti huu, ulilenga kuchunguza mikakati iliyoendeleza maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa kwa kuchunguza lugha na ishara zinazotumika katika vibonzo vya kisiasa.

Eko (2007) alichunguza jinsi wanavibonzo wa kisiasa wanavyotumia sanaa ya uchoraji vibonzo kuwasawiri viongozi wanne wa Kiafrika kwa njia isiyo ya kibinadamu. Katika utafiti wake, Eko aliangazia suala la uongozi mbaya kwa kuwasawiri viongozi hawa wanne kama wanyama. Utafiti wake uliweka wazi mbinu inayotumiwa na wanavibonzo ya kuwapa binadamu sifa za wanyama kwa minajili ya kutashtiti unyama na ukatili unaojitokeza katika uongozi wao. Eko alilinganisha dhana ya unyama na ukatili na uongozi wa kiimla. Pamoja na hayo, alitumia mawazo ya Foucault kuhusu uongozi kudhihirisha uhusiano uliopo kati ya serikali na watawaliwa. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kuwa katika serikali za kiimla masuala ya uongozi mbaya hujitokeza na kwa upande mwingine, watawaliwa husawiriwa kama walio kwenye harakati za kujikomboa kutokana na uongozi mbaya. Utafiti wa Eko, ulifanana kwa kiasi kikubwa na malengo ya utafiti huu, lakini tofauti iliyojitokeza ni kuwa, Eko alizingatia suala moja la uongozi wa kiimla na mbinu zilizotumika kuendeleza maudhui hayo. Halikadhalika, utafiti huu ulinuia kuchunguza mbinu tofauti zinazotumika kuendeleza maudhui mbalimbali katika vibonzo vya kisiasa vya msanii Gado. Hata hivyo, utafiti wa Eko ulitoa mwongozo mwafaka katika utafiti huu.

Vibonzo vya kisiasa huwa vimebeba jumbe maridhawa ambazo mchora vibonzo hunuia kupitisha kwa hadhira yake. Hivyo basi, suala la nia ya mchora kibonzo hujitokeza. Utafiti wa Mulanda na Telewa (2014) uliangazia nia ya mwanavibonzo Gado katika sanaa yake ya uchoraji vibonzo vya kisiasa. Kulingana nao, Gado alidai kuwa katika kazi yake ya uchoraji vibonzo, yeye husawiri maoni ya kampuni ya vyombo vya habari anayofanyia kazi na wakati mwingine usawiri wake huhusu maoni yake binafsi. Watafiti hawa walidai kuwa taaluma ya uchoraji vibonzo vya kisiasa kwa kiasi kikubwa ni sawa na utoaji maoni ya kibinafsi kuhusu masuala ya kisiasa. Hivyo, maoni ya

mchora vibonzo huhusu masuala yanayotokea katika mazingira ya kisiasa ya nchi fulani na huakisi maoni yake. Cha msingi ni kuwa, maudhui yanayojitokeza kwenye vibonzo vya kisiasa huwa yamefungamana na maoni, mawazo na falsafa ya mchora vibonzo. Utafiti huo wa Mulanda na Telewa, ulitofautiana na utafiti huu kwa kuwa, matokeo yao yalithibitisha kuwa vibonzo vilivyochorwa magazetini vilikuwa vimefungamanishwa na maoni ya kampuni ya vyombo vya habari alivyofanyia kazi, ilhali utafiti huu unanuia kuthibitisha kuwa vibonzo vya Gado vinavyochapishwa mtandaoni husheheni maoni yake binafsi na hivyo huwa havijadhibitiwa na yeyote yule.

Kwa kuwa vibonzo vya kisiasa ni sanaa inayolenga kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira yake, basi vinaweza kuathiri maoni ya umma kuhusiana na jambo fulani linalomulikwa na mchora kibonzo. Chonka (2016) aliangazia jinsi mchora vibonzo wa Somali Amin Amir alivyoweza kuathiri maoni ya hadhira yake, kupitia uchapishaji wa vibonzo vya kisiasa kupitia mtandao wake wa kibinafsi. Kwa mujibu wa Chonka, vibonzo vya Amir huwavutia wananchi wengi wa Somali licha ya kuwa Wasomali wamegawika na kutengana kwa misingi ya kikabila na kisiasa. Chonka alidai kuwa kupitia vibonzo vinavyochapishwa kwenye mtandao wake, Amin huweza kuathiri maoni ya umma kuhusiana na masuala mbalimbali kama vile; ufisadi, vurugu za kisiasa, ubaguzi wa kiukoo, na misukumo ya mara kwa mara kutoka nchi za nje. Kufanikiwa kwa sanaa yake kunatokana na usawiri wake usioonekana kuegemea upande wowote wa kisiasa au kikabila. Utafiti wa Chonka ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa uliangazia uundaji wa ajenda na kuathiriwa kwa maoni ya umma kupitia vibonzo vya kisiasa vinavyochapishwa mtandaoni na hasa kutoka kwa mtu ambaye haishi katika nchi anayosawiri. Hivyo inaonekana kana kwamba anatoa maoni yasiyoegemea upande wowote wa kisiasa au kikabila.

Otumwa (2019) alitafitia mbinu na maudhui yaliyojitokeza kwenye vibonzo vya kisiasa katika gazeti la Taifa Leo kati ya mwaka wa 2013 na 2014. Otumwa aligundua kuwa maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo hivyo yalihusiana na siasa, ufisadi, ukosefu wa usalama, ukabila, elimu na kazi. Kutokana na matokeo ya utafiti wake, maudhui ya ufisadi yalichukua asilimia ishirini na sita ya maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa. Hivyo basi ilichukuliwa kuwa suala la ufisadi lilisheheni asilimia kubwa ya vibonzo vya wakati ule kwa kuwa hayo ndiyo yaliyokuwa yakitokea katika mazingira ya mchora vibonzo. Utafiti wa Otumwa ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa,

Otumwa alijikita katika mitindo ya lugha iliyotumika katika vibonzo vya kisiasa vilivyochapishwa katika gazeti la Taifa Leo, ilhali utafiti huu ulikuwa unahakiki lugha pamoja na ishara zilizotumika kwenye vibonzo vya kisiasa vya mitandaoni ili kutambua mikakati ya kitashtiti inayojitokeza katika vibonzo vya kisiasa vya mtandao.

### 2.2.2 Mikakati Inayoendeleza Maudhui ya Kitashtiti

Sifa moja ya vibonzo vya kisiasa ni kuwa lazima viwe vya kitashtiti na kazi yake kuu ni kukejeli wanaosawiriwa kwa minajili ya kuchochea mabadiliko fulani. Ndiposa vibonzo hivi viweze kusemekana kuwa ni vya kitashtiti, kuna mambo yanayotumiwa na mchora vibonzo kwa minajili ya kuibua tashtiti. Katika sehemu hii mtafiti alidurusu tafiti za wengine ili kuelewa ni mambo au fani zipi hutumika katika kuibua tashtiti katika kazi yoyote ile ya kisanaa.

Sani na Yar'duwa (2014) waliangazia uundaji wa tashtiti katika vibonzo vya magazeti nchini Nigeria. Walichunguza maneno yaliyotumika kwenye vibonzo vya kisiasa vya nchi ile, kwa kuunda topoi za kileksia kwa minajili ya kutambua vipengele vya kileksia and matumizi yake katika matini zilizotumika katika vibonzo vile. Wawili hawa walidhihirisha kuwa, wanavibonzo wa Nigeria hutumia vihisishi kuwatashtiti viongozi wa kisiasa. Japo, utafiti wa Sani na wenzake ulitoa mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa kuonyesha jinsi vihisishi vinavyotumika katika uundaji wa tashtiti, utafiti wa Sani na Yar'duwa uliwacha pengo la kiusomi kwa kuwa ulijikita kwenye uhakiki wa matumizi ya lugha katika vibonzo. Pengo ambalo mtafiti alikusudia kuziba kwa kuhakiki ishara zote za kiisimu (michoro na maneno) katika uendelezaji wa tashtiti.

Kwa upande mwingine, (2007) alitafiti jinsi viongozi wa Kiafrika walivyosawiriwa katika magazeti teule nchini Senegal, Cameroon, Burkina Faso na Kenya katika kipindi cha baada ya vita baridi vya dunia. Mtafiti huyu alielezea kuwa kutokana na sampuli ya vibonzo alivyoteua, viongozi wa Kiafrika katika kipindi cha baada ya vita baridi vya dunia walisawiriwa kama wanyama wa pori. Eko aligundua kuwa wanavibonzo hutumia visasili vya Kiafrika, kuwasawiri viongozi kama wanyama wa msituni kutokana na wanavyotendea watawaliwa wao unyama. Mawazo ya Eko yalitoa mchango maridhawa katika utafiti huu kwa kuonyesha jinsi tanzu za fasihi ya Kiafrika, zinavyotumika kutashtiti viongozi wa kisiasa.

Kando na hayo, Sani na Yar'aduwa (2014) walieleza kuwa sitiara za kuonekana na za kunenwa zinatumika katika kuunda tashtiti katika vibonzo vya kisiasa nchini Nigeria. Utafiti wao ulidokeza kuwa sitiara za kuonekana ni balagha inayoteka raghba za wasomaji kuliko sitiara za kunenwa. Utafiti wa wasomi hawa wawili ulithibitisha kuwa toni iliyotumika katika vibonzo vya kisiasa ni yenye kuibua ucheshi. Kando na hayo, walidai kuwa mwingiliano kati ya mbinu za kutamkwa na za kuonekana husaidia katika kuibua dhana ya sitiara inayotumika kukejeli maovu katika siasa na jamii. Utafiti huo ulitoa mchango mkubwa katika kudhihirisha tashtiti kupitia sitiara. Hata hivyo, kazi hii ilitofautiana na utafiti huu kutokana na hali kwamba, watafiti hawa walijikita katika uhakiki wa sitiara kama njia ya kuunda tashtiti ilhali utafiti huu ulijikita katika uhakiki wa modi za kisemiotiki kwenye vibonzo vya kisiasa kwa minajili ya kutambua mikakati ya kitashtiti iliyojitokeza katika vibonzo vilivyoendeleza maudhui mbalimbali ya kitashtiti.

Al- Momani, Badarneh na Migdadi (2017) walifanya uhakiki wa kisemiotiki wa vibonzo vya kisiasa kule Jordan baada ya mwamko wa mwaka wa 2011 Uarabuni. Utafiti wao ulidhihirisha kuwa vibonzo vilivyochapishwa katika kipindi hiki, vilitumia mbinu za lugha kama vile; ucheshi, mchezo wa maneno, polisemia, mwingiliano matini, ubadili msimbo, udokezi na ukopaji kutoka kwa utamaduni ili kukejeli na kutashtiti uongozi na hali ya kisiasa katika nchi ya Jordan. Utafiti huu wa Al-Momani na wenzake ulifanana kwa kiasi kikubwa na utafiti huu lakini tofauti iliyopo ni kuwa; katika uchunguzi wao watafiti walitafitia mikakati ya lugha na ishara zilizotumika katika maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa.

Pamoja na hayo, Kondowe na wenzake (2014) walithibitisha jinsi sifa za kunenwa na zisizo za kunenwa katika vibonzo vya kisiasa zinavyotumika katika kusawiri viongozi wa kisiasa nchini Malawi. Katika utafiti wao, walitumia vibonzo vilivyomsawiri rais wa wakati huo Joyce Banda. Walibainisha kuwa wanavibonzo wa Malawi aghalabu huvunja, kupuuza au kutofuata kanuni shirikishi za mazungumzo katika uangaziaji wa masuala ya kisiasa nchini Malawi. Kulingana na watafiti hawa, mbinu ya kuvunja kanuni shirikishi za mazungumzo ilijitokeza zaidi katika uchambuzi wa vibonzo vya kisiasa vilivyoteuliwa. Matokeo ya utafiti wao, yalidhihirisha kuwa wanavibonzo hutoa habari zisizokuwa kamilifu, kama mkakati wa kuepuka hali ya kutoa makataa na kama mbinu ya kuifanya hadhira yao kuunda uelewa wao kuhusiana na masuala ya kisiasa

nchini mwao. Utafiti wa Kondowe na wenzake ulitofautiana kwa kiasi kikubwa na utafiti huu kwa kuwa ulijikita katika kuchambua sifa za kiisimu zilizojitokeza kwenye vibonzo vya kisiasa mintarafu ya kanuni shirikishi za mazungumzo za Grice, ilhali utafiti huu ulijikita katika uchambuzi wa kisemiotiki wa vibonzo vya kisiasa kwa minajili ya kutambua mikakati ya kitashtiti iliyotumika katika vibonzo ili kuvifanya viwe vya kitashtiti.

Kessler (2022) alichunguza jinsi matumizi ya picha na maneno hushirikiana katika kuwasilisha jumbe za kitashtiti kwa hadhira lengwa. Alipendekeza uainishaji wenye tanzu saba kuu ambazo hueleza jinsi picha na maneno hushirikiana ili kuwasilisha jumbe za kitashtiti kwa msomaji. Tanzu alizoainisha ni kama zifuatavyo; utanzu wa kwanza ni pale ambapo picha huelezea matini iliyo kamili. Utanzu wa pili, ni ule ambao maneno huongezwa "vipovu vya sauti" kwa yale msomaji anayoyaona. Utanzu wa tatu ni pale ambapo picha na maneno huwasilisha ujumbe mmoja, wa nne ni pale ambapo, aidha picha au maneno hutoa maelezo zaida kuhusu aidha picha au maneno yaliyotumika. Utanzu wa tano ni pale ambapo maneno na picha zilizotumiwa hazihusiani kwa vyovyote vile na aghalabu huwa vinazungumzia jumbe tofauti. Utanzu wa sita ulihusu hali ya maneno kuwa sehemu muhimu ya picha zilizochorwa na utanzu wa mwisho ulihusu picha na maneno kutegemeana na kushirikiana kwa minajili ya kusambaza ujumbe fulani. Kutokana na maelezo ya Kessler, mtafiti alipata mwelekeo na nguzo muhimu zilizomsaidia katika kuhakiki uhusiano uliokuwepo kati ya picha na maneno katika vibonzo vya kisiasa alivyoteua.

Zaidi ya hayo, Strainbrook (2013) alieleza kuwa hadithi za vibonzo husawiri matini changamano ambayo inamfanya msomaji kuelewa na kufasiri ishara zilizotumiwa. Msomaji huafikia hali hii kwa kuunganisha maneno yaliyotumiwa ili kuelewa ishara au picha zilizochorwa katika vitabu hivyo. Katika utafiti wake, Strainbrook alieleza kuwa kuna njia maridhawa ambazo hutumika kuunganisha maneno na picha katika kufasiri jumbe zinazopitishwa na mchora vibonzo. Kutokana na maelezo ya Strainbrook kuhusiana na uwiano wa picha na maneno, mtafiti aliweza kutumia utafiti wa Strainbrook kama dira ya kuchunguza ni kwa njia ipi Gado alitumia wingimodi kuwasilisha jumbe zake za kitashtiti.

Oz (2014) anaeleza kuwa vibonzo vya kisiasa huunda picha au taswira na kusababisha taratibu tambuzi katika akili za wasomaji kwa kuchanganya matukio ya ulimwengu

halisi na analojia zinazotumika katika vibonzo vya kisiasa. Ikiwa matukio katika ulimwengu halisi na analojia zilizotumika katika vibonzo havioani, basi msomaji anapata uelewa mpya kuhusiana na yanayowasilishwa. Katika usanii wao, wanavibonzo huunda matukio ya kidhahania yenye wahusika wa kidhahania ili kuelezea matukio ya kihalisia na wahusika waliopo katika ulimwengu wa hivi sasa. Uumbaji wao hulenga kutoa maoni ya kijamii, kisiasa na ya kitamaduni. Wanavibonzo hutumia mandhari ya kidhahania kuelezea matukio pamoja na wahusika wa kihalisia katika siasa wakiwa na kusudi la kufupisha ujumbe changamano katika picha moja inayoteka hisia na raghba za umma.

El Refaie (2009) aliangazia jinsi jumbe na fremu ambazo vibonzo vya kisiasa huwasilisha hutegemea mwingiliano wa wingimodi kati ya modi hizi mbili za kisemiotiki; (yakuonekana na maneno). Modi hizi mbili hukamilishana kwa njia zifuatazo; kwa mfano, maneno yanaweza kutumika kutoa maana kwa yanayoonekana katika michoro iliyopo kwenye vibonzo. Kando na hayo, mtafiti huyo alielezea kuwa maneno yanaweza kutumiwa kuleta dhana ya kejeli katika vibonzo, hali ambayo haiwezekani kupitia picha peke yake. Hivyo basi, vibonzo vya kisiasa ni michoro inayotoa maoni kuhusu masuala ya kisiasa kwa kukiuka mifumo ya kawaida ya usomi na maana na kutokana na hayo, huathiri jinsi wasomaji wanavyotafsiri uhalisia. Mawazo ya El Rafaie yanaunda msingi dhabiti ambamo mtafiti alijengea utafiti wake. Kwa kutumia uhakiki wa kisemiotiki kwa minajili ya kuchanganua vibonzo alivyoteua, mtafiti aliweza kuweka wazi mikakati ya kitashtiti iliyotumika katika vibonzo vya Gado.

Macharia (b.t) alichunguza jinsi ucheshi usiokusudiwa katika matangazo ya umma yanayojitokeza katika vibango, mitandao ya kijamii na hata majina yanayopewa biashara. Alidai kuwa ucheshi huu hujitokeza kutokana na makosa yanayotokea kutokana na tafsiri, kuteleza kwa ulimi, makosa ya kitahajia, makosa ya kimatamshi, makosa ya kimantiki, mpangilio usio sahihi wa maneno na sauti zilizopangwa vibaya. Utafiti wake ulionyesha kuwa mwandishi wa matangazo yale ya umma huwa hana nia ya kusababisha ucheshi lakini ucheshi wenyewe hujitokeza kutokana na makosa mbalimbali ya kisarufi, kimantiki au kisemantiki. Utafiti wa Macharia ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa uliangazia ucheshi usiokusudiwa ilhali utafiti huu ulichunguza

ucheshi uliokusudiwa kama njia ya kutashtiti mambo mbalimbali kama yalivyosawiriwa kwenye vibonzo vilivyoteuliwa.

Highet (2015) anaeleza kuwa uundaji wa vibonzo vya kisiasa ni mchakato wa uashiriaji unaounda uhalisia wa kijamii kwa minajili ya kuwasilisha kwa hadhira masuala yatakayoibua burudani. Mitagusano ya kiwingimodi kati ya maneno na yanayoonekana pamoja na uundaji wa sitiara za vibonzo vya kisiasa huhitaji kiwango fulani cha uelewa wa kusoma na kuandika kutoka kwa msomaji. Ili msomaji aweze kusimbua maana ashiria na aweze kuelewa ucheshi uliopo katika kibonzo fulani, inampasa msomaji ashiriki katika mchakato mzima wa uelewa kwa kutumia mbinu zote za usomaji. Mwanzo kabisa, msomaji lazima atambue kinachorejelewa na kibonzo kile ili aweze kuelewa mwingiliano kati ya mandhari, watu au tukio la kubuniwa kama ilivyoundwa na mchora kibonzo na hali ilivyo katika ulimwengu halisi.

Uchambuzi wa kimakinifu wa masuala ya kijamii na athari ya michoro ya vibonzo huiwezesha hadhira ya vibonzo vya kisiasa kupata maana matilaba katika vibonzo vile. Kwa kifupi, ufasiri wa jumbe zilizosimbwa katika vibonzo vya kisiasa huhitaji wasomaji wa vibonzo hivi wawe na uelewa wa matukio yanayotokea ulimwenguni, sitiara zinazotumika, virejelewa na hata ishara zilizopo katika michoro iliyopo. Kress (2004) anaeleza kuwa jambo la msingi kwa msomaji, ni kuweza kuona jinsi malighafi maridhawa ya kisemiotiki hutumika kuleta maana. Maelezo ya Harris na Kress yalimsaidia mtafiti katika uchambuzi wa vibonzo alivyoteua kwa kuhusisha mbinu zote za uelewa kwa minajili ya kupata jumbe zilizosimbwa katika vibonzo vilivyoteuliwa.

### 2.3 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na mwanaisimu wa Kiswisi Ferdinand de Saussure katika mwaka wa (1857-1913) na baadaye kuendelezwa na wanafalsafa Charles Pierce (1958) pamoja na wahakiki kama vile Umberto Eco, na Roland Barthes (1973). Zaidi ya hayo, nadharia hii iliangaliwa upya na wataalamu kama vile Chandler (2002) na Wamitila (2002). Mtafiti alichagua nadharia ya semiotiki kwa kuwa ilikuwa faafu zaidi katika kuhakiki ishara mbalimbali zilizojitokeza katika vibonzo vya kisiasa kwa minajili ya kuchunguza mikakati iliyotumika katika kuendeleza maudhui ya kitashtiti.

Nadharia ya Semiotiki ilifaidika pakubwa kutokana na mawazo ya mwana- isimu wa Kiswizi Ferdinand de Sasssure kuhusiana na ishara. Chandler (2002) alieleza kuwa Ferdinand alifafanua ishara za kiisimu kama zile zilizo na viambajengo viwili kiashiria na kiashiriwa. Ambapo kiashiria ni kile kinachoonekana, kusikika au kugusika na kiashiriwa ni picha zinazojitokeza akilini tunapoona, kusikia au kugusa kitu; yaani dhana ambayo ishara inawasilisha. Kulingana na Ferdinand, ishara zote zinazotumika ni za kinasibu tu na hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya ishara na maana zake.

Baadaye Mwanafalsafa wa Kimarekani Pierce aliendeleza mawazo ya Ferdinand kuhusiana na ishara na anahusishwa na kielelezo cha pembe tatu cha ishara. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), Pierce alidai kuwa kila ishara huwa na yambwa au kitendwa kinachorejelewa na kifasiri ambacho ni dhana inayojitokeza akilini mwa anayefasiri ishara fulani. Hivyo, mawazo ya Pierce yaliongeza dhana ya yambwa ambayo haikuwepo katika mawazo ya Ferdinand. Pierce aliamini kuwa kila ishara inayotumika ulimwenguni huwa ina misingi fulani inakotegemezwa ili ufasiri wake uwezekane.

Wamitila (2002) alifafanua kuwa ingawaje nadharia ya Semiotiki ilichota mawazo yake kutoka kwa Ferdinand na Pierce, kuzuka kwa nadharia hii kulihusishwa na kipindi cha miaka ya 1970 na mawazo ya Roland Barthes yalitoa mwongozo dhabiti kuhusiana na uchambuzi wa ishara. Katika miaka ya 1950 na 1960 Roland Barthes alipanua mawazo ya Saussure. Chandler (2002) alielezea kuwa Barthes aliamini kuwa maana za kitamaduni huwa zimejikita katika lugha husika. Mtazamo wake ulihusisha dhana ya udokezi ama kama anavyoeleza; maana ya ziada. Kulingana na Barthes, kiashiriwa kinaweza kuwa kiashiria katika kiwango kingine cha maana. Kwa mfano istilahi “nyekundu” humaanisha aina fulani ya rangi, lakini pia inaweza kudokeza “hatari” katika utamaduni wa Kiafrika.

Wamitila (2002), alieleza kuwa Barthes aliangazia misimbo mitano ya usomaji ambayo iliwacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji. Kulingana na mhakiki huyu, matini yoyote ile inapaswa kuvunjwa katika vitengo vidogo vidogo ili kusaidia katika ufasiri wake. Misimbo hii ilichukuliwa kama mihimili au nguzo kuu za nadharia ya semiotiki. Barthes alifafanua misimbo hii kama ifuatavyo:

(a) Msimbo wa matukio ambao ulihusu namna matukio yanayopatikana na kufuatana katika kazi yoyote ile ya kisanaa na jinsi msomaji anavyounda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo ya kisanaa kwa kutathmini jinsi matukio yanavyofuatana kiathari au ki-sababishi. Katika utafiti huu, mhimili huu ulimsaidia mtafiti katika kueleza na kufafanua matukio yaliyojitokeza katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyoteuliwa kwa minajili ya kuhakiki ishara zilizojitokeza.

(b) Msimbo wa kihemenitiki unahusu taharuki au usimulizi. Aghalabu msimbo huu huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unaweza kufumbatwa kwenye anwani ya kazi fulani. Mhimili huu, ulimwongoza mtafiti katika kuelewa yaliyomo kwenye vibonzo alivyoteua kwa kuangazia vidokezo vilivyojitokeza katika anwani za vibonzo vilivyoteuliwa. Kutokana na anwani za vibonzo vile, mtafiti aliweza kujiuliza maswali yaliyojenga taharuki ya kutaka kuhakiki vibonzo vile kwa minajili ya kuelewa ujumbe uliojitokeza.

(c) Msimbo wa ki-seme hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambazo hutupa picha ya mhusika au matukio fulani katika kazi za kisanaa kutokana na viashiria katika kazi zile. Kutokana na mhimili huu, mtafiti aliweza kutathmini ishara zilizokuwepo katika vibonzo vilivyoteuliwa na akaweze kuelezea picha zilizojitokeza akilini mwake kama mhakiki wa vibonzo vile.

(d) Msimbo wa kiishara unahusishwa na namna wasomaji wanavyovumbua maana za ishara katika kazi za kisanaa. Msimbo huu wa kiishara ulikuwa kidokezo kikuu katika kuchanganua ishara kama zilivyojitokeza katika vibonzo vya kisiasa. Katika utafiti huu, mhimili wa msimbo wa kiishara ulimsaidia mtafiti katika kuelezea maana ya ishara zilizokuwepo katika vibonzo vilivyoteuliwa kama vile, rangi zilizotumia, ukubwa wa maneno yaliyotumiwa, kimo cha watu waliosawiri katika vibonzo vile pamoja na mitindo ya lugha katika vibonzo vile.

e) Msimbo wa kirejelezi hujengwa kutokana na viashiria vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi za kisanaa. Huhusisha matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na hivyo kuipa kazi fulani nguzo ya kiutamaduni. Msemaji akisema kuwa anakielewa kitu anachokimaanisha msanii husema hivyo katika msingi wa kiurejelezi au kiutamaduni. Mhimili

huu, ulimwongoza mtafiti katika kuelewa matukio na jumbe zilizosimbwa katika vibonzo vilivyoteuliwa. Hili lilifanyika kwa kuhusisha utamaduni na mazingira ya mchora vibonzo na jumbe zilizojitokeza katika vibonzo vile kwa minajili ya kufasiri na kuhakiki jumbe kama zilivyokusudiwa na mchora vibonzo.

Kwa jumla, utafiti huu uliongozwa na mihimili yote mitano ya nadharia ya kisemiotiki. Ambapo mihimili wa msimbo wa matukio na msimbo wa kihemenitiki ilifungaman na madhumuni ya kwanza na mihimili ya ki-seme, kiishara na kirejelezi ilifungamana na madhumuni ya pili. Mtafiti alitumia kila mhimili kuchambua matukio yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa, kisha akahakiki na kutolea maelezo ishara zilizojitokeza katika vibonzo vile. Mwishowe, nadharia hii ilimsaidia mtafiti kufafanua maana zilizotokana na ishara zilizokuwepo katika vibonzo vile na maana hizi ndizo zilizoibua suala la tashtiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu zilizotumika katika ukusanyaji, uwasilishaji na uchambuzi wa data. Mbinu hizi, kwa njia moja au nyingine, ziliteuliwa kutokana na sababu maalumu ambazo zimeainishwa katika kila kipengele. Vipengele vilivyoshughulikiwa katika sura hii ni muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, kundi lengwa, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data. Utafiti huu ulijikita katika mawasiliano na hasa, katika uhakiki wa matini kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki kwa minajili ya kupata maana.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu uliendelezwa kwa kutumia muundo wa kimaelezo ambapo mtafiti alitoa maelezo kuhusiana na uhakiki na uchambuzi wa yaliyomo katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyoteuliwa. Uchanganuzi ulifanywa kwa kuzingatia madhumuni yote mawili ya utafiti huu na data iliyokusanywa ilisimbwa, ikachanganuliwa na kutolewa maelezo yaliyopangwa katika sura mbalimbali. Newsome (2015) alieleza kuwa muundo wa kimaelezo unazingatia umuhimu wa kufafanua namna watu wanavyofikiri kuhusu hali, kitu au jambo fulani na kutathmini hisia za watu juu ya hali, kitu au jambo hilo. Hivyo basi, maelezo yenyewe yalihusiana moja kwa moja na madhumuni ya utafiti huu.

## 3.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti ulifanyika mtandaoni ambapo mtafiti alidurusu vitabu, magazeti na tafiti za wengine zilizohusiana na mada ya vibonzo vya kisiasa na tashtiti. Kwa kuwa data ya utafiti huu ni vibonzo vya kisiasa vilivyochapishwa na Gado, mtafiti alipekua tovuti ya Gado (www.gadocartoons.com) ambapo alipakua vibonzo sitini vilivyochapishwa katika mwaka wa 2017 kwa minajili ya kupata data ya utafiti wake. Katika udurusu wake, mtafiti aliongozwa na malengo na nadharia ya utafiti huu.

## 3.4 Kundi Lengwa

Newsome (2015) alieleza kuwa uteuzi wa kundi lengwa ni utaratibu ambao mtafiti anatumia katika kuchagua orodha ya vitu au watu kwa ajili ya sampuli yake ya utafiti. Ni muhimu kutambua kuwa kundi lengwa ni elementi ambazo mtafiti anakusudia kuhusisha katika utafiti wake. Utafiti ulilengavibonzo ishirini vya kisiasa vya Gado

vilivyochapishwa kwenye tovuti yake katika mwaka wa 2017 na mtafiti alijikita kwenye vibonzo vilivyohusu nchi ya Kenya. Pamoja na hayo, mtafiti alijikita katika vibonzo vilivyochapishwa katika kipindi cha mwaka wa 2017 kwa kuwa alichukulia kuwa kipindi hiki, kingempa data toshelevu ya utafiti. Kipindi hiki cha mwaka wa 2017 kiliteuliwa kwa sababu kulikuwa na uchaguzi mkuu baada ya miaka mitano ya kuanzishwa kwa serikali za kaunti na ilichukuliwa kuwa kuwepo kwa serikali za kaunti huenda kulileta mabadiliko katika uwanja wa siasa nchini Kenya. Hivyo data ambayo ingepatikana katika vibonzo vilivyoteuliwa ingekuwa pana na changamano. Pili, mtafiti alichukulia kuwa vibonzo vingi vingesheheni utendakazi wa serikali ya Jubilee katika muhula wao wa kwanza na kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017 katika mfumo wa ugatuzi.

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Singh (2007) alielezea kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi ndogo kutoka kwa kundi kubwa la watafitiwa kwa minajili ya kufanya makisio kuhusiana na kundi lengwa. Mtafiti alipekua tovuti ya Gado na kupakua vibonzo sitini vilivyokuwa vimechapishwa katika mwaka wa 2017.Baadaye mtafiti aliteua kundi ndogo la vibonzo ishirini vilivyohusu nchi ya Kenya kutokana na kundi pana la vibonzo sitini alivyokuwa ameteua na katika shughuli hii aliongozwa na madhumuni ya utafiti, huu ambayo ni kuchanganua maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa vilivyochapishwa katika mwaka wa 2017 katika tovuti ya Gado na kuhakiki mikakati ya kitashtiti inayovifanya vibonzo hivi visemekane kuwa ni vya kitashtiti

Usampulishaji wa kimakusudi huhusisha uteuzi wa kazi mahsusi kutokana na sababu maalum zinazomsukuma mtafiti kuteua sampuli hiyo. Sababu zilizompelekea mtafiti kuteua vibonzo vya Gado vilivyochapishwa kwenye tovuti yake ni kwa kuwa, vibonzo hivi huwa havijadhibitiwa na serikali au vyombo vya habari. Hivyo, vilimpa mtafiti data toshelevu na yenye makali ambayo ilihitajika katika utafiti huu. Sababu ya pili ni kuwa, Gado ni mchora vibonzo maarufu nchini Kenya na ana tajriba ya zaidi ya miaka ishirini na saba, hivyo vibonzo vyake vilichukuliwa kuwa na weledi katika usawiri wa masuala ya kisiasa. Tatu, kipindi cha 2017 kilichukuliwa kuwa ni kipindi chenye mengi ya kutafitiwa kutokana na hali kuwa, kilikuwa miaka mitano baada ya mfumo wa serikali za kaunti kuanzishwa na pia mtafiti alijua kuwa kulikuwa kumefanyika uchaguzi mkuu chini ya mfumo wa serikali za kaunti. Hivyo, mtafiti alichukulia kuwa

angepata data pana na changamano kutokana na uteuzi wa kipindi cha mwaka wa 2017. Zaidi ya hayo, mtafiti alitaka kuhakikisha kuwa amepata data pana na toshelevu kwa minajili ya kuafikia madhumuni ya utafiti huu.

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Kwa vile utafiti huu ulifanyika mtandaoni, mtafiti alitumia mbinu ya maandishi kukusanya data. Hapa mtafiti, alipakua vibonzo sitini vilivyokuwa vimechapishwa kwenye tovuti ya Gado katika mwaka wa 2017, kisha akateua kimaksudi vibonzo ishirini vilivyohusu nchini ya Kenya na vilivyofungamana na madhumuni ya utafiti huu na baadaye kuvipa vibonzo hivyo kodi maalamu kulingana na maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vile. Mtafiti aliweza kufanya hivi kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi yaliyomo katika vibonzo vile ilikufanikisha shughuli mzima ya kukodi data. Kwa mfano; kodi K1UWW ilisimamia kibonzo cha kwanza chini ya maudhui ya Unyanyasaji wa Wafanyakazi, K2UWM inamaanisha kibonzo cha pili chini ya maudhui ya Ukosefu wa Maadili, na K1UO, inasimamia kibonzo cha kwanza chini ya maudhui ya Uongozi.

Kwa kuwa baadhi ya maudhui yaliyojitokeza katika utafiti huu yalianza kwa herufi "U" mtafiti aliamua kuchukua herufi za kwanza mbili katika maudhui yaliyojitokeza ili kutofautisha vibonzo vyenyewe. Kwa mfano; kodi K1UF ilimaanisha kibonzo cha kwanza chini ya maudhui ya Ufisadi, kodi K2UP ilimaanisha kibonzo cha pili chini ya maudhui ya Upendeleo na K1UN ilimaanisha kibonzo cha kwanza chini ya maudhui ya Unafiki. Kando na hayo, mtafiti alikodi majina ya wahusika walioangaziwa kwenye vibonzo hivi kwa kuchukua herufi ya kwanza ya jina lao la kwanza na herufi ya kwanza ya jina la pili, Kwa mfano, kodi RO ilisimamia Raila Odinga, MM ilisimamia Musalia Mudavadi, PI ilisimamia Polycarp Igathe, MS ilimaanisha Mike Sonko, MW isamamia Moses Wetangula na BY ilisimamia Baba Yao

Katika ukusanyaji data, mtafiti alidurusu vitabu, magazeti, tasnifu za wengi na mitandao ili kupata data kuhusiana na vibonzo vya kisiasa, tashtiti na hata mitindo mbalimbali inayotumika katika uchoraji wa vibonzo. Mtafiti alitumia vitabu, kalamu, kipakatalishi na kitepetevu hambo kwa minajili ya kurekodi na kuhifadhi data aliyopata. Pamoja na hayo, mtafiti alitumia mtandao kudurusu na kupakua data kutoka kwenye tovuti ya Gado.

Shughuli muhimu katika sehemu hii ilikuwa udurusu wa tovuti ya Gado, www.gadocartoons.com na upakuaji wa vibonzo sitini vilivyochapishwa katika mwaka wa 2017, kwa minajili ya kuhakiki mikakati ya kitashtiti iliyotumika katika vibonzo vilivyoteuliwa. Baada ya kuteua vibonzo ishirini, kutokana na kundi pana la vibonzo sitini, mtafiti alivipanga kulingana na madhumuni ya utafiti wake na baadaye akabaki na kundi ndogo la vibonzo ishirini alivyotumia katika utafiti huu.

**3.7 Uchanganuzi wa Data**

Magigi (2012) alieleza kuwa uchambuzi wa data huhusu kukusanya, kuainisha na kupanga data. Kutokana na maelezo haya, mtafiti alikusanya data kwa kupekua tovuti ya Gado na akachagua vibonzo ishirini kutoka kwa vibonzo sitini alivyokuwa ameteua kimaksudi kwa minajili ya kuvihakiki. Mwanzo kabisa mtafiti alifanya uhakiki wa yaliyomo kwa minajili ya kupata maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo alivyoteua. Kisha baadaye mtafiti alitafsiri yaliyomo katika vibonzo vyenyewe kwa kutumia mbinu ya utafsiri sisisi pamoja na utafsiri maana na kuhakikisha kuwa maana iliyokusudiwa haikupotezwa wakati wa kutafsiri. Data hii ilichambuliwa na kufafanuliwa kwa kutumia maelezo, ambapo mtafiti alitoa maelezo kuhusu yaliyokuwa yakisawiriwa katika vibonzo vile na uhakiki wa yale aliyoelewa kutokana na usawiri huo Uchanganuzi wa data iliyokusanywa ulizingatia madhumuni ya utafiti huu, ambayo yalikuwa ni kuchanganua maudhui ya kitashtiti yaliyojitokeza katika vibonzo vya kisiasa vya Gado. Mtafiti aliafikia madhumuni haya, kwa kuhakiki na kuelezea yaliyojitokeza katika vibonzo alivyoteua ili kupata maudhui yaliyokuwa yakisawiriwa na Gado. Kando na hayo, mtafiti alitumia mihimili ya nadharia ya semiotiki kufafanua na kutoa maelezo kuhusiana na data aliyoipata. Katika utafiti huu, mtafiti alihakiki mikakati ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa kwa kutumia mihimili yote mitano ya nadharia ya semiotiki. Mtafiti alibainisha ishara zilizotumika katika vibonzo vile na kueleza yafuatayo;

- Ishara zilizokuwepo katika vibonzo vile ziliashiria nini?
- Ni dhana zipi zilizojitokeza akilini mwa mtafiti kutokana na ishara zile?
- Msomaji alipata maana gani kutokana na ishara zile yaani alifasiri vipi ishara zile?

### 3.8 Uzingativu wa Maadili

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu mwafaka za kukusanya data kwa minajili ya kupata data iliyo sahihi. Data ya utafiti ilichotwa kutoka kwa vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyochapishwa kwenye tovuti yake na kwa kuwa vibonzo hivi ni hakimiliki ya Godfrey Mwampembwa (Gado), mtafiti alinukuu vibonzo vyote alivyopakuwa na kuelezea alikovitoa. Isitoshe, mtafiti alipata idhini kutoka Shirika la NACOSTI nchini Kenya. Pale ambapo mtafiti alikumbana na vibonzo vilivyochukuliwa kuwa pujufu, kwa mfano vilivyolisawiri mambo ambayo kwa kawaida hayasemwi hadharani, mtafiti alitoa ufafanuzi kuvihusu kwa minajili ya kuzingatia maadili ya kijamii katika utafiti wake. La muhimu ni kuwa mtafiti alihakikisha kuwa kazi yake haikukiuka maadili ya usomi kwa kuhakikisha kuwa hakuiba kazi za wasomi wengine na kuzitumia kama kazi yake mwenyewe.

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliainisha na kutoa maelezo kuhusu maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vya kisiasa alivyopakua kutoka tovuti ya Gado. Kutokana na sampuli kubwa ya vibonzo sitini, mtafiti aliteua kimaksudi vibonzo ishirini vilivyochukuliwa kuwa vya kitashtiti. Mtafiti alivipa vibonzo alivyoteua kodi kulingana na maudhui kama ilivyofafanuliwa katika sura ya tatu, kwa minajili ya kuvichambua na kuvitolea maelezo.

. Baadaye, mtafiti alichanganua vibonzo alivyoteua na kuvipanga kulingana na ujumbe uliokuwa ukipitishwa na kila kibonzo. Jumbe tawala katika vibonzo vile ndizo zilizounda maudhui ya vibonzo vilivyoteuliwa. Mtafiti pia alipanga vibonzo vile kulingana na maudhui yaliyojitokeza ambayo yalijumuisha; uongozi, ulaghai katika siasa, unafiki, ukosefu wa maadili, upendeleo na ufisadi.

Sehemu ya pili ya sura hii ilijishughulisha na kutambua mikakati iliyotumiwa na msanii kuhakikisha kuwa vibonzo vyake ni vya kitashtiti. Katika sehemu hii, mtafiti alichunguza yaliyokuwa yamesawiriwa kwenye vibonzo, maneno yaliyoandamana na vibonzo vyenyewe, namna watu au masuala yalivyosawiriwa katika vibonzo vile, rangi zilizotumika, alama na ishara zilijitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa. Masuala haya yote yalitoa mwongozo kuhusiana na mikakati ya kitashtiti iliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa. Shughuli hii ya uchambuzi wa vibonzo ilifanywa kwa kuzingatia uchanganuzi wa yaliyomo katika vibonzo vilivyoteuliwa pamoja na mihimili ya nadharia ya Semiotiki.

### 4.2 Maudhui katika Vibonzo

Kwa kawaida, vibonzo vya kisiasa husawiri hali ya kisiasa ilivyo katika nchi fulani. Mara nyingi usawiri huu hudhihirisha maoni ya mchora vibonzo kuhusiana na hali ilivyo na wakati mwingine husawiri hali halisi ya nchi fulani. Vibonzo vilivyoteuliwa kwa minajili ya utafiti huu vilimulika hali ya kisiasa katika nchi ya Kenya katika mwaka wa 2017 na kwa kiasi kikubwa vilisheheni maoni ya msanii Gado kuhusiana na masuala mbalimbali kama itakavyodhihirika katika sehemu za sura hii.


### 4.2.1 Uongozi

Uongozi aghalabu humaanisha, hali ya kuwa na mtu mmoja anayetawala nchi kwa minajili ya kusaidia wananchi wanaoishi kwenye nchi ile kufikia malengo yao. Aghalabu, uongozi unafaa kuwaunganisha wananchi wanaotoka kwenye tabaka na makabila mbalimbali. Trommel (2020) alieleza kuwa lengo kuu na thamani ya kiongozi na aina yoyote ile uongozi ni kuwahamasisha wengine, wanaoonekana kama wafuasi, kujiunga kwa hiari kufanikisha malengo ya pamoja. Fasiri hii ya Trommel inadhihirisha kuwa ni lengo kuu ya uongozu ni kuafikia malengo fulani ya pamoja. Miricho (2021) anaelezea uongozi kama dhana ya kisosholojia ambayo ikitafsiriwa katika vitendo inaweza kuelekeza jamii kufikia malengo yake. Ni hali ya kawaida kuwa na kiongozi wakati ambapo kuna zaidi ya mtu mmoja ili watu waweze kuongozwa kwa mpangilio wa usawa na malengo yao kama wanajamii yaweze kutimizwa. Sababu kuu ya kuwa na uongozi wowote katika jamiii ni kuunganisha vipaji, nguvu, uwezo na rasilimali za wanajamii kwa minajili ya kuboresha kila mwanajamii na eneo wanaloishi. Wajibu mkuu wa kiongozi yoyote yule ni kusaidia kuunganisha uwezo wa watu kwa kuratibu na kusimamia shughuli za watu kwa manufaa ya kila mwanajamii.

Utafiti huu uliangazia vibonzo vilivyochapishwa mwaka wa 2017 na hasa vilivyohusu nchi ya Kenya. Nchi ya Kenya ni nchi ya kidemokrasia, ambayo imegawika katika maeneo makubwa yanayojulikana kama kaunti, kisha kaunti zile zina maeneo ya ubunge, na maeneo ya ubunge yamegawika katika wadi ndogo ndogo. Nchi ya Kenya ina mfumo wa serikali ambao wananchi wana mamlaka ya kuchagua viongozi watakaowawakilisha katika Bunge, Seneti na hata Kaunti. Uchaguzi wenyewe huwa wa kura ya siri na husimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka. Serikali ya Kenya huongozwa na rais na naibu wake wanaochaguliwa na wananchi. Kisha kuna bunge ambalo wananchi huchagua wabunge na wawakilishi wa wanawake. Kando na hayo, kuna serikali za kaunti zinazoongozwa na magavana na manaibu wao, maseneta na wawakilishi wa wadi.

Mtafiti alichagua kipindi cha 2017 kwa minajili ya kufanyia uchunguzi vibonzo vilivyochapishwa katika kipindi kile. Mwaka huo ulisheheni mwaka wa mwisho wa muhula wa uongozi wa Rais Uhuru Kenyatta ambaye jina lake lilipewa kodi ya Rais na Naibu wake William Ruto aliyepewa kodi ya Naibu Rais waliokuwa wamechaguliwa kuchukua hatamu za uongozi katika mwaka wa 2013. Rais Uhuru na William Ruto

walishinda kinyang'anyiro cha urais chini ya chama cha Jubilee, kilichoundwa baada ya Rais kuvunja chama chake cha TNA na Naibu Rais kuvunja chake cha URP na kuungana na kuunda chama cha Jubilee. Wapinzani wao wa karibu walikuwa Raila Odinga (RO), Kalonzo Musyoka (KM), Musalia Mudavadi (MM) Moses Wetangula (MW). Viongozi hao wanne waliungana na kuunda muungano wa NASA na aliyekuwa mpeperusha bendera wa muungano huo katika kinyang'anyiro cha urais alikuwa RO na naibu wake KM. Chini ya maudhui ya uongozi, mtafiti alichambua vibonzo vilivyohusu uongozi wa nchi ya Kenya kwa jumla na sifa za uongozi huo.




***Kibonzo 3: $K_1$UO, Jubilee italeta Maziwa na Asali. Kutoka (http://gadocartoons.com/Jubilee-will-bring-milk-honey/).***

Katika Kibonzo $K_1$UO, Gado alisawiri rais wa nchi ya Kenya aliyepewa kodi ya Rais na naibu wake aliyepewa kodi ya Naibu Rais wakifanya kampeni katika eneo linaloonekana likiwa limejaa mafuvu, na mifupa ya binadamu na wanyama. Katika kibonzo kile, kuna mapipa yanayochukuliwa ni ya kutekea maji yakiwa pembeni mwa kibonzo kile. Rais na Naibu Rais wanaonekana wakiwa kwenye gari lenye kibango chenye ishara ya mikono miwili iliyoshikana ambayo ilikuwa ishara ya chama cha *Jubilee* ambacho kilikuwa chama walichounda kwa minajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017. Kauli mbio ya chama hiki cha Jubilee ilikuwa "Tuko Pamoja na huenda ishara hii ya mikono miwili iliyoshikana ilitumika kumaanisha kuwa wawili hawa walikuwa pamoja na wananchi na wananchi waliokuwa wakinuia kuongoza. Msanii Gado amemsawiri Rais akiwa amevalia taji la kifalme hali ambayo ni ya kinaya

kwani nchi ya Kenya ni nchi ya kidemokrasia na haiongozwi na wafalme. Kando na hayo, Naibu Rais amesawiriwa akiwa amevalia kilemba kinachovaliwa na watu wa dini ya Sikh ilhali yeye si mfuasi wa dini ile. Zaidi ya hayo, tunaonyeshwa Rais akiambia mafuvu na mifupa ya mifugo ile;

*Forget Water…Jubilee Will Bring Milk and Honey to You!!*
*Sahauni Maji…Jubilee Itawaletea Maziwa na Asali*!

Naye Naibu Rais anasisitizia "wananchi" ambao wamesawiriwa kama mifupa na mafuvu kuwa;


*Just Remember Kura Yako, Haki Yako*
*Kumbukeni Kuwa Kura Yako Ni Haki Yako*.

Usemi wa *Forget Water…Jubilee Will Bring Milk and Honey to You"* pia unazua dhana ya mwingiliano matini ambapo usemi huu unaweza kufafananishwa na hadithi ya wanaisraeli katika bibilia. Pale ambapo Mungu aliahidi kuwatoa wana wa Israeli kwenye utumwa na kuwapeleka katika nchi yenye maziwa na asali (Bibilia Takatifu, 2001, Kutoka 3:17)

Matukio katika kibonzo hiki yanadhihirisha jinsi ambavyo Rais na naibu wake hawakuwajali wananchi. Msanii anapowasawiri wananchi kama mafuvu na mifupa, alikuwa anapitisha ujumbe kuwa wananchi walikuwa wamekwisha kufa kutokana na ukosefu wa chakula na maji, mahitaji ambayo ni ya kimsingi kwa kila binadamu. Kando na hayo, msanii anapotuonyesha Rais na Naibu Rais wakiwa kwenye gari lililo na kibango cha ishara ya kuwa pamoja, anajaribu kuibua hali ya unyume kwa kuwa viongozi hao wawili hawako kwenye kiwango kimoja na raia waliowachagua. Wananchi walioangaziwa katika kibonzo hiki wanahitaji maji na chakula ndiposa maisha yao yaendelee ilhali Rais na Naibu Rais wanahitaji kura ndiposa waweze kupata kazi ya kutawala nchi ya Kenya pamoja na hadhi na mamlaka yanayoambatana na kuwa rais na naibu rais. Isitoshe, kibonzo kile kinatuonyesha Rais na Naibu wake wakiendelea na kampeni za ahadi ya asali na maziwa ilhali hawajatimizia wananchi haja yao ya maji. Kutokana na usawiri wa Gado, wananchi wamekwisha kufa kutokana na ukosefu wa mahitaji muhimu. Matukio yaliyosawiriwa katika kibonzo $K_1UO$ yalikuwa ishara tosha kuwa uongozi wa Rais na Naibu Rais ulipuuza mahitaji ya kimsingi ya wananchi kwa kujishughulisha na mahitaji yao binafsi. Kutokana na

maelezo yaliyotolewa awali kuhusiana na uongozi; kuwa ni hali ya kuunganisha vipaji, nguvu, uwezo na rasilimali za wanajamii, kwa minajili ya kuboresha kila mwanajamii na eneo wanaloishi; tunaweza kusema kuwa uongozi wa Rais na Naibu Rais haukufikia vipimo vya maelezo ya uongozi mzuri na hivyo uongozi wa serikali ya Rais na Naibu Rais ulikuwa uongozi mbaya uliowahujumu wananchi.

**Implementing the Jubilee Agenda**




***Kibonzo 17: K2UO Utekelezaji wa Ajenda ya Jubilee, Kutoka (www.gadocartoons.com).***

Vilevile, msanii anamulika uongozi wa nchi ya Kenya chini ya Rais kupitia Kibonzo $K_2$UO. Katika kibonzo hiki, tunaonyeshwa picha ya Rais akiwa amevalia sare rasmi ya kijeshi, kichwani amevalia taji la kifalme, kwenye mkono wake wa kulia ameshika kikaragosi kilichovalia sare ya afisa wa polisi na mkononi mwa kikaragosi yule kuna bunduki. Kwenye upande wa kushoto wa mkono wa Rais anaonekana akiwa ameshikilia fimbo rasmi inayotumika kwenye bunge la nchi ya Kenya. Nchini Kenya, fimbo ile inadhihirisha mamlaka ya Spika wa bunge. Kando na hayo, Rais anaonekana akisema;

> *We Have Moved On! Now We Are Implementing Our Agenda. After NGOs Who Is Next?*
> *Sisi Tumeshasahau! Sasa Tunatekeleza Ajenda Yetu. Baada Ya Taasisi Zisizo Za Kiserikali Ni Nani Atafuata?*

Nyuma ya Rais, Gado anatuonyesha aliyekuwa kinara wa wengi bungeni Aden Duale ambaye alipewa kodi ya (AD), akiwa ameshikilia kijitabu. Kulingana na Katiba ya nchi ya Kenya, baada ya uchaguzi mkuu, chama au muungano unaopata wabunge wengi huchukuliwa kuwa ndio wengi bungeni na chama au muungano uliochukua nafasi ya pili huchukuliwa kuwa walio wachache bungeni. Walio wengi bungeni huchagua mmoja wao kuwa mwakilishi wao na ndiposa AD akachaguliwa kuwa kinara wa wengi bungeni. Zaidi ya hayo, AD anaonekana akisema;

*Auditor General, Media, Then….*

*Mkaguzi Wa Hesabu, Vyombo Vya Habari, Kisha…*


Nyuma ya AD, msanii anatusawiria kikaragosi kilicho na sura ya nguruwe kilichoyebeba gunia linaloonekana kuwa limejaa. Vile vile, Naibu Rais anaonekana akivuta nyuzi za kikaragosi kile. Kwenye upande wa kulia wa kibonzo hiki, kuna kijibonzo kingine kidogo kinachoonekana kushangaa.

Matukio ya kibonzo $K_2$UO, yanadhihirisha hali ya uongozi wa serikali ya rais wa Kenya katika mwaka wa 2017. Matukio yaliyojitokeza katika kibonzo hiki, yanalandana na matukio yaliyojitokeza baada ya uchaguzi mkuu wa 2017, ambapo Rais alishinda katika kinyang'anyiro kile na baadaye ushindi wake ukabatilishwa na mahakama kuu ya nchi ya Kenya. Tendo lile lilimkera Rais na mara nyingi alisikika akiwadokezea kuwa atarejelea yaliyojiri kwenye mahakama kuu, hali inayomfanya Rais kusema kuwa wamekwisha sahau na sasa wanaendelea na kutelekeza ajenda yao. Dhana ambayo ni kinyume na hali inayosawiriwa na msanii. Katika kibonzo hiki, hali ya Rais kuvalia sare kamili ya jeshi ilitumika kuashiria kuwa Rais alikuwa ndiye mkuu wa majeshi ya nchi ya Kenya na kuwa alikuwa na mamlaka kamili juu ya nchi ya Kenya.

Hata hivyo, msanii anapomsawiri Rais akiwa amevalia taji la kifalme, anadokeza kuwa Rais anatumia mamlaka yake vibaya kwa kuongoza jamhuri ya nchi ya Kenya kama himaya iliyo chini ya ufalme wake ambapo, anachosema ni sheria na hakuna nafasi ya mazungumzo au majadiliano. Zaidi ya hayo, Rais anaposawiriwa akiwa amebeba fimbo ya bunge inayodhihirisha mamlaka ya Spika wa bunge la nchi ya Kenya, Gado anatuelezea kuwa Rais anachukua mamlaka ya bunge la nchi ya Kenya kupitia Spika wa bunge, hali ambayo haistahili katika nchi ya kidemokrasia kwani bunge linafaa kufanya kazi bila kuathiriwa na rais. Hivyo, Gado anapomuangazia Rais wa Kenya akiwa amebeba fimbo ya bunge anadokeza kuwa bunge la nchi ya Kenya liko chini ya

mamlaka na uelekezi wa Rais na hivyo haliko huru kutenda kama litakalo ama inavyotakikana. Isitoshe, Rais anapoonekana akisema kuwa amekwisha sahau yaliyotendeka na sasa wanaendelea na ajenda yao, msanii alikuwa akimtashtiti Rais kwa kujitia shughuli za kuhujumu taasisi zisizo za kiserikali, mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali na vyombo vya habari.

Pamoja na hayo, msanii anatuonyesha taswira ya Naibu Rais akivuta kikaragosi kilicho na sura ya nguruwe kumaanisha kuwa Naibu Rais alikuwa anadhibiti wabunge wa nchi ya Kenya. Suala la wabunge wa nchi ya Kenya kusawiriwa kama nguruwe, lilitokana na tendo la mwanaharakati Boniface Mwangi (BM), aliyepeleka nguruwe walio hai na waliokuwa wamejaa damu nje ya jengo la bunge kupitisha ujumbe kuwa ni walafi kwa kutaka nyongeza za mishahara ilhali wananchi wa kawaida walikuwa wakiteseka (BBC, 2013). Hivyo, msanii anapotuonyesha taswira ya kikaragosi chenye sura ya nguruwe anayechezewa na Naibu Rais, ina maana kuwa bunge lilikuwa limetawaliwa na kutumiwa na Naibu Rais kutelekeza ajenda zake binafsi. Kutokana na matukio ya kibonzo $K_2$UO, msanii anadokeza kuwa uongozi wa Rais ulikuwa wa kidikteta ambapo alikuwa anadhibiti kitengo cha jeshi, polisi, na bunge la Kenya. Kwa kifupi, msanii alikuwa anatashtiti uongozi wa Rais na Naibu Rais kwa kutumia taasisi moja ya serikali kuhujumu taasisi zingine za serikali zilizoonekana kutofautiana na mkondo wa mawazo wa Rais na naibu wake. Hivyo, kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa Rais na Naibu Rais wa nchi ya Kenya katika mwaka wa 2017 walikuwa madikteta waliotumia mamlaka yao kudhalilisha taasisi huru kama vile; bunge, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya habari, pamoja na wafanyikazi wa serikali wanaopaswa kuhakikisha kuwa serikali inafanya kazi yake kama inavyostahili. Uangaziaji huu wa uongozi wa Rais na Naibu Rais unaonyesha uhuru uliopo katika uchapishaji wa vibonzo katika mitandao kwa kuwa Gado ametumia uhuru huo kuweka wazi masuala ambayo kwa kawaida watu hufikiria na kuona lakini hawawezi kuyachapisha katika magazeti kutokana na uoga kuwa wanaweza kufunguliwa mashtaka au kufutwa kazi.




***Kibonzo 11: K$_3$UO Ugatuzi katika Shamba la Wanyama. Kutoka (http://gadocartoons.com/devolution-animal-farm/).***

Kibonzo K$_3$UO kinaangazia suala la ugatuzi kwa kulinganisha ugatuzi nchini Kenya na matukio katika riwaya ya George Orwell, Shamba la Wanyama (1967). Kenya ni nchi ya kidemokrasia na kuanzia mwaka wa 2013, katiba ya nchi hii ilibadilisha mfumo wa serikali kutoka kwa serikali ya kitaifa hadi serikali za kaunti zinazoongozwa na magavana na manaibu wao. Kando na hayo, kuna maseneta ambao kazi yao ni kuhakikisha kuwa fedha zilizogawiwa serikali za kaunti zinatumika kama ipasavyo. Aidha, kuna wabunge na wawakilishi wa wanawake ambao hupatikana katika bunge la nchi ya Kenya na chini yao kuna wawakilishi wa wadi wanaopatikana katika bunge za kaunti na huwakilisha wadi zilizoko kwenye eneo la ubunge. Katika kibonzo hiki, msanii anatuonyesha cheo cha rais kilichosimamiwa na kikaragosi chenye sura ya nguruwe kumaanisha kuwa aliye kwenye ofisi hii ana sifa za ulafi. Chini ya rais, kwa upande wa kushoto kuna Seneta aliyesawiriwa kama tai ambaye ana sifa ya kunyapanyapa kwenye mizoga, kumaanisha mwenye kushikilia ofisi hii ana sifa za kunyapanyapa mali ya umma.


Katika muktadha wa nchi ya Kenya, kiti cha useneta huchukuliwa kuwa hakina majukumu mengi isipokuwa tu kuhakikisha kuwa mgao wa fedha unaoelekezwa kwenye kaunti unatumika ipasavyo. Kwa kawaida, tai ni ndege ambaye huandama mnyama anayeonekana mnyonge na yuko karibu kufa ndiposa waweze kupata lishe bila hekaheka za kuwinda. Hivyo, msanii anapowasawiri maseneta kama tai anapitisha

ujumbe kuwa ni wakereza, wanaonufaika kutokana na kazi za watu wengine. Zaidi ya hayo, mwakilishi wa wanawake amesawiriwa kama paka. Wakati mwingi paka hufugwa nyumbani ili awinde panya ama kama pambo la nyumbani. Usawiri huu wa wakilishi wa wanawake, ulipitisha ujumbe kuwa nyadhifa za wawakilishi wa wanawake bungeni, ziliundwa kwa minajili ya kuongeza idadi ya wanawake bungeni. Aghalabu wawakilishi hawa wamesikika wakiteta kuwa wanachukuliwa kama pambo tu katika bunge la kitaifa.

Kwa upande wa kulia, mbunge amewakilishwa kama nguruwe kumaanisha kuwa ni mlafi. Hali hii ya wabunge kusawiriwa kama nguruwe, ilitokana na kitendo cha mwanaharakati Boniface Mwangi (BM) kupeleka nguruwe nje ya majengo ya bunge ya nchi ya Kenya kama njia ya kupinga mpango wa wabunge kujiongezea mishahara. Hivyo, msanii anapowasawiri wabunge kama nguruwe anapitisha ujumbe kuwa viongozi hawa ni walafi. Kwenye upande wa chini wa kibonzo hiki, gavana amesawiriwa kama fisi, kumaanisha kuwa wenye kushikilia ofisi hizi ni walafi na wana sifa ya kunyapanyapa. Kwenye sehemu ya mwisho wa Kibonzo $K_3UO$, mwakilishi wa wadi amesawiriwa kama panya. Kwa kawaida panya anachukuliwa kuwa mnyama chafu na ana sifa ya kuguguna na kuwa msumbufu. Hivyo, msanii anamaanisha kuwa mwakilishi wa wadi anachukuliwa kuwa kiongozi wa kitengo cha chini kabisa na hivyo basi ataweza kuguguna tu mali ya umma. Kando na hayo, msanii anapitisha ujumbe kuwa kazi ya wawakilishi wa wadi ni kusumbua tu na hivyo kuwatashtiti kwa tabia zao. Licha ya hayo, Gado alipotumia analojia ya riwaya ya Shamba la Wanyama katika kuelezea ugatuzi nchini Kenya. Usawiri wake ulionyesha ukosefu wa usawa katika vitengo mbalimbali vya uongozi na jinsi viongozi fulani hujiona kuwa wanastahili zaidi kuliko wengi, kama tu nguruwe alivyojipendelea na kujiona mwenye hadhi kuliko wanyama wengine. Kutokana na maelezo haya, mtafiti aligundua kuwa msanii alikuwa anaelezea suala la ukosefu wa usawa katika uongozi wa kaunti na serikali kuu, hali inayoleta utengano katika uongozi wa nchi. Hali inayoibua tashtiti kupitia ushambulizi wa serikali kuu na serikali za kaunti, kwa minajili ya kuchochea mabadiliko.

Waaidha, kutokana na maelezo haya, mtafiti aligundua kuwa Gado aliangazia uongozi wa serikali ya Rais na naibu wake wa mwaka wa 2017 kama uongozi uliojaa viongozi walafi, wenye tabia ya kunyapanyapa mali ya umma na wasiojali maslahi ya wananchi. Kwa kawaida, ofisi za uongozi hupewa hadhi na heshima kubwa, hivyo Gado

anaposawiri rais kama nguruwe, kwa kifupi anamuita Rais nguruwe, hali inayodhihirisha uhuru na ukali katika usawiri wake, hali ambayo haingejitokeza ikiwa alichapisha kibonzo hiki katika magazeti au televisheni. Isitoshe, uangaziaji huu wa uongozi wa vitengo mbalimbali ulikuwa wa kitashtiti.




***Kibonzo 15: $K_4$UO kinyang'anyiro cha ugavana katika Kaunti ya Nairobi. Kutoka (http://gadocartoons.com/nairobi-gubernotorious-race/).***

Hali kadhalika, Gado alitumia matukio katika kibonzo 15, $K_4$UO kuelezea dhana ya uongozi na aina ya viongozi wanaochaguliwa nchini Kenya kwa kuangazia wagombeaji wa kiti cha Ugavana cha Kaunti ya Nairobi kwa njia mbalimbali. Kwenye upande wa kushoto wa kibonzo hiki, msanii ametusawiria mtu aliyemtaja kama Kidero akiwa na pua refu. Kulingana na utamaduni wa nchi za kiafrika, usawiri huu hutumiwa kumaanisha mtu mwongo. Imani hii ilitokana na hadithi ya watoto *Adventures of Pinocchio* (Collodi, 2005). Kazi hii ya kisanaa ilihusu kikaragosi kilichokuwa kimechongwa kwa kutumia ubao lakini kilikuwa na ndoto ya kuwa mvulana halisi aliye hai. Hatimaye, ndoto yake ilitimia na akawa hai. Jambo la kushangaza ni kuwa kila aliponena uongo pua lake lilirefuka. Kutokana na hadithi ile ya *Pinocchio*, watu walianza kuhusisha mtu mwongo na pua ndefu. Hivyo, msanii alikuwa anamtashtiti Kidero kwa kuwa mwongo.


Mchoro wa pili kutoka upande wa kushoto ni mgombeaji aliyesawiriwa kama mtoto aliyevalia suti. Mdomoni ana kitu kinachochukuliwa kuwa ni sigara na kwenye mkono wa kulia ameshika chupa ya mvinyo na kwenye mkono wa kulia ameshika pesa. Kando na hayo, mgombeaji huyu amevalia kiwinda kinachochukuliwa kuwa na kinyesi kutokana na nzi wanaoonekana karibu naye. Usawiri huu wa mgombeaji huyo ulipitisha ujumbe kuwa ingawaje kiongozi huyu ana mali, bado alichukuliwa kuwa na tabia za kitoto ambazo hazifai kwa mtu anayewania wadhifa wowote ule. Isitoshe, msanii alidokeza kuwa mienendo ya mgombeaji huyu haikuwa sawa na ilijihusisha na mambo yasiyokuwa halali na ndiposa akamchora akiwa amesimama kwenye maji chafu. Mgombeaji wa tatu ambaye msanii alimtaja kama PK amesawiriwa kama tumbiri, mwenye masikio marefu na mkia mrefu. Kwa kawaida tumbiri ni mnyama mwenye tabia ya kuruka kutoka kwa mti mmoja hadi mwingine. Kwa msingi huu, mtafiti aligundua kuwa msanii alimsawiri mgombeaji wa tatu kama tumbiri kutokana na tabia yake ya kubadilisha maeneo na hata nyadhifa alizokuwa akigombea. Kwanza kabisa PK ambaye ni Peter Kenneth alikuwa mbunge wa eneo la Gatanga, ambalo ni eneo la ubunge chini ya Kaunti ya Murang'a kwa mihula miwili, kisha katika mwaka wa 2013, akawania kiti cha urais na akashindwa na baadaye katika mwaka wa 2017, alikuwa akigombea kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi. Hivyo, Gado alikuwa anatujuza kuwa mgombeaji PK alikuwa na tabia za tumbiri za kutapatapa na kurukaruka kutoka kiti kimoja hadi kingine na usawiri huu, ulilenga kutashtiti tabia yake ya kukosa msimamo.

Kwenye upande wa kulia wa $K_4UO$, msanii alimsawiri mgombeaji aliyemtaja kama Miguna kama mwenye mdomo uliokuwa kama vuvuzela. Vuvuzela ni kifaa kinachotumika kupigia kelele na kupaza sauti kwenye michezo, makanisa au hata kwenye maandamano. Hivyo, msanii anapomsawiri mgombeaji Miguna kama mwenye mdomo wa vuvuzela anapitisha ujumbe kuwa mgombeaji huyu ni mwenye kelele na maneno mengi tu. Kutokana na usawiri huu wa viongozi mbalimbali waliokuwa wanawania kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi, msanii alikuwa anaonyesha udhaifu wa uongozi na viongozi wa nchi ya Kenya.

Kando na hayo, msanii Gado amekipa kibonzo hiki anwani ya *Nairobi Gubernotorious Race* badala ya Nairobi Gubernatorial Race. Kutokana na anwani hiyo, tunaona kuwa kuna ujumbe maalum ambao msanii alinuia kupitisha kwa hadhira yake. Neno

Gubernotorious huenda limeundwa kutokana na maneno mawili yaliyokatwa na kuunganishwa pamoja, "*Gubernatorial*" lenye maana inayohusu gavana na "*Notorious*" lenye maana ya umaarufu kwa tabia ambayo haikubali katika jamii fulani. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa mtafiti tumia dhana ya "*Gubernotorious*" kutujuza kuwa viongozi waliokuwa wakiwania kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi walikuwa maarafu kwa tabia ambazo hazikukubali katika jamii. Hivyo, gado alitumia dhana ya *Gubernotorious* kuwa tashtiti viongozi hawa kwa tabia zao ambazo alichukulia kuwa zilikuwa hazikubali na jamii.

Aghalabu, watu wanapochagua kiongozi atakayewawakilisha, inachukuliwa kuwa watachagua mtu mwenye tabia za kuigwa na anayeweza kuheshimika. Hivyo, Gado anapotusawiria viongozi ambao ni waongo, wenye tabia za kitoto, wenye mienendo isiyo sawa, na wenye kelele tu anatashtiti aina ya viongozi wanaochaguliwa nchini Kenya na anatumia kibonzo kile kushambulia uongozi wao kwa njia yenye kuthibitisha ukali katika uangaziaji.




***Kibonzo 16: K$_5$UO Kura za Waliowengi dhidi ya Kura za waliteuliwa. Kutoka (www.gadocartoon.com*).**

Msanii ametumia matukio katika Kibonzo K$_5$UO kuelezea mchakato wa kupata uongozi nchini Kenya na hasa yaliyojitokeza katika uchaguzi mkuu wa nchi ya Kenya katika mwaka wa 2017. Katika sehemu ya juu ya kibonzo hiki, tunaonyeshwa taswira ya aliyekuwa mgombeaji urais na kinara wa muungano wa NASA, Raila Odinga aliyepewa kodi ya RO akiwa amevalia joho la rangi ya zambarau huku akiwa amebeba fimbo inayofafana na fimbo ya bunge la nchi ya Kenya. Msanii amemsawiri RO akiwa

uchi kwenye sehemu ya mbele ya mwili wake. Nyuma yake kuna umati uliojumuisha wanawake, wanaume na hata watoto ambao wameshikilia joho lake na wanaonekana kumcheka huku wakimnyoshea vidole. Anwani ya sehemu ile ya kibonzo ina maandishi;

"*Popular Vote"*

*"Kura za Waliowengi"*.

Si jambo la kawaida kwa mtu kutembea akiwa uchi na hasa kuonyesha watu utupu wake. Katika jamii za Kiafrika watu wanaojulikana kutembea uchi ni wachawi au watu waliorukwa na akili. Hivyo, msanii anapomsawiri RO akiwa uchi huenda alitaka kueleza hadhira yake kuwa huenda RO alikuwa anaonyesha wafuasi wake udhaifu alionao kwa kusawiriwa aki uchi.

Katika sehemu ya chini ya kibonzo $K_5$UO, tunaonyeshwa taswira ya Uhuru Kenyatta aliyepewa kodi ya Rais akiwa amevalia joho la rangi nyekundu, taji la ufalme kichwani na mkononi kuna fimbo inayofanana na fimbo ya bunge la nchi ya Kenya. Nyuma yake kuna wanajeshi wanaoonekana wakiwa wameshikilia joho lake huku wakilindwa na wengine waliojihami. Anwani ya sehemu hii ya kibonzo ina maneno *Electoral College*. Kwenye upande wa kulia wa kibonzo hiki kuna kijibonzo kingine kidogo kinachoonekana kushangazwa na yanayotokea.

Kwanza, dhana za *Popular vote* na *Electoral College* ni dhana ambazo zimekopwa kutoka kwa mfumo wa uchaguzi wa Marekani. Kule Marekani, mgombeaji yeyote wa viti mbalimbali vya uongozi hushinda uchaguzi kutokana na kura za walio wengi *Popular Vote* na kura hizi hutokana na wananchi waliosajiliwa kama wapiga kura. Hata hivyo, uchaguzi wa urais na naibu wake hutokana na kura za wapiga kura waliochaguliwa kutokana na sampuli kubwa ya wapiga kura wote nchini na sampuli ya wapigaji kura hawa hujulikana kama *Electoral College*. Hivyo, ushindi wa kiti cha urais na naibu rais hautokani na wananchi wote bali ni kwa wapiga kura walioteuliwa kutokana na sampuli kubwa ya wananchi (*Presidential election process*, 2022). Hivyo msanii anapotumia dhana hizi mbili kuelezea uchaguzi mkuu wa mwaka 2017, huenda anadokeza kuwa mgombeaji RO alikuwa ndiye rais wa jamhuri ya Kenya kutokana na kura za walio wengi lakini Uhuru Kenyatta ndiye aliyeshinda kwa kuwa alichaguliwa na wapiga kura waliokuwa wamechaguliwa na katika hali hii, msanii anadokeza kuwa

taasisi za kijeshi ndizo zilihakikisha kuwa Rais ndiye aliyeshinda kinyang'anyiro cha urais.

Kando na hayo, msanii anatusawiria RO na Rais wakiwa uchi hasa sehemu za mbele za mwili wao. Usawiri huu, unalingana na hadithi ya watoto "*The Emperor's New Clothes*" iliyoandikwa na Hans Christian Andersen. Hadithi ile ilihusu mfalme mkuu aliyependa kuvalia nguo za thamani na zilizopendeza. Ilisemekana kuwa alikuwa na nguo ya kila wakati wa siku. Siku moja kukaja wezi wawili katika himaya yake na wakamweleza mfalme mkuu kuwa walikuwa na uwezo wa kumtengenezea nguo ambayo ni wajinga tu hawangeweza kuiona. Mfalme mkuu alifurahishwa na wazo la nguo ile na akaagiza atengenezewe nguo ile kwa minajili ya kutambua watu werevu katika himaya yake. Wezi wale wakajifanya kuanza kazi na baada ya siku kadhaa, mfalme mkuu alienda kuangalia mafundi walikuwa wamefikisha wapi kushona nguo yake. Alipofika kwenye karakana hakukuwa na nguo yoyote na akakasirika sana, lakini hakuambia yeyote kuwa hakuna nguo.


Baadaye, alituma mawaziri wake kwenda kuangalia mafundi walikuwa wamefikisha wapi shughuli ya kumshonea mfalme mkuu nguo yake. Siku moja wezi wale waliamua kuwa wamemaliza kushona nguo ya mfalme na wakaipeleka kwa mfalme na kujifanya kuwa wanamvalisha nguo hiyo. Baada ya kujifanya kuwa wamemvalisha mfalme mkuu nguo ile, mfalme mkuu pamoja na mawaziri wake waliandamana kwenye vitongoji vya himaya yake kwa minajili ya kuwaonyesha watu "nguo" ya mfalme. Kwa kuwa watu walihofia kutambulika kama wajinga hakuna aliyethubutu kumweleza mfalme mkuu kuwa alikuwa uchi isipokuwa kijana mmoja mchanga aliyepasa sauti na kusema;

> *But the King is Naked*
> *Lakini Mfalme ako Uchi*.

Hali ya msanii kuwasawiri wagombeaji hawa wawili wakiwa uchi inatuelekeza kwenye tabia ya watu walio karibu na viongozi hawa, ambao kazi yao ni kuwasifu viongozi hata wanapofanya mambo ya kijinga. Kwa mfano, nchini Kenya inadaiwa kuwa wafuasi wa RO ni waaminifu kwa kiongozi huyu kiasi kwamba anaweza kuwaongoza wafuasi wake mpaka pembeni mwa mwamba na wafuasi wake watamfuata tu. Msanii anatuonyesha taswira ya wananchi wakimfuata RO huku wakiwa wameshikilia joho lake, ishara tosha kuwa wako tayari kumfuata kokote atakapowaongoza. Kando na

hayo, Rais anaposawiriwa akisindikizwa na wanajeshi waliovalia sare kamili, na kichwani ana taji la kifalme na mkononi fimbo ya bunge, msanii anatuelezea kuwa Rais anatumia kitengo cha jeshi kutekeleza anayotaka nchini.

Gado anapomsawiri Rais akiwa amevalia taji la kifalme anamtashtiti kwa tabia yake ya kuongoza nchi ya Kenya jinsi apendavyo na kana kwamba ni himaya yake. Zaidi ya hayo, fimbo ya bunge, husimamia mamlaka ya Spika wa bunge na hivyo Rais akisawiriwa akiwa amebeba fimbo ile, msanii anapitisha ujumbe kuwa Rais amechukua mamlaka ya Spika wa bunge la kitaifa na huenda anamtumia kupitisha sheria anazozitaka mwenyewe. Hivyo, kutokana na matukio ya Kibonzo K$_5$UO, msanii alikuwa anatashtiti Rais na RO kwa tabia zao na pia alikuwa anazindua hadhira yake kuhusu uongozi wa kidikteta uliokuwa ukiendelezwa na Rais.




***Kibonzo 19: K$_6$UO Kubuni Upya Gurudumu la Wananchi. Kutoka (www.gadocartoons.com)***.

Kibonzo 19, K$_6$UO vilevile kinachimuza maudhui ya uongozi nchini Kenya. Msanii anatusawiria picha ya mwanaume na mwanamke wakivuta mkokoteni uliowabeba Rais na Naibu Rais. Katika kibonzo hiki, Rais amechorwa kama mfalme aliyevalia nguo za kifalme naye Naibu Rais amesawiriwa kama mwanamke mja mzito. Mwanamume na mwanamke wanaovuta mkokoteni wamevalia nguo zenye viraka na hawana viatu miguuni na wanaonekana wakivuta mkokoteni kwenye mlima uliojaa mawe. Cha kushangaza ni kuwa, mkokoteni wenyewe una magurudumu ya umbo la miraba minne

badala ya magurudumu duara. Msanii anatuonyesha taswira ya magurudumu ya duara yakiwa yametolewa kwenye mkokoteni na kutupwa. Anwani ya kibonzo hiki ni;

*Re-Inventing the WHEEL of the People*

*Kuunda upya gurudumu la wananchi*".


Rais anaposawiriwa akiwa amevalia nguo za kifalme ilhali anaongoza nchi ya kidemokrasia, ni ishara kuwa uongozi wake hauelekezwi na matakwa ya wananchi lakini matakwa yake binafsi. Nchi zinazoongozwa na wafalme hazina nafasi ya demokrasia na usemi wa mfalme huchukuliwa kuwa sheria. Hivyo, msanii anapomsawiri Rais kama mfalme, anamtashtiti Rais kwa kuongoza nchi ya Kenya kama himaya yake ambapo asemacho ni sheria, hali ambayo haiwezekani katika nchi ya kidemokrasia. Kwa kifupi, msanii alikuwa anamsawiri Rais wa nchi ya Kenya wa mwaka wa 2017 kama dikteta aliyetawala nchi huru ya Kenya kama himaya yake.

Kwa upande mwingine, Gado anamsawiri Naibu Rais kama mwanamke mjamzito kuashiria matarajio ya azma yake ya kuchukua uongozi baada ya kustaafu kwa Rais. Uangaziaji huu wa Naibu Rais ulilenga kutashtiti tabia yake ya kufikiria kuhusu azma yake ya kuchukua hatamu ilhali hashughuliki na hali ya maisha ya wananchi. Kando na hayo, taswira ya mwanamke na mwanamume kuvuta mkokoteni wenye magurudumu ya miraba minne kwenye mlima uliojaa mawe, imetumika kuzindua hadhira ya msanii, kuhusu uongozi wa Rais unaohujumu na kuwabebesha wananchi mzigo mzito wasioweza kubeba. Ugumu wa kukwea mlima uliojaa mawe na kuvuta mkokoteni mzito wenye magurudumu ya miraba minne, unaashiria ugumu wa maisha ya wananchi chini ya uongozi wa Rais na Naibu Rais. Hii ni mojawapo wa sifa za uongozi mbaya.

### 4.2.2 Unyanyasaji wa Wafanyikazi

Chini ya maudhui ya uongozi, mtafiti aliangazia maudhui ya unyanyasaji wa wafanyikazi uliotokana na uongozi wa Rais na Naibu Rais wa nchi ya Kenya. Wakati ambapo walioaminiwa na nyadhifa za uongozi hukiuka maadili na matakwa ya wanajamii, basi tunaweza kusema kuwa jamii hiyo iko chini ya uongozi unaowanyanyasa wananchi. Katika shughuli ya ukusanyaji data, mtafiti alikumbana na vibonzo vilivyoendeleza maudhui ya uongozi mbaya kupitia unyanyasaji wa wafanyikazi.

**Gov and The Doctor's Strike**




**Kibonzo 1: $K_1$UWW, Serikali na Mgomo wa Madaktari. Kutoka (*http://gadocartoons.com/govt-doctors-strike/*).**

Kwa mfano, katika Kibonzo $K_1$UWW, Gado anatuonyesha hali ilivyokuwa nchini Kenya baada ya mgomo wa madaktari uliokuwepo kwa siku mia moja. Madaktari na wauguzi walioajiriwa na serikali walikuwa wanataka kuongezewa mishahara na serikali iwapatie mazingira bora ya kufanyia kazi yao. Katika kibonzo hiki msanii alituonyesha taswira ya watu walionekana kana kwamba wamekwisha kufa waliokuwa wamerundikwa kwenye kitanda kimoja bila kujali jinsia au mauguzi yao. Kwenye upande wa kushoto wa kibonzo $K_1$UWW, kuna wagonjwa wengine waliolazwa sakafuni na karatasi na chupa za dawa zilikuwa zimetapakaa kila mahali. Kutokana na usawiri huu, mtafiti alipata ujumbe kuwa hospitali nchini Kenya hazikuwa na miundo msingi ya kutosha.

Katika picha hii, wagonjwa au wafu wa kike na wa kiume walikuwa wamewekwa kwenye kitanda kimoja na wengine walikuwa wamelala sakafuni, ishara tosha kuwa hospitali hazina miundo msingi za kutosha na wakati mwingine huenda hazipo. Kwa upande mmoja wa kibonzo kile msanii anatuonyesha Rais na Naibu Rais wakiwa wameshika gazeti lenye maandishi;

*Doctors jailed as patients continue to die*

*Madaktari wafungwa huku wagonjwa wakiendelea kufa.*

Kando na hayo, tunaonyeshwa Naibu Rais akimwambia Rais atafakari ni kura ngapi wanazopoteza kutokana na wagonjwa kufa. Pembeni mwa kibonzo kile kuna kijibonzo kingine kidogo kinaonekana kikisema kuwa wagonjwa wale wanaweza kusajiliwa bado wakiwa katika hali ile. Usemi huu kutoka kwa kijibonzo hiki, unazua kinaya kwani, kulingana na katiba ya chini ya Kenya, watu ambao wanapaswa kusajili ni watu walio timia miaka kumi na minane na walio na akili timamu. Hivyo usemi huu wa kijibonzo unazua hali ya unyume na huenda pia ulikuwa unadokezea yaliyokuwa yakijiri nchini Kenya katika uchaguzi wa hapo awali ambao hata wafu walipiga kura kama njia ya kuiba kura katika uchagui mkuu. (Afp, 2020)

Matukio katika Kibonzo, $K_1$UWW yalidhihirisha hali ya viongozi kuwanyanyasa wafanyikazi na wananchi kwa kuwanyima haki zao za kimsingi. Katika nchi ya Kenya ni haki ya kila mwananchi kupata matibabu bora anapoenda hospitalini. Zaidi ya hayo, sheria za nchi ya Kenya zinaamuru kila mfanyikazi kuwa na mazingira bora na salama ya kufanyia kazi pamoja na msharara unaolingana na kazi ambayo mtu anafanya. Katika kibonzo $K_1$UWW, msanii anapotuonyesha taswira ya Rais na Naibu Rais wakiwa wameshika gazeti lenye maandishi kuwa, madaktari wanafungwa jela ilhali wagonjwa wanaendelea kufa hospitalini. Maneno hayo alinuia kutashtiti serikali ya Rais na Naibu Rais kwa kutowajali wafanyikazi wao.

Hali ya madaktari kufungwa jela kwa kutetea haki zao, kupitia maandamano na migomo ambayo imekubalishwa na katiba ya nchi ya Kenya ni mojawapo wa sifa za uongozi mbaya wenye kuwahujumu wafanyikazi. Msanii alituonyesha jinsi serikali ya Rais na naibu wake ilivyowanyanyasa na kuwanyima madaktari haki ya malipo bora na mazingira bora ya kufanyia kazi. Usawiri wa wagonjwa au wafu waliorundikwa kwenye kitanda kimoja bila dawa au madaktari wa kuwatibu, ilidhihirisha ukiukaji wa malengo ya uongozi kwa upande wa serikali. Kwa kifupi, Gado alitumia Kibonzo $K_1$UWW, kutashtiti Rais na Naibu Rais kwa kuwanyima wafanyikazi wao haki zao. Msanii anapotuonyesha Naibu Rais akifikiria kuhusu kura walizokuwa wakipoteza badala ya kufikiria jinsi watakavyookoa maisha ya wananchi ni ishara tosha kuwa viongozi hawa hawajali maslahi ya wananchi wao na si viongozi kwa hakika.

**Doctors Vs Govt – An Abusive Marriage**




***Kibonzo 5: $K_2$UWW. Madaktari dhidi ya Serikali- Ndoa ya unyanyasaji. Kutoka*** **(http://gadocartoons.com/doctors-vs-govt-abusive-marriage/).**

Katika Kibonzo $K_2$WW msanii anatuonyesha taswira ya Rais akimchapa mwanamke aliyevalia nguo zilizoandikwa *Doctors.* Nyuma ya Rais tunaona taswira ya Naibu Rais akiwa ameshikilia taji la ufalme la rais na nyuma yake kuna watu wawili. Mmoja wao hatuonyeshwi uso wake na mwingine ana uso wa paka. Kwenye upande wa kushoto wa kibonzo hiki, kuna Imam na mtu anayechukuliwa kuwa mchungaji kutokana na mavazi yake. Nyuma ya mchungaji na Imam kuna umati unaoonekana kustaajabika.

Kwenye upande wa kushoto wa kibonzo hiki, msanii anatuonyesha taswira ya mwanamke akisema;

*It has been an abusive marriage*
*hii imekuwa ndoa ya unyanyasaji*

Naye Rais anaonekana akijibu,

*Stay out of this, let me sort her out!*
*msijihusishe na haya, wacheni ni mshughulikie!*

Kwa kawaida, katika jamii nyingi wanawake hufanya kazi ya kutunza familia zao. Hivyo, msanii anapowasawiri madaktari kama mwanamke anapitisha ujumbe kuwa kazi ya madaktari ni kuwajali na kuwatunza wagonjwa. Hata hivyo, msanii anapomsawiri Rais akimchapa mwanamke na kuwaonya watu wasiingilie mambo yao


kwa kuwa anataka kumshughulikia mwanamke yule kwa kumchapa, msanii anapitisha ujumbe kuwa uhusiano kati ya Rais na madaktari ni uhusiano wa kinyanyasaji. Pale ambapo mwenye nguvu, ambaye ni Rais anawahujumu na kuwanyanyasa wanyonge ambao ni madaktari. Kando na hayo, msanii anapotuonyesha mwanamke anayeonekana akisema kuwa, hii imekuwa ndoa ya unyanyasaji anatueleza kuwa kuna jambo lisilo la kawaida linajitokeza katika uhusiano wa madaktari na serikali ya Rais na Naibu Rais.

Kwa kawaida ndoa huwa kati ya watu wawili wanaopendana na wameamua kuishi pamoja kwa upendo. Mwanamume anapaswa kumpenda mkewe na mwanamke anapaswa kumheshimu mumewe. Hivyo, msanii anapotusawiria ndoa ambayo mwanamke anachapwa na mumewe, msanii anatusawiria hali ya mnyonge kunyanyaswa na mwenye nguvu. Kwa kifupi, msanii analinganisha uhusiano kati ya madaktari na serikali ya Rais na Naibu Rais na ndoa yenye unyanyasaji kwa minajili ya kuendeleza maudhui ya unyanyasaji wa wafanyikazi. Tendo la Rais kusawiriwa akiwaadhibu madaktari ni ishara tosha kuwa uongozi wake haukuwa tayari kusikiza na kukidhi mahitaji ya madaktari walioajiriwa na serikali yake.

Kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa maudhui ya uongozi wa serikali ya Rais na Naibu Rais yalijitokeza kupitia hali kama vile; kutowajibika kwa viongozi hawa wawili, kutokidhi mahitaji ya kimsingi ya wananchi na unyanyasaji wa wafanyikazi walioajiri wa serikali ya nchi ya Kenya. Gado alipoangazia uongozi wa Rais na naibu wake, alitashtiti viongozi hawa kwa kuwa watu wasiowajibika, wenyewe kutumia mamlaka yao kuwanyanyasa wanyonge na watu ambao hawafai kuwa viongozi.

### 4.2.3 Ulaghai katika Siasa

Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja inaelezea ulaghai kama uwongo unaotumiwa na mtu kwa manufaa yake binafsi. Katika jamii nyingi ulimwenguni, siasa huchukuliwa kuwa mchezo wa kushindana nguvu, na watu hutumia mbinu zozote zile kuhakikisha wameibuka washindi katika ulingo wa siasa. Katika shughuli za kuchanganua data ya utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa baadhi ya vibonzo vya msanii Gado vilivyoteuliwa vilidhihirisha ukweli kuwa wanasiasa hutumia ulaghai kama mojawapo ya mbinu za kuhakikisha kuwa wameibuka washindi katika vinyang’anyiro vya viti mbalimbali. Maudhui ya ulaghai katika siasa yalijitokeza sana katika vibonzo vilivyosawiri kampeni za uchaguzi wa 2017 na siasa za nchi ya Kenya kwa jumla.




***Kibonzo 2: $K_1$UKS Kampeni za NASA: Kutoka (<u>http://gadocartoons.com/nasa-and-their-campaign/</u>.***

Kwa mfano; Kibonzo $K_1$UKS kilionyesha vinara wa muungano wa NASA walivyokuwa wanajaribu kuwarai wanasiasa mbalimbali kuungana nao kwa ahadi kuwa wangepata nyadhifa mbalimbali serikalini. Katika $K_1$UKS msanii alimchora kiongozi wa muungano wa NASA, RO akiwa ameshikilia mlingoti uliokuwa na bendera iliyoandikwa *FLAG BEARER* na kwenye mlingoti huo vinara wenza Musalia Mudavadi (MM), Moses Wetangula (MW) na Kalonzo Musyoka (KM) walionekana wakiwaashiria wanasiasa wale wengine kuwa mambo yako shwari kwa kuwaonyesha kidole cha gumba. Kwenye bendera iliyoandikia "*Flag Bearer"* kuna umbwi ambaye mwonekano wake wa uso unalandana na Kalonzo Musyoka (KM)

Katika $K_1$UKS, vyeo vya serikali vimesawiriwa kama kuku aliyeonekana akitoa harufu ya kuvutia. Msanii ametumia matukio katika kibonzo $K_1$UKS kuelezea hali ilivyokuwa katika kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017. Kama mtafiti alivyokuwa ameeleza awali, kinyang'anyiro cha urais na cha wabunge, kilikuwa kati ya vyama viwili, chama cha Jubilee, ambacho viongozi wao walikuwa Rais na Naibu Rais na muungano wa NASA uliokuwa umeundwa na viongozi RO, KM, MM na MW. Katika kipindi hiki, kulikuwa na mvutano katika muungano wa NASA kuhusu ni nani angepeperusha bendera ya chama chao katika kinyang'anyiro cha urais, na ndiposa

msanii akawasawiri viongozi hawa wanne wakiwa wameshikilia mlingoti uliokuwa umeandikwa "*Flag Bearer*".

Baada ya vuta ni kuvute, kinara wa NASA, RO alipata uongozi wa muungano wa NASA na naibu wake akawa KM. katika kibonzo hiki KM amesawiriwa kama umbwi ambaye anatabia kutembea polepole na ni kana kwamba huwa ananyemelea. Zaidi ya hayo, umbwi anatabia ya kubadili rangi kulingana na mazingira yake. Hivyo, huenda Gado alimsawiri KM kama umbwi kama njia ya kumtashtiti kwa tabia yake ya kubadili rangi kulingana na mazingira yake kama njia ya kujikinga na kuhakikisha kuwa yuko salama kisiasa.

Isitoshe, msanii anaposawiri nyadhifa mbalimbali za serikali kama kuku aliye na harufu ya kuvutia, alipitisha ujumbe kuwa, muungano na NASA ulikuwa unajaribu kuwarai wanasiasa. Ulaghai katika kibonzo hiki ulijitokeza pale ambapo nyadhifa za serikali zimesawiri kama jambo la kuvutia ilhali vimewekwa ndani ya mtego. Hivyo, msanii alijaribu kupitisha ujumbe kuwa kujiunga na muungano wa NASA ni kama kujipeleka kwenye mtego unaojua kuwa utakunasa tu. Kibonzo $K_1$UKS kinaonyesha jinsi wanasiasa mbalimbali hutumia uwongo kuwarai wananchi kwa manufaa yao wenyewe.

Kutokana na maelezo haya, Gado alisawiri viongozi wa NASA kama walaghai na muungano wao ulichorwa kama mtego tu unaowanasa wanasiasa na kuwaangamiza. Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki na hasa mhimili wa kiishara kama ulivyoelezwa na Wamitila (2002), kwa kawaida, unapotaka kumshika panya kwenye mtego, huwa unateka nathari yake kwa chakula kinachotoa harufu nzuri, ndiposa aingie kwenye mtego. Vivyo hivyo, msanii alitumia ishara ya mtego, uliokuwa na kuku aliyetoa harufu nzuri na ulioandikwa NASA, kuwatega wanasiasa waliolaghaiwa kujiunga na muungano wa NASA, huku wakiwa na matumaini kuwa wangepata nyadhifa mbalimbali ambazo kwa hakika viongozi wa NASA hawakuwa nazo. Basi, msanii alikuwa anamaanisha kuwa viongozi hawa wa NASA walikuwa walaghai na alikuwa anawatashtiti, jambo ambalo kwa kawaida hangelisawiri kwa wazi ikiwa alikuwa anachapisha kibonzo hiki kwenye magazeti au televisheni, lakini kutokana na uhuru alioupata kutokana na kutumia tovuti yake binafsi, aliweza kusawiri masuala kama alivyoyaona bila kudhibitiwa.

**Oloo Joins NASA**




***Kibonzo 4: $K_2$UKS, Oloo ajiunga na NASA. Kutoka (http://gadocartoons.com/oloo-joins-nasa/).***


Mfano mwingine wa ulaghai katika siasa unajitokeza katika Kibonzo $K_2$UKS. Katika kibonzo hiki msanii alituonyesha Waheshimiwa RO, MW, MM na KM wakiwa juu ya Punda aliyeandikwa NASA. Punda yule anaonekana kuwa kwenye mbio na mtu aliyetajwa kama Oloo anaonekana akiwa ameshikilia mkia wa punda anayetoa kinyesi. Oloo alikuwa Katibu Mkuu wa chama cha TNA, chama ambacho kilitumika kuunda chama cha Jubilee katika mwaka wa 2013. Katika kibonzo kile, Oloo anaonekana akiwaambia vinara wa NASA kuwa;

> *I helped Jubilee to steal the last election... Now i'm going to help NASA to steal the election…!*
>
> *Nilisaidia Jubilee kuiba kura katika uchaguzi uliopita na sasa nitasaida NASA kuiba uchaguzi huu*..!

Hali ya msanii kuchagua punda kusawiri muungano wa NASA ulitokana na msemo uliokuwepo katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2017, kuwa hekaheka za uchaguzi zilikuwa kati ya wanyama wawili, farasi na punda. Ambapo chama cha Jubilee kilikuwa farasi na muungano wa NASA ulikuwa punda.

Kando na hayo, msanii anapotuonyesha taswira ya Oloo akiwa ameshikilia mkia wa punda aliyekuwa akitoa kinyesi, anatuonyesha kuwa yale yaliyokuwa yakisemwa na Oloo hayakuwa na maana au manufaa yoyote na ndiposa akayalinganisha na kinyesi

cha punda ambacho hakina manufaa yoyote, na ufasili huu tunaupata kwa msingi wa mhimili wa kirejelezi chini ya nadharia ya Semiotiki kama ilivyofafanuliwa na Wamitila (2002). Matukio katika kibonzo $K_2$UKS yanaonyesha udanganyifu katika shughuli ya uchaguzi kwa kupanga kuiba kura, ilhali tunajua shughuli ya uchaguzi inapaswa kuwa huru, ya haki na ya kidemokrasia. Hivyo tunapoona ahadi ya wizi wa kura tunajiuliza ikiwa ni kweli kuwa serikali ya Jubilee ilipata uongozi kupitia mbinu za udanganyifu. Pili, Oloo alipowaahidi vinara wa NASA kuwa atawasaidia kuiba kura akiwa kwenye upande wao, uwongo unajitokeza pale kwani inaonekana ni kana kwamba anatafuta mbinu ya kuingia kwenye mrengo wa NASA baada ya kutemwa na serikali ya Jubilee. Mintarafu ya maelezo haya, tunaona kuwa Gado alikuwa anatashtiti viongozi wa mirengo yote miwili, Jubilee na NASA kwa ulaghai wao. Katika jamii za kiafrika, kinyesi cha punda hakina manufaa yoyote; hakiwezi kutumika kama mbolea na hivyo huachwa tu kikakauka tu. Kwa hivyo, Gado anapotusawiria ahadi ya Oloo kama kinyesi cha punda, anatueleza kuwa ahadi zake hazina maana yoyote kwa muungano wa NASA kwa kuwa hakuna siku punda atakuja kumshinda farasi katika mbio.




***Kibonzo 10: $K_3$UKS, Kukodisha na kununua shahada. Kutoka (www.gadocartoons.com*).**

Maudhui ya ulaghai katika siasa yanajitokeza katika kibonzo10: $K_3$UKS, ambapo msanii anatuonyesha taswira ya viongozi mbalimbali wanaowania viti vya ugavana nchini Kenya. Kwenye upande wa juu wa kibonzo hiki alituonyesha viongozi waliotajwa kama Baba Yao ambaye alipewa kodi ya BY na mwenzake aliyetajwa kama Dr. Nyoro ambaye alipewa kodi ya DN. katika mchoro huo. BY, anaonyeshwa akisema;

*Why struggle to get a fake degree while you can hire a real one…*

*Mbona ujisumbue kupata shahada ghushi ilhali unaweza kodisha shahada halali…*

Kwa upande wa chini wa $K_3$UKS msanii anatuonyesha kiongozi aliyetajwa kama Igathe na aliyepewa kodi ya PI kusimamia (Polycarp Igathe) na mwenzake aliyechorwa akiwa amevalia mikufu, miwani ya jua na koti refu lililochorwa ishara ya dola. Aghalabu katika ishara ya dola hutumika kuashiri pesa na tena pesa nyingi kwani dola inathamani ya juu ikilinganishwa na shilingi ya Kenya. Hivyo Gado anapomsawiri Mike Sonko akiwa na mikufu, miwani ya jua na koti lenye ishara ya dola anamaanisha kuwa alikuwa tajiri.

Ni vyema kufafanua kuwa waliokuwa wakiwania kiti cha ugavana na unaibu gavana katika Kaunti ya Nairobi katika mwaka wa 2017, walikuwa Polycarp Igathe (naibu gavana) aliyepewa kodi ya PI na Mike Sonko (gavana) aliyepewa kodi ya MS. Katika kibonzo hiki MS alionekana akisema;

*…Better still, why buy a fake paper degree while you can buy a walking one…*

*…Mbona ununua karatasi ghushi la shahada ilhadi unaweza nunua shahada inayotembea.*

Hapa MS anadokezea kuwa shahada inayotembea ni naibu wake PI ambaye alikuwa amesoma hadi kiwango cha uzamili.

Pembeni mwa kibonzo hiki mna kijibonzo kingine kidogo kinachosema kuwa viongozi hawa wanaweza bahatika na kupata "shahada" yenye akili pia. Matukio katika kibonzo hiki yalionyesha udanganyifu unaotumika na viongozi kwa minajili ya kupata vyeo. Kwa upande mmoja tunaona wazo la kununua shahada ghushi au kukodisha shahada halali na upande mwingine tunapata wazo la "kumnunua" mtu mwenye shahada ndiposa waweze kuwania ugavana. Kutokana na maelezo haya, msanii anatuonyesha taswira ya viongozi wanaopenda njia za mkato, ambao hawapendi kufuata sheria zilizowekwa na watu ambao wako tayari kufanya lolote kupata wanachotaka. Waliounda sheria za Kenya na hasa zilizohusiana na watu waliotaka kuwania viti vya ugavana, walitaka viongozi waliokuwa wamesoma hadi kwenye kiwango cha shahada ya kwanza na watu waliokuwa waadilifu. Hivyo, Gado anapotusawiria viongozi wanaonunua na kukodi shahada ghushi anatuelezea kuwa waliokuwa wakiwania viti vya ugavana katika Kaunti za Kiambu na Nairobi, waliokuwa viongozi ambao si

waadilifu na walikuwa walaghai na msanii alitumia Kibonzo $K_3$UKS, kutashtiti viongozi kwa kuwalaghai na watu wadanganyifu waliopenda njia za mkato.

### 4.2.4 Ufisadi

Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja inafafanua dhana ya ufisadi kwa njia mbili. Kwanza kabisa, inaeleza dhana hii kama utoaji na upokeaji wa hongo. Pili, inafafanua ufisadi kama utumiaji mbaya wa mali ya chama, shirika au serikali. Kwa kifupi ufisadi ni tabia ya ubadhirifu. Sababu kuu ya mtu yeyote yule kujishughulisha na ufisadi ni kwa nia ya kujinufaisha yeye mwenye.





***Kibonzo 6: $K_1$UF Kongamano la ugatuzi la mwaka wa 2017. Kutoka (http://gadocartoons.com/devolution-conference-2017/).***

Kwenye utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa msanii alisawiri ufisadi kwa njia mbalimbali. Kuna pale ambapo alieleza mambo wazi wazi na pale ambapo alitumia mafumbo. Kwa mfano; katika kibonzo 6, $K_1$UF msanii alitumia mafumbo kuelezea dhana ya ufisadi. Katika kibonzo hiki, tunaonyeshwa kongamano la nne la ugatuzi la mwaka wa 2017. Kwenye kibonzo kile msanii ametusawiria helikopta nyingi zilizopaa angani na chini yake tunaona wananchi wakisema;

> *Ooh we are making progress…before they used to arrive in cars!*
> *Ah tunapiga hatua…. Hapo mbeleni walikuwa wanatumia magari*!

Tangu kuanzishwa kwa mfumo wa ugatuzi nchini Kenya katika mwaka wa 2013, kaunti zilizoundwa kutokana na ugatuzi zimekuwa zikiandaa kongomano kila mwaka tangu mwaka wa 2014.

Waliohudhuria makongomano haya ni viongozi mbalimbali wa kaunti pamoja na wawekezaji walionuia kuwekeza kwenye kaunti mbalimbali. Tangu makongamano haya yaasisiwe, viongozi hawa walionekana wakienda kwenye mikutano hii kwa magari makubwa makubwa. Hivyo msanii anaposawiri kongamano la mwaka wa 2017 viongozi wakiwasili kwa helikopta alikuwa anakejeli hali ya viongozi kutumia mali ya umma kuonyesha ubabe, starehe na utajiri ilhali wananchi wanaofaa kuwashughulikia hawana mahitaji yao ya kimsingi. Kwa msingi wa nadharia ya semiotiki, hasa mhimili wa kiishara na kirejelezi, ndege ni ishara ya utajiri na uwezo, katika nchi ya Kenya si jambo la kawaida kwa mtu wa kawaida kutumia ndege kwa safari za ndani ya nchi. Safari za helikopta huwa jambo la kawaida kwa viongozi na matajiri, hivyo msanii alipotusawiria viongozi wakiwasili kwa ndege alitashtiti tabia yao ya kuonyesha ubabe na utajiri wao huku wananchi hawana mahitaji yao ya kimsingi. Kando na hayo, msanii anapotuonyesha taswira ya mwanamke akisema; "Ah tunapiga hatua…. hapo mbeleni walikuwa wanatumia magari!" alikuwa anatumia kinaya kupitisha ujumbe kuwa wanaopiga hatua ni wanasiasa na wala sio wananchi. Matukio ya K1UF yanatumia njia fiche kuendeleza maudhui ya ufisadi.




***Kibonzo 13: K2UF Lala Salama Mfanyikazi Mnyenyekevu. Kutoka*** **(http://gadocartoons.com/rip-humble-civil-servant/).**

Kando na hayo, suala la ufisadi linajitokeza katika kibonzo 13, $K_2UF$, ambapo Gado anatuonyesha taswira ya hafla ya mazishi ya mfanyikazi wa serikali. Mbele ya hadhira iliyohudhuria mazishi yale kuna jeneza lililofunikwa kwa bendera ya nchi ya Kenya. Kwa kawaida, bendera huwekwa juu ya jeneza za viongozi, wanajeshi na watu mashuhuri katika serikali, hivyo huenda msanii alitaka kutujuza kuwa mazishi yake yalikuwa ya mtu mashuhuri katika serikali au mwanajeshi. Kando ya jeneza lile kuna mkono unaoonekana ukimpatia padre kitita cha pesa ambacho padre anaweka mfukoni mwake. Jeneza lenyewe limewekwa juu ya meza iliyoficha mifupa ya watu na kule chini kuna mabango yaliyoandikwa;

> *Grand Theft, Murder Inc, Corruption*
> *Wizi Wa Ngazi Ya Juu, Mauaji Ufisadi.*

Gado anapotuonyesha maneno *wizi wa ngazi ya juu, mauaji na ufisadi*, yakiwa yamefichwa chini ya meza iliyowekelewa jeneza la mwendazake, anapitisha ujumbe kuwa mwendazake aliyetajwa kama mfanyikazi wa serikali mnyenyekevu, alikuwa mfisadi, muuaji na mwizi wa ngazi ya juu; lakini kwa kuwa katika jamii za kiafrika watu huwa hawataji maovu yaliyotendwa na mtu wakati wa kufa kwake, padre anaonelea amsifu kama mfanyikazi mnyenyekevu aliyewatumikia wananchi maisha yake yote jambo ambalo ni kinyume na picha anayotuchorea msanii.

Zaidi ya hayo, Kwenye upande wa juu wa $K_2UF$, msanii anatuonyesha padre akielezea kuwa mwendazake alikuwa mfanyikazi mnyenyekevu na aliyejitolea mhanga kuwatumikia wanachi. Na hivyo, mtafiti anakisia huenda padre anamsifu mwendazake kwa kuwa amekuwa akitoa michango kanisani na haya tunayapata kutokana na taswira ya mkono unaochimuza kutoka kwenye jeneza ukimpatia padre kitita cha pesa. Katika nchi ya Kenya, wanasiasa wana tabia ya kuwapelekea viongozi wa madhehebu pesa hasa wakati wa kampeni, wakidai kuwa ni sadaka au ni michango kwa miradi ya madhehebu. Mara nyingi, pesa hizi huwa njia ya kuwafumba viongozi wa madhehebu ndiposa wasizungumzie maovu yanayofanywa na wanasiasa. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa msanii, alikuwa akiwatashtiti viongozi wa madhehebu kwa kuwa wafisadi. Isitoshe, tunagundua kuwa msanii alitumia uhuru huo mpya unaotokana na uchapishaji wa vibonzo kwenye mitandao kueleza kwa uwazi maovu yanayotendwa na wanasiasa na wafanyikazi wa serikali, pamoja na unafiki unaoendelezwa na viongozi

wa madhehebu ambao wanapaswa kuwa mwanga kwa jamii na kazi yao kubwa ni kukosoa wafuasi wao na kuwaongoza kwenye njia za kweli na haki.




***Kibonzo 14: K3UF Majini yametoka kwenye chupa #Unyakuzi wa Ardhi.* (www.gadocartoons.com)**.


Kulingana na maelezo yaliyotolewa hapo awali kuhusu ufisadi, suala la unyakuzi wa ardhi iliyotengewa umma ni ufisadi. Msanii alisawiri suala la ufisadi kupitia unyakuzi wa ardhi ya umma kupitia kibonzo 14 K3UF ambapo alimchora Rais akifungua nyungu iliyokuwa na maandishi;

*Land Grabbing*
*Unyakuzi Wa Ardhi Ya Umma*

na mle ndani ya chupa kunaonekana mvuke wa kijani kibichi uliokuwa na nyuso za viongozi mbalimbali kama vile; hayati Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya, hayati Rais wa pili wa Jamhuri ya Kenya, Rais wa tatu wa Jamhuri ya Kenya, Naibu Rais, Mheshimiwa MM wa muungano wa NASA kuna uso wa mtu aliyevalia nguo zinazofanana na za askofu, na mwanamume anayechukuliwa kuwa alikuwa kamishina wa mkoa kutokana na sare aliyovalia, na wengine wanaochukuliwa kuwa wakoloni kutokana na sini zao.

Wizi wa ardhi za umma na hata ardhi za watu binafsi ulianza wakati wa ukoloni, pale ambapo Waingereza walijinyakulia ardhi za watu binafsi hasa walioishi kwenye maeneo yenye hali nzuri ya anga ambayo ingenufaisha ukulima. Baada ya nchi kupata uhuru, inasemekana kuwa rais wa kwanza wa jamhuri ya Kenya, hakuwarudishia watu waliokuwa wamenyang’anywa ardhi zao, ilhali wajinyakuliwa vipande hivyo na kuwapa waliomuunga mkono. Baada ya rais wa kwanza kuaga, rais wa pili alipochukua hatamu, inasemekana kuwa alijinyakulia vipande vya ardhi katika sehemu mbalimbali

za nchi ya Kenya, na zingine akawatunuku viongozi wa serikali yake. Hivyo, kutokana na usawiri katika kibonzo hiki, mtafiti aligundua kuwa suala la wizi wa ardhi ya umma ni jambo lililoanza katika nyakati za ukoloni na bado linaonekana kuendelea hata katika uongozi wa Rais wa mwaka wa 2017. Gado anapoangazia suala la unyakuzi wa ardhi kama mvuke ulikuwa umefungiwa kwenye chupa iliyokuwa imeandikwa "*LAND GRABBING*" anaonyesha kuwa ni suala sugu linalokumba nchi ya Kenya. Kwa kawaida, mvuke unaotoa gesi ya rangi ya kijani kibichi ni gesi ya klorine na inachukulikuwa kuwa na harufu mbaya na mmemenyuko wa hali ya juu. Hivyo, Gado alikuwa anapitisha ujumbe kuwa Rais akijua waliohusika na unyakuzi wa ardhi ya umma, ni jambo ambalo litampa tumbo joto kwani washukiwa ni baba yake mzazi, naibu wake, marais watatu waliostaafu, viongozi wa madhehebu na wakoloni waliokuwa wamekwisha aga dunia. Kando na hayo, hali ya Gado kudokeza kuwa naibu rais pamoja na marais wastaafu ni wezi wa ardhi za umma si jambo ambalo hangeweza kuangazia kwa uwazi ikiwa alikuwa anachapisha kibonzo hiki kwenye magazeti. Hivyo, uhamiaji wa uchapishaji wa vibonzo vya kisiasa kutoka kwenye magazeti hadi kwenye mtandao, ulimpa Gado uwezo wa kusawiri masuala kwa ukali na bila kudhibitiwa.




***Kibonzo 20: K4UF. Funga Macho na Uombe. Kutoka (http://gadocartoons.com/close-eyes-pray/).***

Vilevile suala la ufisadi linajitokeza katika kibonzo 20 K4UF ambapo mtafiti alikumbana na mchoro ulioonyesha Rais akiwa amevalia taji la kifalme huku akiwa amebeba sanduku lililofungwa kwa kufuli. Kando ya Rais, Naibu Rais anaonekana

akiwa amevalia kilemba kwenye kichwa chake huku akiwa amebeba gunia linalochukuliwa kuwa limejaa pesa. Nyuma yao kuna mwanamke anayeonekana ni kana kwamba anaomba. Katika kibonzo kile Naibu Rais alionekana akimwambia mwanamke yule aendelee kufunga macho na kuomba. Kwenye upande wa kulia wa kibonzo kile kunaonekana kijibonzo kingine kidogo kikisema;

*And open them after we count five years*
*Na uyafumbuwe tukishahesabu miaka mitano*.

Katika kibonzo hiki msanii alitumia mchoro wa mwanamke kuwakilisha wananchi wa nchi ya Kenya. Kila wakati wa uchaguzi wananchi wa Kenya huungana kuomba wapate viongozi wazuri watakaowafanyia kazi na walete maendeleo na kila baada ya miaka mitano wanachagua viongozi wanaowaibia na wasiowafanyia kazi. Matukio katika kibonzo hiki yalionyesha bayana udhaifu wa viongozi wanaochaguliwa nchini Kenya, ambapo wananchi wanaomba wapate viongozi wazuri ilhali wanaendelea kuchagua viongozi wanaojua kwa hakika ni wafisadi. Kutokana na maelezo haya, Gado aliangazia ufisadi uliokuwa unaendelezwa na Rais na Naibu Rais wa nchi ya Kenya na ujinga wa wananchi wanaibiwa wakiwa wamefumba macho na wanagutuka baada ya miaka mitano. Kwa kifupi, msanii alikuwa anatashtiti Rais na Naibu Rais kwa kuwa wezi wa mali ya umma badala ya kuwa watunzaji wa mali ya umma. Kwa kawaida, Rais anapaswa kuwa mtu mwenye maadili na uadilifu wa hali ya juu, hivyo msanii anapotusawiri Rais na Naibu Rais ambao ni wezi, hili linakuwa ni jambo ambalo lina ukali katika usawiri wake.

### 4.2.5 Ukosefu wa Maadili

Maadili ni tabia nzuri au mienendo inayokubalika katika jamii fulani. Ni jambo la kawaida kwa watu wa jamii fulani kufuata tabia au mienendo inayoaminika na kukubalika kuwa nzuri. Katika kibonzo 8: $K_1$UWM msanii alimsawiri mkuu wa Benki Kuu ya Kenya akiwachagua mameneja wa kupokea pesa za benki kuu ya Kenya. Katika kibonzo kile mameneja wale wasawiriwa kama nguruwe, paka, tai na wengine wamesawiriwa kama wanaume vibonge ambao hatukuonyeshwa sura zao. Kwa msingi wa nadharia ya semiotiki kama ilifafanuliwa na Wamitila (2002), na hasa mhimili wa kiishara na kirejelezi, meneja mmoja akisawiriwa kama nguruwe, picha inayojitokeza katika akili ya mtafiti ni kuwa meneja yule ni mlafi, kutokana na imani kuwa nguruwe

ni mnyama mchafu anayekula chochote na ana sifa ya ulafi. Kando na hayo, taswira ya meneja mmoja akiwa amesawiriwa kama paka tunapata picha ya mtu mtukutu na msiri.

Kando na hayo, meneja aliyesawiriwa kama tai anachukuliwa kuwa na sifa ya kunyapanyapa kwenye mzigo akitafuta kitu cha kukula na kumaliza bila kusaza chochote. Kutokana na usawiri huu, mtafiti aligundua kuwa msanii alikuwa anadhihirisha udhaifu wa mameneja waliochaguliwa na Mkuu wa Benki Kuu ya Kenya. Kwa kawaida, mtu anapoteuliwa kama meneja wa benki inachukuliwa kuwa mtu yule ni mwaminifu, mwadilifu na mtu ambaye anaweza kutegemewa na anayeweza kuwajibika katika kazi yake. Hivyo, msanii anapotusawiria mameneja wa benki kuu wa Kenya kama watu walafi, wasiri, wenye tabia ya kunyapanyapa, hatuna budi ila kujiuliza ikiwa utajiri wa nchi ya Kenya uko kwenye mikono salama.


Zaidi ya hayo, kwenye upande ya kushoto wa kibonzo kile tunaonyeshwa jengo lililoporomoka na mle ndani mna mafuvu ya watu, magurudumu ya magari, gunia lilowekwa hela, kuna damu inayoonekana imetapakaa kwenye maeneo mbalimbali karibu na jengo lililoporomoka lenye maandishi;

*Moral Bank*

*Benki ya Maadili* ($K_1$UWW).

Kwa mujibu wa mhimili wa kiishara katika nadharia ya semiotiki, ishara ya damu, mafuvu ya watu huashiria kifo au mauaji ya watu. Kwa hivyo, msanii alikuwa anadokeza kuwa maadili ya wanaofanya kazi kwenye Benki kuu ya Kenya, yamezorota kiasi cha watu kuuliwa ili wizi wa hela uweze kufanyika katika benki ile. Usawiri wa hali ya benki kuu ya Kenya unaonyesha uozo ulioko kwenye taasisi ile. Benki kuu ya Kenya ni hifadhi ya utajiri wa nchi ya Kenya na hivyo kukichaguliwa mameneja wenye sifa za ulafi, usiri na kunyapanyapa, kuna uwezekano kuwa nchi ya Kenya inaweza kufilisika. Taswira hii inaendeleza maudhui ya ukosefu wa maadili miongoni mwa wafanyikazi wa serikali hasa wa Benki Kuu ya Kenya. Uangaziaji wa Benki kuu ya nchi ya Kenya kama jengo la maadili lililoporomoka ulinuia kuweka wazi ukosefu wa maadili miongoni mwa wafanyikazi wa nchi ya Kenya na pia kutashtiti tabia na mienendo yao. Katika nchi ya Kenya, watu wanaoajiriwa kama wafanyikazi wa serikali lazima watimize mahitaji ya kitengo cha sita cha katiba ya nchi ya Kenya kinachohitaji kila mfanyikazi awe mwadilifu, hana rekodi yoyote ya uhalifu, awe mtu wa kujitegemea kwa kulipa ushuru na mikopo yote aliyochukua. Kwa hivyo, inakuwa ni

kinaya kwa mameneja wanaopokea pesa kwa benki kuu ya nchi ya Kenya kuwa walafi, wasiri, na watu wa kunyapanyapa.




***Kibonzo 12: K₂UWM Kuadhimisha kipengele cha Sita. Kutoka (www.gadocartoons.com)***.

Zaidi ya hayo, katika kibonzo $K_2$UWM, mtafiti alikumbana na matukio yaliyoendeleza maudhui ya ukosefu wa maadili. Katika kibonzo hiki, mtafiti alituonyesha taswira ya Rais na Naibu Rais na walionekana kana kwamba walikuwa wakijisaidia kwenye kaburi lililoandikwa;

*Here Lies Chapter 6 Aka Integrity*

*Kaburini Mna Sura ya Sita ya Katiba ya Kenya Almaarufu Uadilifu*.

Naibu Rais anaonekana akimuuliza Rais;

*Remind Me Again…. Is This The 5th, 6th Or 7th Commemration…?!"*

*Nikumbushe Tena…. Je Huu Ni Ukumbusho Wa Tano, Sita Au Saba…?!*

Kwa kawaida katika jamii za Kiafrika, watu huheshimu na pia kuogopa mahali ambapo kuna makaburi. Katika jamii zingine ni mwiko kuelekezea kidole kwenye kaburi, hivyo msanii anapotusawiria Rais na Naibu Rais wakienda haja ndogo juu ya kaburi, anapitisha ujumbe kuwa viongozi hawa wawili wamefanya jambo ambalo si la kawaida na jambo ambalo ni mwiko katika jamii nyingi za kiafrika (Baloyi na Rabothata, 2014) Kando na hayo, msanii alikuwa anaonyesha hadhira yake jinsi Rais na Naibu Rais walivyokosea heshima katiba ya nchi ya Kenya na hasa jinsi walivyopuuza kipengele

kilichohusiana na uadilifu. Kitendo cha kwenda haja ndogo kwenye kaburi la kipengele cha sita cha katiba ya Kenya na hasa kinachotaka anayewania rais kuwa na uadilifu kinaonyesha kudharau na kutotilia maanani sheria iliyo ya kitengo cha juu zaidi katika nchi ya Kenya.

**RageAholics Anonymous**




***Kibonzo 7: $K_3$UWM Mkutano wa Kusaidia Kudhibiti Hasira. Kutoka (www.gadocartoons.com)***.

Kadhalika, msanii alisisitizia maudhui ya ukosefu wa maadili kwa kumsawiri Rais akiwa kwenye mkutano wa kudhibiti hasira kama inavyoonekana katika kibonzo 7: $K_3$UWM. Gado anatuonyesha Rais akiwa mbele ya watu wanaonekana kuwa kwenye mkutano na nyuma yake kuna kibango kilichoandikwa "*RAGEAHOLICS ANONYMOUS Kenyan Chapter 12 steps to ANGER MANAGEMENT*" kumaanisha kuwa huo ni mkutano wa watu wenye shida ya hasira na wako pale kujifunza jinsi ya kudhibiti hasira. Dhana ya *rageaholics anonymous Kenyan Chapter 12 steps to Anger Management*, imekopwa kutoka kwa mikutano ya watu ambao wameshindwa kudhibiti unywaji mvinyo na mikutano ile huitwa *Alcoholics Anonymous 12 steps to Alcohol Management*. Hivyo, Gado anapomsawiri Rais akihudhuria mikutano hii, anapitisha ujumbe kuwa, Rais wa nchi ya Kenya katika mwaka wa 2017, alikuwa na shida ya kudhibiti hasira na kulipaswa kuwa na mkakati wa kujaribu kumsaidia yeye pamoja na viongozi wengine waliochorwa kwenye kibonzo kile kama vile; aliyekuwa Gavana wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi, aliyekuwa Mwakilishi wa Wanawake Kaunti ya Nairobi na aliyekuwa Seneta wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi.

Viongozi hawa watatu wameunganishwa na Rais katika kibonzo $K_3$UWM kwa kuwa mnamo mwaka wa 2013, aliyekuwa Gavana wa Nairobi alimzaba kofi Mwakilishi wa Wanawake baada ya kutoelewana. Pamoja na hayo, aliyekuwa Seneta wa Nairobi wakati huo walikosana na Mwakilishi wa Wanawake katika mwaka wa 2013 baada ya uvumi kuenea kuwa wawili hao walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Katika Kibonzo hiki Rais anaonekana akijitambulisha na baadaye kufoka;

*Devils! Shetani* na *Shindwe!*

Usawiri huu wa Rais unaelezea matukio ya Machi 2017 ambapo Rais alimfokea na kumtusi Gavana wa Turkana wa wakati huo kuhusu mafuta yaliyokuwa yamepatikana kule Turkana. Msanii anatuonyesha ukosefu wa maadili upande wa viongozi ambao walichaguliwa kuongoza nchi. Katika utamaduni wa Kiafrika ni makosa kwa kiongozi au mtu mwenye cheo kutoa cheche za matusi hadharani hata kama kuna sababu ya kumfanya kukasirika. Kwa hivyo, msanii anapomsawiri Rais akitoa cheche za matusi hadharani, anatuonyesha udhaifu wake na ukiukaji wa maadili. Usawiri huo wa Rais ulinuia kutashtiti tabia yake ya kuonyesha hasira hadharani na pia kumkosoa Rais kwa tabia yake. Katika jamii za kiafrika, viongozi wa ngazi ya juu kama vile rais, huchukuliwa kuwa watu wenye maadili na heshima na hivyo si jambo la kawaida kwa msanii kama vile Gado, kujaribu kukosoa rais hadharani kwa kutumia vibonzo vyake. Hivyo basi, uhuru unaotokana na kuchapisha vibonzo vya kisiasa kwenye tovuti yake binafsi ambako hadhibitiwi na yeyote, kunampa uhuru wa kutashtiti na kukosoa Rais hadharani.

### 4.2.6 Upendeleo

Kwa kifupi upendeleo ni hali ya kupendelea ndugu au jamaa yako hasa katika nafasi za ajira. Katika Kibonzo 9: $K_1$UP tunaonyeshwa picha ya Rais akimfokea mwanamke aliyebeba mtoto mgongoni huku akiwa na uteo kichwani na kando yake kuna watoto wawili na mwanamme mmoja.

Same Forest Same Monkeys




***Kibonzo 9: $K_1$UP Msitu Mmoja, Tumbili wale wale. Kutoka*** (***<u>www.gadocartoons.com</u>***).

Katika picha ile Rais anaonekana akisema;

> *Yes, my sister and the DP's relatives have a right to government tenders like any other kenyan.*
>
> *Ndio, dadangu na jamaa za naibu wangu wana haki ya kupata zabuni za serikali kama mkenya yeyote yule*.

Kwenye sehemu ya chini ya $K_1$UP, msanii anatuonyesha kinara wa muungano wa NASA RO akiwa na mgombea mwenza mheshimiwa KM anaonekana akiwaambia wananchi;

> *My brother and my deputy's son have a right like any other Kenyan to be nominated for any position.*
>
> *Ndugu yangu pamoja na mtoto wa kiume wa naibu wangu wana haki ya kuteuliwa katika nyadhifa zozote zile kama wakenya wengine*.

Kibonzo hiki kinaelezea hali ilivyokuwa wakati jamaa za viongozi hao wanne walinufaika kutokana na zabuni za serikali pamoja na nyadhifa mbalimbali serikalini ilhali kulikuwa na wakenya wengine ambao walikuwa na uwezo wa kupata nafasi hizo. Suala hili linathibitisha upendeleo katika uongozi wa nchi ya Kenya ambapo wanasiasa wanatumia nyadhifa na mamlaka waliopewa na wananchi kwa manufaa yao wenyewe na watu wa familia zao. Kwa kawaida, jukumu la viongozi kuleta rasilimali za nchi pamoja kwa manufaa ya wananchi waliowachagua. Hivyo, msanii anapotuonyesha taswira ya viongozi waliokuwa kwenye ngazi ya Rais na Naibu Rais wakitumia

nyadhifa zao kujinufaisha wao wenyewe pamoja na jamaa zao, alikuwa anaibua suala la upendeleo na kuwatashtiti viongozi hawa kwa kutumia rasilimali na nafasi zilizoko nchini kwa manufaa ya jamaa zao. Huenda Gado aliangazia suala la upendeleo kwa minajili ya kuzindua umma kuhusu nia kuu ya Rais na Naibu wake pamoja na viongozi wa upinzani, kutumia mamlaka na nafsi zao kujifaidi.

### 4.2.7 Unafiki

Kamusi ya Karne ya Ishirini na moja inaelezea unafiki kama hali au tendo la kujifanya mkweli. Katika Kibonzo 18: $K_1$UN tunaonyeshwa taswira ya Naibu Rais na aliyekuwa Gavana wa pili wa Kaunti wa Kirinyaga wakitembea pamoja wakielekea kwenye meza iliyowekelewa Bibilia na kwa upande wa kulia kuna umati wa watu wanaonekana kuwa na sura zenye mshangao. Taswira ile inawakilisha hafla ya kuapishwa kwa viongozi.

**Join the Catwalk…! #DP#Waiguru**




***Kibonzo 18: $K_1$UN Jiunge na Tamasha la Maonyesho ya Urembo...! #Dp #Waiguru (Kutoka www.gadocartoons.com).***

Katika kibonzo kile Naibu Rais amechorwa akiwa amevalia kilemba na aliyekuwa gavana wa pili wa Kaunti ya Kirinyaga amesawiriwa akiwa na nywele ndefu zilizoandikwa NYS. Katika kibonzo hiki Naibu Rais anaonekana akimwambia gavana;

*Nice Hair Governor*

*Nywele Nzuri Gavana*, naye gavana anamjibu Naibu Rais,

*Nice Turban Deputy President*!

*Kilemba Kizuri Naibu Wa Rais!*

Msanii alitumia mazungumzo baina ya Naibu Rais na aliyekuwa gavana wa pili wa Kaunti ya Kirinyaga kuendeleza maudhui ya unafiki katika uongozi wa nchi ya Kenya. Matukio yaliyochangia msanii kuchora kibonzo hiki yalitokea kabla ya uchaguzi wa Agosti 8 2017, ambapo Naibu Rais na gavana walikuwa hawapatani. Gavana alikuwa anakashifiwa kwa wizi na uporaji wa mali ya umma katika taasisi ya mafundisho ya vijana ya NYS na Naibu Rais alirekodiwa na vyombo vya habari akidai kuwa kazi ya gavana ilikuwa kutembea kana kwamba alikuwa kwenye maonyesho ya urembo badala ya kuelezea kamati ya uchunguzi jinsi hela za NYS zilivyoibiwa. (KTN, 2016)

Kwa upande mwingine Naibu Rais kwa muda mrefu alikuwa akikashifiwa kwa wizi wa ardhi za umma na hivyo, msanii anapomsawiri kama mtu muungwana na mtu anayefuata maadili ya dini, kutokana na kumsawiri akiwa na kilemba, anamkejeli Naibu Rais. Kwa kifupi, msanii alikuwa anasawiri hali ya Naibu Rais kumkashifu aliyekuwa gavana wa pili wa Kirinyaga kwa tuhuma za kuhusiana na sakata ya NYS naye gavana alikuwa akimkashifu Naibu Rais kwa tuhuma za ufisadi na wizi wa mashamba ya umma.

Msanii anapowasawiri wawili hawa wakielekea kwenye meza ya kukula kiapo pamoja wakitabasamu na kubadilishana sifa za uzuri, alikuwa anapitisha ujumbe kuwa yote yanaonekana kusahaulika baada ya wawili hawa kunyakua viti walivyokuwa wakigombea na wakaweza kuwa serikalini kupitia chama cha *Jubilee*. Msanii anapotuonyesha taswira ya viongozi wawili waliokuwa na kashifa za ufisadi na wizi wa mali ya umma wakielekea kwenye mzee ya kuapishwa, wakiwa tayari kuapa kuwa watawajibika na kufanya kazi walioteuliwa kufanya kwa uaminifu na uadilifu ni jambo la kushangaza na linalozua kinaya. Ikiwa viongozi hawa wawili walishindwa kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu katika ofisi walizokuwa wameshikilia awali, basi ni jambo lipi lingewafanya wawe waadilifu katika nyadhifa walikuwa wamechaguliwa katika mwaka wa 2017? Kibonzo $K_1$UN kinaibua maudhui ya unafiki katika viongozi wanaochaguliwa nchini Kenya kwa kutashtiti tabia zao za kupuuza sheria na katiba ya nchi ya Kenya

#### 4.2.8 Hitimisho

Kutokana na maelezo katika sehemu hii, mtafiti aligundua kuwa maudhui yaliyojitokeza katika sehemu hii yalihususiana na uongozi wa serikali ya Rais na Naibu Rais na maovu yalikuwa yakitendeka katika kipindi cha mwaka wa 2013 hadi 2017 na mengine yanaonekana yakirudi nyuma hadi enzi za ukoloni**.** Usawiri wa msanii ulinuia kukashifu na kutashtiti serikali na uongozi wa Rais na Naibu Rais pamoja na viongozi wa upinzani wa wakati huo. Maudhui yaliyojitokeza katika uchanganuzi wa vibonzo vya kisiasa vya Gado yalinuia kutashtiti, kukejeli na kuweka wazi uovu uliokuwa ukitendeka nchini Kenya katika kipindi cha 2017. Isitoshe, upambanuzi wa maudhui haya ulidhihirisha uhuru na ukali mwingi katika usawiri wa viongozi na taasisi za uongozi. Kwa mfano, katika sehemu hii, tuliona Rais na Naibu Rais wakisawiriwa kama wafisadi, watu wasiozingatia maadili ya jamii zao, viongozi wanaowahujumu wafanyikazi wao na watu wanaoendeleza mapendeleo. Kwa kawaida, usawiri kama huu huwezi kufanyika katika vibonzo vinavyochapishwa kwenye magazeti kwa sababu ya kudhibitiwa na mashirika ya vyombo vya habari au woga wa kufunguliwa mashtaka kwa tuhuma za kuharibia watu jina.


### 4.3 Mikakati ya Kitashtiti

Kama mtafiti alivyoeleza awali, ni muhali kwa tashtiti kufaulu kivyake na aghalabu hutegemea mbinu zingine za lugha ili iweze kutambulika. Stinson (2019), alidai kuwa tashtiti husawiri "ushambulizi wa ainasafu" ambapo mara nyingi huwa inafaulu kwa kujifanya kuwa kitu kingine. Kwa kifupi, tunaweza kusema kuwa tashtiti ni kimelea kinachotumia tanzu, mitindo mbalimbali ya lugha na aina zote za mawasiliano ili iweze kufaulu. Katika sehemu hii, mtafiti alitambua na kuainisha mitindo mbalimbali ya lugha pamoja na ishara zilizotumika na msanii Gado kwa minajili ya kuvifanya vibonzo vilivyoteuliwa kuwa vya kitashiti.

#### 4.3.1 UKaragosi


Das (2019) anaeleza kuwa ukaragosi ni mbinu ya mawasiliano ya kuonekana ambayo huwasilisha ujumbe kwa njia yenye kupiga chuku kwa kutumia michoro au picha. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia neno karagosi kumaanisha usawiri wa mtu uliopigwa chuku na hasa sifa bainifu za mhusika aliyesawiriwa. Kutokana na neno karagosi, mtafiti aliunda neno ukaragosi kumaanisha mbinu yenyewe ya usawiri wa sifa bainifu za mtu fulani zilizopigwa chuku. Kutokana na uelewa huu, mtafiti aligundua kuwa,

msanii alitumia mbinu ya ukaragosi alipowachora Rais, Naibu Rais, vinara wa NASA RO, MM na MW. Kwa mfano; katika vibonzo $K_1$UWW, $K_1$UO, $K_2$UWW, $K_3$UWM, $K_5$UO, $K_2$UO, $K_6$UO, $K_4$UF, msanii alipiga chuku mwonekano wa sura wa Rais na Naibu Rais. Katika vibonzo hivi, msanii aliwasawiri Rais na Naibu Rais wakiwa na vichwa vikubwa, macho makubwa au hata midomo mikubwa kuliko kawaida kwa minajili ya kuzua ucheshi na kuwakejeli. Kwa kupiga chuku mwonekano wao wa uso, msanii alilenga kuonyesha umma kuwa viongozi hawa ni watu wa kawaida tu na wanaweza kuchambuliwa na kutashtitiwa kama watu wengi.




***Kibonzo 15: $K_4$UO kinyang'anyiro cha ugavana katika Kaunti ya Nairobi. Kutoka (http://gadocartoons.com/nairobi-gubernotorious-race/).***

Zaidi ya hayo, mbinu hii ya ukaragosi pia inajitokeza katika kibonzo $K_4$UO ambapo wagombea kiti cha Ugavana cha Kaunti ya Nairobi walisawiriwa kwa njia iliyopigwa chuku. Kwa mfano; aliyekuwa gavana wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi alichorwa akiwa na pua refu, Mheshimiwa PK akiwa na uso mpana kuliko kawaida na Mheshimiwa Miguna akiwa na mdomo uliofanana na baragumu. Usawiri huu ulilenga kuzua ucheshi kwa kupiga chuku sifa hasi za kila kiongozi. Tendo la kumsawiri aliyekuwa gavana wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi akiwa na pua kubwa ni njia moja ya kumkejeli na kumuita mwongo. Vilevile, PK kusawiriwa akiwa na uso mpana na masikio makubwa na mkia ni njia moja ya kutashtiti tu mwonekano wake wa uso. Zaidi ya hayo, Gado alipomsawiri Miguna Miguna akiwa na mdomo unaofanana na baragumu, alikuwa anapitisha ujumbe kuwa mheshimiwa huyo ana kelele nyingi na kazi yake ni kuongea tu na kupiga kelele. Kutokana na maelezo haya, ni bayana kuwa msanii alitumia mkakati wa ukaragosi kama mbinu ya tashtiti sifa hasi za kila kiongozi.




***Kibonzo 2: $K_1$UKS NASA na Kampeni Zao: Kutoka (http://gadocartoons.com/nasa-and-their-campaign/).***

Kando na hayo, katika kibonzo $K_1$UKS, vinara wa muungano wa NASA, Waheshimiwa RO, MM na MW wamesawiriwa wakiwa na vichwa vikubwa kuliko kawaida. Usawiri huu ulilenga kuwakejeli viongozi hawa na kuwachora kwa njia iliyozua ucheshi kwa watu waliotazama vibonzo vile. Hivyo, ni dhahiri kuwa msanii Gado alitumia mbinu ya ukaragosi sio tu kuzua ucheshi bali pia kuwatashtiti na kukejeli viongozi mbalimbali wa Kenya. Mbinu ya kupiga chuku mwonekano wa viongozi hawa, ulilenga kuonyesha kuwa viongozi hawa ni watu wa kawaida waliokuwa na udhaifu wao na hivyo hawakuwa watu wakamilifu kitabia na kimienendo, bado walihitaji kurekebishwa.

### 4.3.2 Sitiara

Wamitila (2003) alieleza sitiara kama mbinu inayotumika kuhamisha maana. Maina (2012) anafafanua mawazo ya Wamitila kwa kuelezea kuwa sitiara ni mbinu ya kisanaa inayotumia kitu kimoja kurejelea kitu kingine. Kwa kifupi, sitiara ni mbinu ya kutumia mfanano uliopo baina ya vitu kwa minajili ya kutumia dhana moja kurejelea dhana nyingine na hapa ndipo uhamishaji wa maana hujitokeza. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia dhana ya sitiara kumaanisha ulinganisho wa vitu viwili ambapo hujatumia maneno lakini ni wa "kuonekana" kupitia michoro au picha.

Kwa mfano, sitiara inajitokeza katika kibonzo $K_1$UKS ambapo nyadhifa za serikali zimesawiriwa kama kuku anayetoa harufu ya kuvutia na mtafiti anapata haya kutoka na mvuke unaoonekana ukitoka kwenye kuku yule aliyepikwa. Kwa kawaida kuku

aliyepikwa akaivaa hutoa harufu nzuri inayovutia watu. Hivyo, msanii anaposawiri ahadi za kupata nyadhifa mbalimbali serikalini kwa watu watakaojiunga na muungano wa NASA, anamaanisha kuwa nyadhifa zile ni jambo la kuvutia kwa wanasiasa mbalimbali. Kando na hayo, katika kibonzo kile, nyadhifa za serikali ziko kwenye mtego ulioandikwa NASA na mtego ule una mnyororo uliofungiliwa kwenye mlingoti ulio na bendera iliyoandikwa "*FLAG BEARER*".

Kwanza kabisa, kazi ya mtego ni kunasa windo au mnyama anayeharibu vitu. Hivyo msanii anapochora mtego na kisha kuupa jina NASA, anapitisha ujumbe kuwa kujiunga na muungano wa NASA ni kama kuingia kwenye mtego utakao kunasa. Kwa kifupi, msanii anamaanisha kuwa ahadi ile ya nyadhifa mbalimbali za serikali ni mtego tu wa kuwanasa wanasiasa mbalimbali. Kando na hayo, taswira ya vinara wa NASA, MM, MW na KM wakiwa wamekwea mlingoti ulioshikiliwa na RO na wenye mnyororo uliofungiliwa kwenye mtego ina maana kuwa vinara wa NASA tayari wako kwenye mtego wa NASA kwa kuwa hata wao wenyewe hawajakubaliana ni nani atakayepeperusha bendera ya muungano wao katika kinyang'anyiro cha urais cha mwaka wa 2017.




***Kibonzo 3: $K_1$UO, Jubilee italeta Maziwa na Asali. Kutoka (http://gadocartoons.com/Jubilee-will-bring-milk-honey/).***

Katika Kibonzo 3, $K_1$UO msanii anatumia mifupa ya wanyama na binadamu kuonyesha kuwa binadamu na wanyama wamekwisha kufa kutokana na ukosefu wa maji. Mifupa ya wanyama na binadamu inaashiria kufa kwa watu. Pamoja na hayo, katika mchoro

ule kuna makopo yaliyowekwa ni kana kwamba yako tayari kuwekwa kitu. Kwa kawaida, sehemu za nchi ya Kenya ambazo hazina maji, watu huteka maji na kuyahifadhi kwenye mitungi au makopo makubwa. Hivyo, msanii anapotuonyesha mandhari yaliyo na makopo ni ishara kuwa wananchi walikuwa wanangoja serikali iwaletee maji, lakini kwa kuwa serikali ile haikuwa na mipango ya kuwafaidi wananchi na miundo msingi, wananchi pamoja na mifugo yao walikwisha fariki wakingoja serikali iwaletee maji. Hivyo, msanii ametumia ishara ya mafuvu na mifupa ya wanyama kama tafsiri ya kifo cha matumani ya wananchi. Kutokana na matukio yaliyosawiriwa katika Kibonzo 3, $K_1$UO, Gado alikuwa anawatashtiti Rais na Naibu Rais kwa kutojali maslahi ya wananchi. Wananchi walihitaji maji na chakula, ilhali serikali ya Rais na Naibu Rais walitaka kura za wananchi kwa ahadi kuwa wataleta maziwa na asali. Kwa kawaida, kiongozi mzuri ni yule anayeelewa mahitaji ya wananchi waliomchagua na sio kuelewa tu, bali anapanga mikakati ya kutimiza mahitaji ya wananchi. Hivyo msanii anapotuonyesha taswira ya viongozi wasioelewa mahitaji ya wananchi wao, tunajiuliza ikiwa Rais na Naibu Rais kwa kweli ni viongozi wazuri na wanaofaa kwa wananchi wa Kenya.

**OLOO JOINS NASA**




***Kibonzo 4: $K_2$UKS, Oloo ajiunga na NASA. Kutoka (http://gadocartoons.com/oloo-joins-nasa/).***

Zaidi ya hayo, katika kibonzo 4, $K_2$UKS msanii anatuonyesha aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama cha TNA, na aliyetambulishwa kwetu kama Oloo, akiwa ameshikilia mkia wa punda aliyeandikwa NASA na inaonekana ni kana kwamba punda yule alikuwa akimtolea kinyesi Oloo. Pamoja na hayo, Oloo anaonekana akiwaeleza vinara wa NASA kuwa atawasaidia kuiba kura za uchaguzi huo kama alivyosaidia chama cha Jubilee. Kutokana na matukio yaliyosawiriwa katika kibonzo hiki, ni dhahiri kuwa msanii anapitisha ujumbe kuwa maneno yanayosemwa na Oloo sio muhimu au yanachukuliwa kuwa si ya maana. Taswira ya Oloo kushikilia mkia wa punda anayemtolea kinyesi, ni ishara kuwa tendo la Oloo kujiuzulu kama katibu mkuu wa muungano wa Jubilee na kuhamia muungano wa NASA ni jambo ambalo halina maana au manufaa yoyote kwa muungano wa NASA. Katika $K_2$UKS msanii analinganisha tendo la Oloo kuhamia muungano wa NASA na kinyesi cha punda ambacho hakina maana au manufaa yoyote. Isitoshe, Gado anaposawiri muungano wa NASA kama punda, uangaziaji huu ulitokana na msemo uliokuwa maarufu katika kipindi cha kampeni za mwaka wa 2017, kuwa mbio za kinyang'anyiro cha urais zilikuwa kati ya punda na farasi, ambapo chama cha Jubilee kiliashiriwa kama farasi. Katika uhalisia huu, hakuna siku punda angeweza kumshida farasi katika mbio. Hivyo, kitendo cha Oloo kujaribu kuhamia muungano wa NASA kwa ahadi kuwa atawasaidia kuiba kura, hakina maana kama kinyesi cha punda.

Katika kibonzo 5, $K_2$UWW mbinu ya sitiara inajitokeza pale ambapo msanii anawasawiri madaktari kama mwanamke aliye kwenye ndoa ya unyanyasaji. Ulinganisho huu wa madaktari na wanawake ulinuia kuleta dhana ya unyonge. Kwa muda mrefu katika utamaduni wa Kiafrika, mwanamke amechukuliwa kuwa kiumbe dhaifu na hali hii imesababisha hali ya kunyanyaswa na kukandamizwa. Hivyo, msanii anapowasawiri madaktari kama mwanamke anapitisha ujumbe kuwa, kwa wakati ule madaktari ni wanyonge na hawana njia ya kujikomboa kutoka kwa mikono ya unyanyasaji ya serikali ya Kenya.


Vilevile, msanii anapoonyesha mmoja wa wananchi katika $K_1$UWW akisema;

> *This Has Been an Abusive Marriage*
>
> *Hii Imekuwa Ndoa Ya Unyanyasaji*

analinganisha uhusiano wa madaktari na serikali na taasisi ya ndoa yenye unyanyasaji. Ulinganisho huu unaonekana kuhamisha maana ya unyanyasaji kutoka kwa uhusiano

wa madaktari na serikali hadi kwa uhusiano wa mwanamke anayenyanyaswa na mumewe kwenye taasisi ya ndoa ambayo kwa kawaida inafaa kuwa na mapenzi, furaha na kusaidiana. Hivyo, ishara zilizotumika katika kibonzo hiki, ziliunda taswira ya rais anayewanyanyasa wafanyikazi wake kwa kutumia mkakati wa sitiara akiwa na lengo la kutashtiti tabia ya Rais na Naibu Rais.

**Moral Bank Collapse**




***Kibonzo 8: $K_1$UWM, Kusambaratika kwa Benki ya Maadili. Kutoka (http://gadocartoons.com/morals-bank-collapse/).***


Katika Kibonzo 8, $K_1$UWM sitiara inajitokeza pale ambapo mameneja wa Benki Kuu ya Kenya wamesawiriwa wakiwa na nyuso za nguruwe, fisi na tai. Katika kibonzo hiki, ulinganisho unaojitokeza ni wa moja kwa moja na ni wa kuonekana. Msanii anaposawiri meneja mmoja akiwa na kichwa cha nguruwe ujumbe unaopitishwa ni kuwa meneja yule ni mlafi, kutokana na imani kuwa nguruwe ni mlafi. Pili, usawiri wa meneja mwingine kama tai una maana kuwa meneja yule ana sifa za kunyapanyapa, hivyo mtafiti alichukulia kuwa mameneja wale walikuwa na sifa za kunyapanyapa wakitafuta mali ya umma na kujinyakulia. Pamoja na hayo, usawiri wa meneja mmoja kama fisi ulithibitisha kuwa baadhi ya mameneja wa benki kuu walikuwa walafi na haini.

Kando na hayo, kuanguka kwa jengo lililokuwa na maandishi "*Moral Bank*" kunaashiria ukosefu wa maadili miongoni mwa wafanyikazi wa Benki kuu ya nchi ya Kenya. Msanii anapodokeza kuwa mameneja waliochaguliwa kuwa ni walafi, wahaini na watu wa kunyapanyapa mali ya umma ili kujinufaisha, anaashiria ukosefu wa maadili miongoni mwa mameneja waliochaguliwa. Vilevile, katika kibonzo hiki msanii

anatuonyesha taswira ya jumba lililoporomoka na mle ndani mnaonekana miguu ya watu, mafuvu na mifupa ya binadamu, chembechembe za damu, karatasi zilizotapaka, mifereji iliyotoboka na magunia ya pesa. Usawiri wa mafuvu, damu na mifupa ya watu, kunaashiria kifo au kufa kwa watu na uozo na kuzorota kwa maadili. Kutokana na udokezo wa msanii, inaweza kusemekana kuwa maovu ambayo yalikuwa yakitendeka katika Benki kuu ya nchi ya Kenya, huenda yalisababisha vifo vya watu kwa minajili ya kuficha maovu na uozo uliokuwa ukiendelea katika taasisi ile. Yamkini msanii alikuwa akisema kwa uwazi kuwa mameneja walioteuliwa kupokea pesa katika Benki Kuu ya Nchi ya Kenya ni wezi, watu wa walafi na watu ambao wanaweza hata kuua watu kwa minajili ya kuficha maovu yao.

Kwa msingi wa nadharia ya semiotiki, mhimili wa urejelezi, miaka iliyopita, katika nchi ya Kenya, Mameneja waliofanya kazi katika benki kuu ya nchi ya Kenya, walihusika na sakata ya "*Goldenberg",* iliyohusu uuzaji wa dhahabu katika nchi za nje ya Kenya. Sakata hii, ilihusisha viongozi pamoja na mameneja wa benki kuu ya nchi ya Kenya. Sakata hii ilipojulikana, kuna watu waliopotoze maisha yao kutokana na watu kutaka kuficha yaliyotokea. (Grynberg & Singogo, 2021). Huenda msanii, alikuwa anarejelea kisa hiki aliposawiri kuporomoka kwa maadili katika Benki Kuu ya nchi ya Kenya.

**DEVOLUTION AT THE ANIMAL FARM**




***Kibonzo 11: K$_3$UO Ugatuzi katika Shamba la Wanyama. Kutoka (http://gadocartoons.com/devolution-animal-farm/)***

Licha ya hayo, dhana ya kuhamisha maana pia inajitokeza katika kibonzo 11 K$_3$UO ambapo ofisi mbalimbali za uongozi zimesawiriwa kama wanyama. Kwa mfano, rais

na mbunge wamesawiriwa kama nguruwe kumaanisha kuwa wanaoshikilia ofisi zile wana sifa za ulafi. Hali ya msanii kusawiri ofisi hizi mbili kama nguruwe inatokana na hali ya wanaoshikilia ofisi hizi kuwa na tabia ya kutotosheka na mishahara na marupurupu wanayolipwa na kuiba mali ya umma. Isitoshe, katika kibonzo hiki tunaona seneta akiwa amesawiriwa kama tai, kumaanisha wanaoshikilia ofisi hizi wana sifa za kunyapanyapa kwenye mizoga. Msanii anaposawiri seneta kama tai anamaanisha kuwa wanaoshikilia ofisi zile wana tabia ya kuchakura mali ya umma na kuitumia kwa manufaa yao bila kubakishia wananchi chochote. Kwa hakika, msanii anaposawiri rais, maseneta wa nchi ya Kenya kama watu walafi na wafisadi, anatashtiti viongozi hawa na kudokeza kuwa viongozi hawa hawapaswi kuwa viongozi kwani matendo yao hayaandamani na sifa za kiongozi bora.

Vilevile, ofisi ya Mwakilishi wa wanawake bungeni imesawiriwa kama paka kumaanisha kuwa wanaoshikilia ofisi zile ni wasiri, watukutu na wako pale kupendeza tu. Wakati mwingi katika jamii nyingi za nchi ya Kenya paka hufugwa kwa minajili ya kufukuza panya na kumliwaza mfugaji wake. Kutokana na uelewa huu, tunaweza ng'amua kuwa msanii alitaka kumaanisha kuwa wanaoshikilia ofisi za wawakilishi wa wanawake wako pale kuliwaza na kufurahisha waliowachagua. Na hivyo, kutokana na usawiri wa msanii, anapitisha ujumbe kuwa haoni haja ya ofisi ya Mwakilishi wa wanawake bungeni kutokana na ukweli kuwa si kila boma inahitaji paka wakuwaliza wanaoishi pale ili iwe boma kamili. Zaidi ya hayo, ofisi ya ugavana imesawiriwa kama fisi kumaanisha kuwa wanaoshikilia ofisi zile wana sifa za ulafi na kunyapanyapa. Tukiangalia hali ilivyokuwa kutoka mwaka wa 2013 serikali za kaunti zilipoanzishwa, asilimia kubwa ya magavana waliochaguliwa katika kipindi hicho walikuwa na kesi za ufisadi na utumizi mbaya wa mali ya umma.

Hivyo, msanii anapowasawiri magavana kama fisi anajaribu kueleza umma kuwa magavana ni walafi na wana sifa ya kunyapanyapa. Pamoja na hayo, katika kibonzo $K_3UO$, msanii amesawiri wawakilishi wa wadi kama panya. Kwa kawaida panya ana sifa ya kuguguna na kuwa mchafu. Kutokana na uelewa huu, Gado alikuwa anamaanisha kuwa wawakilishi wa wadi huguguna mali ya umma iliyobaki katika kiwango cha wadi, na kuwa kazi yake ni kusumbua tu. Kwa kawaida, kuguguna kwa panya hutoa sauti na kelele za kukera. Kwa hakika hali hii, ilijitokeza katika kipindi cha mwaka wa 2013 hadi 2017, ambapo wawakilishi wa wadi nyingi nchini Kenya

waliwasumbua magavana kwa kutishia kuwa watawang'atua mamlakani, ikiwa hawatatimiza matakwa yao. Kutokana na usawiri wa ofisi ya mwakilishi wa wadi, huenda Gado alikuwa akipitisha ujumbe kuwa wanaoshikilia nyadhifa hizi ni watu wasumbufu tu wasiokuwa na kazi yoyote muhimu katika uongozi ila vitisho na kelele nyingi.

Kando na hayo, msanii amekipa kibonzo hiki anwani ya "*Devolution at the Animal Farm"* kama ulinganisho na riwaya wa George Orwell ya Shamba la Wanyama, ambayo huangazia ukosefu wa usawa. Katika riwaya ile ya George Orwell, mnyama aliyewaongoza wanyama wengine na baadaye kuwakandamiza wanyama wengine ni nguruwe. Kutokana na uelewa huo, inaweza chukuliwa kuwa msanii alilinganisha uongozi wa aliyekuwa rais na waliokuwa magavana katika nchi ya Kenya na uongozi wa nguruwe katika riwaya ile ya George Orwell. Zaidi ya hayo, katika riwaya ya Shamba la Wanyama, kulikuwa na sheria iliyosema kuwa mnyama yeyote aliyetumia miguu minne kutembea au mnyama yeyote aliyepaa ni rafiki wa uongozi wa nguruwe. Kwa msingi huo, wanyama waliosawiriwa na msanii hutembea kwa miguu minne na tai hupaa, hivyo msanii huenda alikuwa anadokeza kuwa wanaoshikilia ofisi zilizosawiriwa katika kibonzo kile ni marafiki wa uongozi wa Rais na hivyo wanakubaliana na uongozi wa kuwakandamiza wanyama wanaotembea kwa miguu miwili ambao katika hali hii ni wananchi wa Kenya. Kwa kifupi, msanii alitumia anwani ya kibonzo $K_3UO$ kama sitiara ya kuhalalisha ukandamizaji wa wananchi wa Kenya ambao ni wanyama wanaotembea kwa miguu miwili.

Katika Kibonzo 15 $K_4UO$, wagombeaji wa kiti cha Ugavana cha Kaunti ya Nairobi wamesawiriwa kwa njia ya kisitiara. Kwa mfano, aliyekuwa gavana wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi amesawiriwa akiwa na pua refu kuliko kawaida. Kwa kawaida, inachukuliwa kuwa mtu mwongo husemekana kuwa ana pua refu ama husawiriwa akiwa na pua lililo refu kuliko kawaida. Wazo hili lilitokana na riwaya ya watoto; "*Adventures of Pinocchio*" iliyochapishwa nchini Italia na Carlo Collodi katika mwaka wa 2005. Kazi ile ya kisanaa ilihusu kikaragosi aliyekuwa amechongwa kwa kutumia ubao lakini alikuwa na ndoto ya kuwa mvulana halisi aliye hai. Hatimaye, ndoto yake ilitimia na akawa hai. Jambo la kushangaza ni kuwa kila aliponena uongo pua lake lilirefuka. Kutokana na hadithi ile ya Pinocchio, watu walianza kuhusisha mtu mwongo na pua refu. Hivyo, usawiri huo wa aliyekuwa gavana wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi


ulilenga kulinganisha tabia yake na ya Pinocchio aliyekuwa mwongo kwa minajili ya kuibua tashtiti.

Pili, msanii alimsawiri aliyekuwa Seneta wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi kama mtoto aliyevalia koti la suti na badala ya suruali ndefu amevalia kiwinda kinachoonekana kuwa na kinyesi kutokana na nzi wanaoonekana wakimfuata. Kando na hayo, Seneta wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi, amesawiriwa akiwa amesimama kwenye maji na mkononi ameshika chupa ya mvinyo na bunda la noti. Gado anapomsawiri seneta huyo akiwa na sigara mdomoni, mvinyo na pesa mkononi ina maana kuwa yenye ni mtu mzima mwenye hadhi na utajiri, lakini anapochorwa akiwa na kiwinda chenye kinyesi, msanii anatujuza kuwa bado kiongozi huyu ana utoto au bado hajakomaa kiwango cha kuongoza wananchi. Kwa kawaida, kiwinda hufungwa watoto wadogo na hivyo msanii anapomsawiri aliyekuwa seneta wa Kaunti ya Nairobi akiwa na kiwinda anapitisha ujumbe ingawaje kiongozi yule ni mtu mzima mwenye hadhi na utajiri bado ana utoto na hivyo hafai kuwa kiongozi. Kwa kawaida, huwa inachukuliwa ni matusi kuita mtu mzima mtoto na si jambo linaloweza kutamkwa hadharani hasa mtu anapozungumzia kiongozi. Hivyo, mawazo ya Eko (2007), kuhusiana na kuongezeka kwa uhuru na ukali katika usawiri wa masuala katika vibonzo vinavyochapishwa kwenye mtandao unajitokeza. Hali ya msanii kumsawiri aliyekuwa seneta wa kwanza wa kaunti ya Nairobi kama mtoto mdogo aliyefungwa kiwinda, inadhihirisha ukali wa kumuita kiongozi yule mtoto.

Zaidi ya hayo, mgombeaji wa tatu aliyetambulishwa kama PK amechorwa akiwa na masikio makubwa, mkia na taswira yake inafanana na tumbiri. Msanii alilinganisha kiongozi huyu na tumbiri na anahusisha tabia ya PK na msemo wa Kiingereza "*monkey business*" kumaanisha mtu mwongo, mtukutu na mwenye udanganyifu. Usawiri huu wa PK unatokana na tabia yake ya kutokuwa na msimamo katika siasa. Katika maisha yake ya kisiasa PK alikuwa amewania viti mbalimbali vya uongozi katika vitengo tofauti tofuati na maeneo tofauti tofauti. Kwanza aliwania kiti cha ubunge cha eneo la ubunge la Gatanga, lililo katika Kaunti ya Murang'a nchini Kenya. Kisha baadaye, akawania kiti cha Urais cha nchi ya Kenya na hatimaye kiti cha Ugavana cha Kaunti ya Nairobi, inaweza kuchukuliwa ana tabia ya kuruka ruka kutoka eneo moja hadi lingine jinsi tumbiri anavyoruka ruka kutoka mti mmoja hadi mwingine. Kutokana na usawiri huu, msanii alikuwa alilinganisha tabia ya PK na ya tumbiri anayetapatapa na kuruka

ruka kutoka mti mmoja hadi mwingine, na nia kuu ya ulinganisho huu ilikuwa kumtashtiti kiongozi huyu kwa minajili ya kumsababisha abadili tabia zake.

Pamoja na hayo, msanii alimsawiriwi mgombeaji wa nne aliyetambulishwa kama Miguna akiwa na mdomo uliofanana na baragumu. Kwa kawaida, baragumu hutumiwa kupaza sauti. Hivyo mtafiti alichukulia kuwa usawiri wa Miguna akiwa na mdomo baragumu ulimaansisha kuwa kiongozi huyu sio msiri ni mtu wa kutangaza tangaza mambo na ana kelele nyingi. Hivyo basi, usawiri wa wagombeaji wa kiti cha Ugavana cha Kaunti ya Nairobi ulilenga kutashtiti tabia hasi za viongozi hawa kwa kutumia mbinu ya sitiara ambapo viongozi hawa walilinganishwa na wanyama na vitu mbalimbali.




***Kibonzo 16: K$_5$UO Kura za Waliowengi dhidi ya Kura za waliteuliwa. Kutoka (www.gadocartoon.com).***

Kando na hayo, mbinu ya sitiara inajitokeza katika kibonzo 16, K$_5$UO ambapo Rais na Kinara wa muungano wa NASA, RO wamesawiriwa wakiwa uchi. Katika kibonzo kile, RO amevalia gauni la zambarua ambapo linamuacha uchi sehemu ya mbele ya mwili wake. Vilevile, upande wa chini wa kibonzo hiki Rais amechorwa akiwa amevalia gauni la rangi nyekundu lilomuacha uchi sehemu ya mbele ya mwili wake. Usawiri huu wa msanii uliashiria udhaifu wa viongozi hawa wawili. Kwa msingi wa mihimili ya kiishara na kirejelezi kama ilivyofafanuliwa na Wamitila (2002), si jambo la kawaida kwa mtu kutembea akionyesha utupu wake, na hasa utupu wake wa mbele. Uchi wa mtu huwa jambo la siri, hivyo msanii anapotusawiria Rais wa nchi ya Kenya pamoja na mpinzani wake RO wakiwa uchi, anatuonyesha wazi udhaifu wao na usiri wao ukiwa

wazi. Ndiposa anatumia tovuti yake ya kibinafsi kuchapisha kibonzo hiki kwa kuwa hakiwezi kuchapishwa kwenye magazeti au majaribu kutokana na udhibiti ulipo katika vyombo vya habari kama vile magazeti, majarida au televisheni.

Kando na hayo, katika Kibonzo 16, $K_5$UO tunaona taswira ya wananchi wakiwa wameshikilia gauni la RO, ambaye ni kinara wa muungano wa NASA, huku wakimfuata nyuma na katika sehemu ya juu ya kibonzo kile kuna anwani "*Popular Vote*". Kwa upande wa chini ya kibonzo kile tunaona wanajeshi wakiwa wameshikilia gauni la Rais na sehemu ile ina anwani "*Electoral college*". Waller (2021), anafafanua dhana za "P*opular Vote*" na "*Electoral College"* hutumika katika uchaguzi Marekani, ambapo *Popular Vote* hutumika kumaanisha pale ambapo wananchi wote kwa kujumla hupigia kura viongozi watakaochukua hatamu za uongozi kule Marekani. Kwa upande mwingine, *Electoral College* humaanisha wananchi walioteuliwa kama sampuli itakayopiga kura na hutumika kuaamua ni nani atakayekuwa Rais na Naibu Rais. Kura zao ndizo hutoa uamuzi huo. Kutokana na usawiri huu, msanii analinganisha dhana za *Popular Vote* and *Electoral College* na hali ilivyokuwa katika uchaguzi wa 2017, ambapo kinara wa muungano wa NASA, alionekana kana kwamba atashinda kutokana na umati mkubwa wa watu waliokuwa wakijitokeza katika kampeni zake. Kwa kifupi, ulinganisho huo ulilenga kutashtiti uongozi wa Rais wa nchi ya Kenya, ulionekana kama wa kidikteta kutokana na utumiaji mbaya wa kitengo cha wanajeshi kutimiza alichotaka Rais.

### 4.3.3 Kejeli

Wamitila (2003) anafananua dhana ya kejeli kama yenye ukaribiano mkubwa na dhana ya kinaya. Anadai kuwa kejeli ni hali yoyote inayodokeza unyume katika tukio, usemi au hali. Kwa upande mwingine Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2010), linaeleza kejeli kama neno au tendo la kuonyesha dharau kwa mtu. Hivyo, kutokana na maelezo haya, mtafiti alichukulia dhana ya kejeli kama maneno au matendo yenye unyume ndani yake na kazi yake kuu ni kuonyesha dharau.




***Kibonzo 1: $K_1$UWW, Serikali na Mgomo wa Madaktari. Kutoka (http://gadocartoons.com/govt-doctors-strike/)***

Kutokana na maelezo haya, mtafiti alikumbana na kejeli katika Kibonzo $K_1$UWW ambapo tunaonyeshwa hali iliyosababishwa na mgomo wa madaktari nchini Kenya. Katika kibonzo hiki, wagonjwa au wafu wamerundikwa kwenye kitanda kimoja, hakuna vifaa vya kimsingi vya kuhudumia wagonjwa waliolazwa kwenye hospitali ile. Cha kushangaza ni kuwa Naibu Rais anaonekana akimwambia Rais;

> *Imagine The Number of Votes We Are Losing…!!*
> *Hebu Tafakari ni Kura Ngapi Tunapoteza...!!*

Katika kibonzo hiki kejeli inajitokeza pale ambapo kuna sauti pembeni mwa kibonzo hiki inayomjibu Naibu Rais;

> *They Can Still Be Registered You Know!*
> *Wajua Wanaweza Sajili Bado!*

Maneno haya yanalenga kukebehi na kushambulia mawazo ya Naibu Rais kuwa hali ya wagonjwa waliorundikana hospitalini si ya dhararu na muhimu kama kusajiliwa kwao kama wapiga kura na hatimaye kuwapigia kura. Zaidi ya hayo, maneno yale yalimkebehi Naibu Rais kwa kufikiria hali ya wananchi kufa hospitalini kwa kukosa matibabu sio jambo lenye uzito kuliko wao kupoteza kura za wapigaji kura. Hivyo,

Gado anatusawiria viongozi wabinafsi wasiojali wananchi waliowachagua na azma yao kuu si kubadili maisha ya wananchi bali ni kubadili maisha yao mwenyewe. Katika kibonzo hiki, msanii alitumia kejeli kama mkakati wa kutashtiti Rais na Naibu Rais kwa ubinafsi wao.

Jubilee Will bring Milk & Honey




***Kibonzo 3: $K_1$UO, Jubilee italeta Maziwa na Asali. Kutoka (http://gadocartoons.com/Jubilee-will-bring-milk-honey).***

Vilevile, katika kibonzo 3, $K_1$UO kejeli inajitokeza katika maneno;

> *Forget Water...Jubilee Will Bring Milk and Honey to You. Just Remember...Kura Yako, Haki Yako*!!
> *Sahau Maji .... Jubilee Itawaletea Maziwa Na Asali. Kumbuka Kura Yako, Haki Yako*.

Tukilinganisha maneno haya na hali iliyochorwa na msanii, tunaona hali ya unyume na matumizi ya maneno yenye kusimanga. Katika kibonzo hiki, msanii anatuonyesha taswira ya mizoga na mafuvu ya binadamu iliyotapakaa kila mahali, ishara tosha kuwa wananchi pamoja na mifugo walikwishafariki kutokana na ukosefu wa chakula na maji. Matamshi ya Rais na Naibu Rais katika kibonzo hiki yanadhihirisha kutojali wananchi na kuwadharau wananchi na mahitaji yao.

Zaidi ya hayo, kejeli inajitokeza katika Kibonzo 7, $K_3$UWM ambapo Gado anamsawiri Rais, aliyekuwa Seneta wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi, aliyekuwa gavana wa kwanza

wa Kaunti ya Nairobi na aliyekuwa mwakilishi wa wanawake wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi wakiwa kwenye mkutano wa kudhibiti hasira.

**RageAholics Anonymous**




***Kibonzo 7: $K_3$UWM Mkutano wa Kusaidia Kudhibiti Hasira. Kutoka (www.gadocartoons.com).***

Katika Kibonzo hiki, msanii anatuchorea taswira ya Rais akijitambulisha mbele ya umati uliokusanyika katika mkutano wa kudhibiti hasira. Katika ujitambulishaji wake, msanii anatuonyesha Rais akitamka maneno yanayochukuliwa kuwa ni matusi na ambayo yamesawiriwa na alama kama vile heshtegi, nyota, na mviringo. Isitoshe, Rais anaonekana akisema; *Devils!*

*Mashetani*! na *shindwe*!

Usawiri huu wa Rais unalenga kukebehi tabia yake ya kughadhabika na kutolea watu cheche za matusi, hali iliyojitokeza katika mkutano katika Kaunti ya Turkana ambapo Rais alikuwa ameenda kuzindua mradi wa uchimbaji mafuta ya petroli katika Kaunti ile.

Maneno *RAGEAHOLICS ANONYMOUS Kenyan chapter 12 STEPS OF ANGER MANAGEMENT* yanalenga kukejeli Rais pamoja na viongozi waliosawiriwa wakiwa kwenye mkutano huo. Dhana ya *Rageaholic anonymous* inatokana na mikutano ya watu walio na ugonjwa wa ulevi wa kupindukia *Acoholics Anonymous*. Katika mikutano ile ya kudhibiti ulevi wa kupindukia watu hutiana moyo na kusaidiana katika kuacha ulevi

wa kupindukia. Hivyo, msanii anatumia dhana ile kukejeli Rais kwa tabia yake ya kuonyesha hasira hadharani na kando na hayo, Gado anamshauri Rais kuwa anahitaji usaidizi wa kudhibiti "ugonjwa" wake wa hasira. Kwa kawaida ni vigumu kwa mtu kumkosoa Rais hadharani na kudokeza kuwa anahitaji usaidizi wa wengine ambao wana shida kama yake. Uangaziaji huu wa Gado unathibitisha ukali na uhuru mwingi unaotokana na uchapishaji wa vibonzo katika mitandao.

Isitoshe, hali ya msanii kuwasawiri waliokuwa viongozi mbalimbali wa Kaunti ya Nairobi pamoja na Rais wakiwa kwenye mkutano wa kudhibiti hasira inatokana na matukio mbalimbali yaliyohusu viongozi hawa na wao kuonyesha hasira zao hadharani. Katika muhula wa kwanza wa serikali ya Jubilee, aliyekuwa gavana wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi walijipata na mkwaruzano na aliyekuwa mwakilishi wa wanawake wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi na akamzaba kofi kutokana na hasira (Michira 2013). Vilevile, aliyekuwa Seneta wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi alisawiriwa akiwa kwenye mkutano wa kudhibiti hasira kutokana na mgogoro uliokuwepo kati yake na mwakilishi wa wanawake wa kaunti ile, uliosababisha wawili hawa kutupiana cheche za matusi hadharani. Hivyo, msanii anatumia usawiri huu kuwakejeli na kuwakebehi viongozi hawa kwa kudhihirisha tabia ambazo hazistahili kwa viongozi. Ukebehi huu ulinuia kutashtiti viongozi hawa kwa kukosa maadili na kuonyesha hasira zao hadharani kiasi cha kutupiana cheche za matusi jambo ambalo ni mwiko katika jamii za kiafrika.

Kadhalika, katika Kibonzo 10, $K_3$UKS msanii anatuonyesha hali ya wagombeaji wa viti vya ugavana walivyokuwa wanang'ang'ana kutafuta shahada ili waweze kuwania viti vya ugavana vya kaunti mbalimbali. Katika $K_3$UKS, tunaonyesha taswira ya wawaniaji wa viti vya ugavana katika Kaunti za Kiambu na Nairobi pamoja na manaibu wao. Katika kibonzo hiki tunamwona Baba Yao aliyepewa kodi ya (BY) akisema kuwa hakuna haja ya kujisumbua kutafuta shahada ghushi ilhali mtu anaweza kukodisha shahada halali. Msanii anatumia usemi huu wa BY kumaanisha kuwa Dr. Nyoro aliyepewa kodi ya (DN) na ambaye ni naibu wake alilipwa kuwa naibu wake kwa kuwa ana shahada ambayo inahitajika katika uwaniaji wa kiti cha Ugavana. Kwa upande wa chini wa kibonzo hiki, msanii anatuonyesha taswira ya mheshimiwa Mike Sonko aliyepewa kodi ya MS na naibu wake Polycarp Igathe aliyepewa kodi ya PI. Katika kibonzo hiki tunamuona MS akisema;

*Better Still, Why Buy a Paper Degree While You Can Buy a Walking One*!


*Mbona Ununue Karatasi Ghushi la Shahada Ilhadi Unaweza Nunua Shahada Inayotembea*!

Usemi huu ulikuwa unakejeli hali ya wanasiasa kutafuta shahada ndiposa waweze kuwania viti vya ugavana. Msanii anapomsawiri MS akisema kuwa hamna haja ya kununua "karatasi" ambayo ni shahada. Anaonyesha jinsi viongozi hawa wanavyodharau usomi wa chuo kikuu na kupata shahada kwa kuiita karatasi tu. Kwa upande mwingine usemi huu unakejeli hali ya MS kumchagua PI kama naibu wake, kwa kudokeza kuwa alimchagua kwa kuwa amesoma hadi chuo kikuu na ana shahada.

Pamoja na hayo, mtafiti alichukulia kuwa usemi huo ulimaanisha kuwa Mheshimiwa MS na PI hawakuwa marafiki na inachukuliwa kuwa "alimlipa" PI ndiposa akubali kuwa naibu wake. Isitoshe, pembeni mwa kibonzo hiki kuna kijibonzo kidogo kinachosema kuwa viongozi hawa wanaweza pata bahati na wakapata naibu mwenye maarifa na werevu. Hivyo, kejeli inajitokeza katika usemi wa BY, MS na usemi uliopo pembeni mwa kibonzo kile. Zaidi ya hayo, mtafiti aligundua kuwa msanii alitumia semi hizi kukejeli jinsi viongozi kama vile BY na MS ambao shahada zao zilishukiwa kuwa sio halali waliovyoteua manaibu waliokuwa wamejiimarisha kimasomo na walikuwa na weledi wa miaka mingi katika sekta mbalimbali ili "kuhalalisha" shahada zao na kujenga picha kuwa walikuwa viongozi bora na waliosoma.

### 4.3.4 Kinaya

Kama ilivyokuwa imedokezwa awali, dhana za kinaya na kejeli zina ukuruba mkubwa sana. Wakati mwingi watu hutumia dhana hizi mbili kama visawe. Hata hivyo, tofauti iliyopo kati ya kejeli na kinaya ni kuwa, kejeli inahusisha dhihaka ya moja kwa moja kwa kutumia maneno ya kinyume na ukweli kwa nia ya kudhihaki au kudhalilisha, ilhali kinaya inahusisha tofauti kati ya hali halisi na matarajio, bila lengo la wazi la kudhihaki moja kwa moja. Wamitila (2008) anafafanua kinaya kama tamathali ya usemi ambayo inahususha ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemekana kuwa. Kwa minajili ya utafiti huu, neno kinaya limetumiwa kumaanisha kutenda mambo kinyume cha matarajio. Kamusi ya Karne ya 21, inaeleza dhana ya kinaya kama kinyume cha jambo au hali ya kukinai. Katika vibonzo vilivyoteuliwa, msanii ametumia mbinu ya kinaya kama mkakati wa kutashtiti mienendo na tabia za baadhi ya viongozi wa serikali ya Kenya. ``





***Kibonzo 6: K$_1$UF Kongamano la ugatuzi la mwaka wa 2017. Kutoka (*[http://gadocartoons.com/devolution-conference-2017/](http://gadocartoons.com/devolution-conference-2017/)).**

Kwa mfano, katika Kibonzo 6 K$_1$UF msanii anatuonyesha taswira ya kongamano la nne la ugatuzi nchini Kenya na jinsi magavana na manaibu wao walivyowasili kwenye eneo la mkutano kwa ndege. Kisha kunaonekana mwanamke mmoja, ambaye ametumiwa kuwakilisha wanachi akisema;

*Ooh We Are Making Progress…Before They Used to Arrive in Cars!*
*Aah Tunapiga Hatua…Hapo Mwanzoni Walikuwa Wanawasili Kwa Magari!*

Usemi huu ulinuia kuonyesha hali ya unyume katika matarajio ya wananchi. Kwa kawaida, maendeleo katika nchi yoyote ile hupimwa kwa kuangalia ikiwa maisha ya wananchi yameimarika lakini katika kibonzo hiki, msanii anatuonyesha taswira ya kupima maendeleo kwa kuangalia kuendelea na kuimarika kwa hali ya maisha ya wanasiasa. Isitoshe, matukio katika kibonzo K$_1$UF yanaonyesha tofauti kubwa kati ya wananchi na wanasiasa. Msanii anatuonyesha wananchi walioko chini wakitembea na wanasiasa wakiwa hewani katika ndege zao. Taswira hii ilinuia kuonyesha tofauti zilizopo katika hali za maisha kati ya wanasiasa na wananchi. Hivyo, msanii alitumia mbinu ya kinaya kutashtiti hali ya wanasiasa kuinua hali yao ya maisha badala ya kuzingatia maslahi ya wananchi waliowachagua kuwawakilisha katika bunge au seneti.




***Kibonzo 9: $K_1$UP Msitu Mmoja, Tumbili wale wale. Kutoka*** (***www.gadocartoons.com).***

Kando na hayo, Gado anatumia mbinu ya kinaya katika Kibonzo 9 $K_1$UP, pale ambapo anawasawiri Rais, Naibu Rais pamoja na kinara wa muungano wa NASA RO wakiwa na naibu wake Kalonzo Musyoka aliyepewa kodi ya KM na wanaonekana wakiwafokea wananchi. Katika sehemu ya juu ya kibonzo hiki, Rais anaonekana akisema kuwa dadake pamoja na jamaa za Naibu Rais wake wana haki ya kupata zabuni za serikali kama Wakenya wowote wale. Kando na hayo, RO naye anasema kuwa ndugu yake pamoja na mtoto wa kiume wa naibu wake, KM wana haki ya kupendekezwa kwenye nyadhifa zozote zile. Matamshi ya viongozi hawa ni kinyume na matarajio kwa kuwa, viongozi walioteuliwa na wananchi wanapaswa kuzingatia maslahi ya wananchi na sio kutumia nyadhifa zao kujinufaisha wao wenye pamoja na familia zao. Hivyo, hali ya Rais, Naibu Rais, RO na KM ujinyakulia zabuni za serikali na nyadhifa mbalimbali za serikali na kuwatunuku jamaa zao ilhali kuna mamilioni ya Wakenya waliofikia vipimo vya kupata kazi zile au zabuni zile, ni ubinafsi kwa upande wao. Gado anapoangazia suala la upendeleo na ubinafsi kupitia Kibonzo 9 $K_1$UP, anatumia kinaya kama mkakati wa kutashtiti tabia ya viongozi hawa.

Vilevile msanii ametumia kinaya kutashtiti hali ya Rais na Naibu Rais kutotilia maanani sheria za nchi ya Kenya. Katika Kibonzo 12 $K_2$UWM, tunaonyeshwa taswira ya Rais na Naibu Rais wakienda haja ndogo kwenye kaburi lilioandikwa;

> *Here Lies Chapter 6 Aka Intergity*
>
> *Kaburini Mna Sura ya Sita ya Katiba ya Kenya, Almaarufu Uadilifu*.

Matamshi haya yananuia kueleza msomaji kuwa Rais na Naibu Rais hawana uadilifu katika utendakazi wao. Kando na hayo, msanii anatuonyesha Naibu Rais akimuuliza Rais amkumbushe huo ni ukumbusho wa ngapi, "je ni wa tano, sita, saba?" (Kibonzo 12, K2UWM). Maneno haya yanaonyesha kuwa sio mara ya kwanza kwa viongozi hawa wawili kuvunja sheria na hasa kitengo cha sita ambacho huhitaji watu wanaoshikilia nyadhifa za serikali kuwa na uadilifu.

Matukio katika $K_2$UWM ni kinyume na hali ya kawaida, kwa kuwa inachukuliwa kuwa viongozi na hasa viongozi wa ngazi ya juu kama Rais na Naibu Rais wanapaswa kuwa kwenye mstari wa mbele katika kuzingatia sheria za nchi wanayoiongoza. Hivyo, ni kinaya kuona Rais na Naibu Rais wakiongoza katika kuvunja au kupuuza sheria za nchi. Ndiposa Gado ametumia mbinu ya kinaya kutashtiti tabia ya viongozi hawa wawili. Zaidi ya hayo, kama mtafiti alivyokuwa ameelezea awali kuwa katika jamii za Kiafrika, kuna heshima fulani hupewa wafu na mahali walipozikwa. Hivyo, Gado anaposawiri Rais na Naibu Rais akienda haja ndogo juu ya kaburi la kitengo cha sita cha katiba ya Kenya, usawiri ule unatuonyesha jambo ambalo ni mwiko katika utamaduni wa Kiafrika. Hivyo msanii anapowasawiri Rais na Naibu Rais wakifanya jambo ambalo ni mwiko wakiwa na ufahamu kuwa ni mwiko, alikuwa anapitisha ujumbe kuwa viongozi hawa hawana heshima kwa sheria za nchi ya Kenya na utamaduni wao kama waafrika, hali ambayo ni kinyume cha matarajio yetu.

Pamoja na hayo, msanii ametumia kinaya kama mkakati wa kuibua tashtiti katika Kibonzo 13, $K_2$UF ambapo tunaonyeshwa taswira ya mazishi ya mfanyikazi wa serikali na inachukuliwa kuwa, mwendazake alikuwa mfanyikazi wa ngazi ya juu kwa kuwa Rais na Naibu Rais pamoja na viongozi wa upinzani wa wakati huo walihudhuria mazishi yale. Katika upande wa juu wa kibonzo kile, tunaonyeshwa padre akisifu mwendazake kama mfanyikazi mnyenyekevu aliyejitolea mhanga kuwatumikia wananchi. Hali ya unyume inajitokeza katika kibonzo hiki kwani msanii anatuonyesha mwendazake akimpatia padre hongo na chini ya kaburi lake kumefichwa uchafu mwingi uliotajwa kama, ufisadi, mauaji na hata wizi wa ngazi ya juu.

Katika jamii nyingi za Kiafrika watu huwa hawaneni kuhusu maovu ya watu waliokufa, hata kama aliyekufa alijulikana kuwa alikuwa mwizi au mtu fisadi, watu huzungumzia mazuri yake. Hivyo, msanii alituonyesha hali ya unyume kwa kutuonyesha taswira ya padre akimsifu mfanyikazi aliyeendeleza maovu kama vile, ufisadi, mauaji, na wizi wa

ngazi ya juu kama kiongozi mnyenyekevu. Katika kibonzo hiki, Gado anatumia mbinu ya kinaya kutashtiti tabia ya viongozi wa madhehebu kuwasifu viongozi waliojulikana kuwa wafisadi na waongo kwa minajili ya kupata faida kutokana na mifuko ya viongozi walio serikalini.

## Join the Catwalk…! #DP#Waiguru




***Kibonzo 18: K$_1$UN Jiunge na Tamasha la Maonyesho ya Urembo...! #Dp #Waiguru Kutoka (www.gadocartoons.com).***

Zaidi ya hayo, Gado anatumia mbinu ya kinaya kutashtiti Naibu Rais na aliyekuwa gavana wa pili wa Kaunti ya Kirinyaga kama inavyoonekana katika Kibonzo 18, K$_1$UN. Matukio katika kibonzo hiki yanatuonyesha taswira ya Naibu Rais na gavana wakitembea kwenye zulia inayowaelekeza kwenye meza ya kuapishwa. Gavana amesawiriwa akiwa na nywele ndefu zilizoandikwa NYS, ambacho ni kitengo cha mafundisho cha vijana nchini Kenya na Naibu Rais amevalia kilemba. Katika kibonzo kile tunaonyeshwa Naibu Rais akimsifia Gavana kwa nywele zake ndefu kwa kumwambia;

*Nice Hair, Governor*
*Nywele Nzuri, Gavana*


Naye Gavana anaonekana akimwambia Naibu Rais;

*Nice Turban, Deputy President*!
*Kilemba Kizuri, Naibu Rais*!

Gado amemsawiri Naibu Rais akiwa na kilemba kumtashtiti baada ya Naibu Rais kuonekana akiwa amevalia kilemba cha wafuasi wa dini ya Sikh alipohudhuria harusi ya wafuasi wa dini ile katika mwaka wa 2016. Kulingana na itikadi za wafuasi wa dini

ya Sikh kilemba huvaliwa kama ishara dhabiti ya imani yao, uadilifu na uazimaji wao katika kutumikia binadamu wote bila ubaguzi kwa misingi ya rangi, jinsia au dini ("What the Sikh Turban Means", 2017). Hivyo, Gado anapomsawiri Naibu Rais akiwa na kilemba anajaribu kumtashtiti na kumsuta kwa kuvali kilemba kinachoashiria uadilifu, ukweli na usawa ilhali msanii amekuwa akimsawiri Naibu Rais kama mwanasiasa ambaye hana maadili na mwenye kupuuza sheria za nchi kama ilivyotambulika katika Kibonzo 12, $K_2$UWM. Katika kibonzo 18 $K_1$UN, msanii anatuelezea jinsi unafiki wa Naibu Rais na Gavana wa Kaunti ya Kirinyaga unavyoimarisha kinaya. Naibu Rais anaposawiriwa akiwa amevalia kilemba cha waumini wa dini ya Sikh, anajifanya kuwa mwadilifu na mtu ambaye hutenda mema ilhali, ni mtu mfisadi ambaye ana tuhuma nyingi za ufisadi, hali inayokinai picha ya kiongozi mwaminifu na mwenye maadili.

Vilevile, katika kibonzo $K_1$UN, aliyekuwa gavana wa pili wa Kaunti ya Kirinyaga amesawiriwa akiwa na nywele ndefu zilizojisokota na zilizoandikwa NYS kumaanisha kuwa ingawaje kiongozi huyu alichaguliwa kama Gavana wa Kaunti ya Kirinyaga, bado alikuwa anafuatwa na tuhuma za ufisadi na ufujaji wa pesa katika kitengo cha NYS. Hapa mbinu ya kinaya inajitokeza msanii anapomsawiri Naibu Rais akiwa wamevalia kilemba cha dini ya Sikh kilichoficha tuhuma zake za ufisadi na sakata za wizi wa ardhi za umma ilhali matendo yake ni kinyume na tabia na mienendo ya mfuasi wa dini ile. Pili, tashtiti inajitokeza pale ambapo Gado anamsawiri Naibu Rais akisifia nywele za Gavana ilhali inaashiri tuhuma za ufisadi katika kitengo cha NYS alichokuwa akisimamia kabla ya kuwania ugavana. Katika nchi ya Kenya, ili mtu aweza kuwania wadhifa wowote ule ni lazima atimize mahitaji ya kitengo cha sita cha katiba ya nchi ya Kenya, kinachomhitaji mgombeaji awe mtu mwaminifu, asiyekuwa na rekodi ya uhalifu na awe mwadilifu. Hivyo, ni kinaya kuona kuwa Gavana wa Kaunti ya Kirinyaga anaapishwa kama gavana ingawaje bado alikuwa anafutwa na tuhuma za ufisadi katika kitengo cha NYS.  Kwa kifupi, Gado alitumia kinaya kama mkakati wa kutashtiti Naibu Rais na Gavana wa Kaunti ya Kirinyaga wa wakati huo.




***Kibonzo 20: K$_4$UF. Funga Macho na Uombe. Kutoka (http://gadocartoons.com/close-eyes-pray/).***

Pamoja na hayo, Gado alitumia mbinu ya kinaya kuwatashtiti na kuwasuta Rais na Naibu Rais kama inavyoonekana katika Kibonzo 20 K$_4$UF. Katika kibonzo hiki tunaonyeshwa taswira ya Rais akiwa amebeba sanduku linalochukuliwa kuwa na pesa huku Naibu Rais amebeba gunia linaloonekana kuwa na pesa. Nyuma yao, kuna mwanamke anayeonekana akiomba, na mtafiti alichukulia kuwa mwanamke yule alikuwa akiombea viongozi hawa wawili. Gado anatusawiria Naibu Rais akimwambia mwanamke yule ayafumbue macho yake baada ya miaka mitano. Matukio katika kibonzo hiki yanadhihirisha kinaya kwa kuwa, inachukuliwa kuwa kiongozi aliyechaguliwa katika ngazi ya urais anapaswa kuwa akilinda na kuzalisha mali ya nchi na sio kuipora. Kwa kawaida, wananchi hutarajiwa kuombea na kuheshimu uongozi wa nchi yoyote ile.

Hivyo katika kibonzo hiki, Gado anatuonyesha kuwa wananchi wanatimiza wajibu wao lakini viongozi wanawapora na kuwanyanyasa wananchi kwa kuwaibia. Usemi wa Naibu Rais;

> *And Open Them After We Count Five Years!*
> *Na Uyafumbue Tukishahesabu Miaka Mitano!*

unadhihirisha kuwa wananchi watagundua kuwa walihadaiwa baada ya miaka mitano wakielekea kwenye uchaguzi mwingine. Kwa miaka mingi, wakenya wamekuwa wakichagua viongozi ambao ni wafisadi na wanaopora mali yao, cha kushangaza ni

kuwa suluhu yao kwa tatizo hili ni kuombea viongozi hawa wabadilike na baada ya miaka mitano badala ya kubadilisha aina ya viongozi wanaowachagua, wanachagua viongozi walewale wafisadi. Kwa upande mmoja, Gado anatumia kinaya kama mkakati wa kitashtiti kwa minajili ya kushambulia viongozi wanaotumia mamlaka waliyopewa kuiba mali ya umma. Pili, msanii anawatashtiti wananchi wanaochagua viongozi wafisadi kila baada ya miaka mitano na badala ya kuchukua hatua ya kubadili viongozi wanaowachagua wanaamua kuwaombea viongozi hawa wabadilike. Hivyo, msanii alikuwa anawatashtiti wananchi wa Kenya kwa ujinga wao.

### 4.3.5 Metonimia

Dhana ya metonimia hutumika kuwakilisha neno au dhana nyingine ambazo zina uhusiano fulani. Kovecses (2006) anaeleza metonimia kama uhusiano ambao elementi moja husimamia elementi nyingine ambayo ina ukaribiano mkubwa na hutumika badala ya kitu kingine ambacho kinahusiana nacho. Kwa kifupi, metonimia hujitokeza pale ambapo kuna uhamishaji wa maana kwa misingi ya ushirika. Kwa mfano, mtu anaposema "Je umelionaje gurudumu langu?" neno gurudumu pale limetumika kumaanisha gari na sio gurudumu la gari. Hivyo neno gurudumu pale limetumika kama metonimia inayomaanisha gari. Katika utafiti huu, mtafiti alitambua metonimia za kuonekana kama anavyoeleza katika sehemu hii.

Mfano mmoja wa metonimia unajitokeza katika Kibonzo 10 $K_3$UKS ambapo Gado anazungumzia hali ya sheria ya nchi kuwataka wagombea viti vya ugavana kuwa na shahada. Katika kibonzo kile msanii anatuonyesha taswira ya mgombeaji kiti cha ugavana cha Kaunti ya Kiambu, Baba Yao (BY) na Naibu wake Dr. Nyoro (DN). Msanii anatuonyesha BY akisema;

> *Why Struggle to Get a Fake Degree While You Can Hire a Real One…*
> *Mbona Ujisumbue Kupata Shahada Ghushi ilhali Unaweza Kodisha Shahada Halali*,

Kumaanisha kuwa maneno *You Can Hire a Real One* yametumika kumaanisha kuwa BY alimkodisha DN kuwa naibu wake kwa kuwa ana shahada. Hivyo usemi wa BY unadhihirisha metonimia. Wakati BY alikuwa akiwania kiti cha Ugavana cha Kaunti ya Kiambu, kulikuwa na madai kuwa shahada yake aliyoipata kutoka India ilikuwa ghushi. Hivyo, msanii aliangazia tendo lake la kumchagua DN aliyekuwa na shahada ya uzamifu kutoka Uingereza kama njia ya kujaribu kuhalalisha ugombeaji wake, kwa


kuonyesha watu ingawaje walishuku shahada yake, angalau naibu wake alikuwa na shahada kutoka Uingereza na alikuwa na tajriba ya kuwa mkurugenzi katika kampuni kubwa. Kwa kifupi tendo la BY kumteua DN kama naibu wake, lilichukuliwa kwamba alimkodisha DN kwa sababu ya masomo yake na sio kwa sababu ya uwezo wake wa kuwa kiongozi wanayeweza kufanya kazi naye. Kutokana na maelezo haya, inadhihirika kuwa msanii alitumia metonimia kwa kulinganisha DN na shahada iliyo halali kwa minajili ya kutashtiti uteuzi wa manaibu gavana nchini Kenya.

Vilevile, katika sehemu ya chini ya Kibonzo 10 $K_3$UKS tunaonyeshwa mgombeaji kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi Mike Sonko aliyepewa kodi ya MS akisema;

> *Better Still, Why Buy a Paper Degree While You Can Buy a Walking One…*
> *Mbona Ununue Karatasi Ghushi La Shahada Ilhadi Unaweza Nunua Shahada Inayotembea*.


Usemi huu katika Kibonzo 10 $K_3$UKS unamaanisha kuwa MS "amemnunua" naibu wake Polycarp Igathe aliyepewa kodi ya PI kwa kuwa ana shahada. Polycarp Igathe alikuwa amesoma hadi kiwango cha uzamili na isitoshe alikuwa amefanya kazi kama mkurugenzi mkuu wa mojawapo wa benki maarafu nchini Kenya. Hivyo basi, msanii anapotuonyesha MS akimteua PI kama naibu wake, ujumbe anaotupasha ni kuwa MS alimnunua au kumrai PI kwa hela ili aweze kuwa naibu wake, ndiposa aweze kuhalalisha uwaniaje wake. Kitendo hiki kilisababishwa na madai kuwa shahada ya MS ilikuwa ghushi. Usemi huo wa MS unadhihirisha matumizi ya metonimia kwa minajili ya kutashtiti tabia ya viongozi mbalimbali kuchagua manaibu wao kutokana na sababu zao za kibinafsi na sio kwa kuwa wanajuana na wanaweza wakafanya kazi pamoja.

Zaidi ya hayo, msanii anatumia metonimia katika kibonzo 17, $K_2$UO, pale ambapo Rais amesawiriwa akiwa amevalia sare kamili ya wanajeshi, mkononi amebeba fimbo ya uongozi na kichwani kuna taji la ufalme. Kwa kawaida, Rais wa nchi ya Kenya anatambulika na kujulikana kama kamanda mkuu wa majeshi na si muwala kuvalia sare rasmi ya wanajeshi.





***Kibonzo 17: K2UO, Utekelezaji wa Ajenda ya Jubilee. Kutoka (<u>www.gadocartoons.com</u>).***

Kando na hayo, Gado anapomsawiri Rais akiwa amevalia taji la ufalme na fimbo ya ufalme anajaribu kutashtiti hali ya Rais kusisitiza kuwa yeye ndiye Rais aliyeteuliwa. Hivyo, Gado ametumia ishara ya Rais kuvalia sare rasmi ya wanajeshi pamoja na taji na fimbo za kifalme kutashtiti tabia ya Rais ya kujigamba na kutumia mamlaka yake vibaya kwa kuwa anajiona kama Rais, mkuu wa majeshi na pia mfalme wa nchi ya Kenya ilhali nchi ya Kenya ni nchi ya kidemokrasia inayofuata mfumo wa uongozi wa urais na si wa Kifalme.




***Kibonzo 15: K4UO kinyang'anyiro cha ugavana katika Kaunti ya Nairobi. Kutoka (<u>http://gadocartoons.com/nairobi-gubernotorious-race/</u>).***

Vilevile, mbinu ya metonimia inadhihirika katika kibonzo 15, $K_4UO$ pale ambapo msanii anamsawiri MS akiwa amevalia kiwinda kinachoonekana kuwa na mkojo na kinyesi. Kwa kawaida, kibenda au nepi hufungwa watoto wachanga ambao bado hawajakomaa. Hivyo, Gado anapomsawiri mheshimiwa MS kwa njia ile anajaribu kumaanisha kuwa kiongozi yule ana utoto na bado hajakomaa. Uangazijia huu wa mgombeaji MS huenda ulitokana na tabia ya kiongozi huyu, kuwa na mavazi ambayo kwa kawaida, huwa ya vijana wadogo na si mzee wa miaka yake. Isitoshe, kiongozi huyu alikuwa na mazoea ya kuunda video za kujigamba na kuonyeshana utajiri wake na alikuwa mtu ambaye hawezi kuweka siri. Mara nyingi alitoboa siri za viongozi wenzake na kuwatia aibu mbele ya watu, tabia ambayo ni kawaida kwa watoto. Hivyo, msanii alitumia metonimia kwa msawiri MS akiwa na kiwinda kilicho na kinyesi kutashtiti kiongozi huyu kwa tabia zake za kitoto pamoja na maovu aliokuwa akitenda.




***Kibonzo 16: $K_5UO$ Kura za Waliowengi dhidi ya Kura za waliteuliwa. Kutoka (www.gadocartoon.com).***

Pamoja na hayo, metonimia inajitokeza katika Kibonzo 16, $K_5UO$ ambapo msanii anatuonyesha taswira ya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017. Kibonzo hiki kinatuonyesha taswira mbili zinazohusiana na ukinzani uliozuka baada ya uchaguzi wa Rais. Kwa upande mmoja, kinara wa muungano wa NASA RO amesawiriwa akiwa amevalia gauni la ufalme la rangi ya zambarau. Kulingana na wataalamu wa masuala ya rangi, rangi ya zambarau hupatikana baada ya kuchanganya rangi nyekundu na samawati. Kwa kawaida rangi nyekundu katika siasa huwakilisha mamlaka na kuwa mwenye mamlaka ilhali samawati humaanisha kuaminika (Yu, 2014).

Hivyo, Gado anapomsawiri RO akiwa amevalia gauni la zambarua anamaanisha kuwa Mheshimiwa RO alikuwa na mamlaka, madaraka na alikuwa kiongozi wa kuaminika. Kando na hayo, gauni lile lilikuwa limeshikiliwa na wananchi na upande wa juu wa kibonzo kile kuna maneno "*Popular Vote*" ambayo yanamaanisha kuwa Mheshimiwa RO alichaguliwa na kushinda uchaguzi wa 2017 kupitia kura za walio wengi na hasa wananchi. Kwa upande mwingine, msanii anatuonyesha taswira ya Rais akiwa amevalia gauni la kifalme la rangi nyekundu. Gauni lile linawakilisha mamlaka na linatumika kupitisha ujumbe kuwa aliyelivalia ni mwenye kushika hatamu za uongozi wa nchi ya Kenya.

Zaidi ya hayo, tunaonyeshwa gauni la Rais likiwa limeshikiliwa na wanajeshi. Hapa mtafiti alipata ujumbe kuwa msanii alikuwa anaonyesha kuwa ushindi wa Rais uliwezekana kupitia wanajeshi na kuwa uongozi wake utalindwa na wanajeshi. Kwenye upande wa juu wa kibonzo kile kuna maneno "*Electoral College*" ambayo ni dhana inayotumika katika uchaguzi nchini Marekani ambapo watu maalum huchaguliwa kwa minajili ya kumchagua Rais na Naibu Rais watakaochukua hatamu za uongozi. Kutokana na maelezo haya, mtafiti alithibitisha kuwa msanii alitumia rangi za zambarau na nyekundu kama metonimia kwa minajili ya kutashtiti uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017. Zaidi ya hayo, dhana za kura za walio wengi na kura za wateule na hali ya gauni ya RO kushikiliwa na wananchi na gauni la Rais kushikiliwa na wanajeshi lilitumika kama metonimia kwa minajili ya kutashtiti hali ya mvutano uliozuka baina ya viongozi hawa wawili baada ya uchaguzi mkuu, ambapo kila mmoja aliamini kuwa alikuwa ameteuliwa kama Rais wa nchi ya Kenya. Kutokana na maelezo haya, huenda msanii alitaka kutueleza kuwa kinara wa muungano wa NASA, RO huenda ndiye aliyeshinda uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017, kwa misingi ya dhana ya "*Popular Vote*", lakini Rais akatangazwa kuwa Rais wa nchi ya Kenya kutokana na mamlaka aliyokuwa nayo kama mkuu wa majeshi.

Kando na hayo, Gado ametumia mbinu ya metonimia katika Kibonzo 19, $K_6$UO kupitia mchoro wa mwanamke na mwanaume wanaovuta mkototeni uliobeba Rais na naibu wake Msanii Gado anatusawiria mkokoteni ulio na magurudumu ya miraba minne. Kwa kawaida, mkokoteni huwa na magurudumu ya duara ambayo huufanya uwe rahisi kuuvuta. Hivyo, Gado anapotuonyesha mkokoteni ulio na magurudumu ya miraba minne unaojaribu kuvutwa kwenye mlima uliojaa mawe, mwanakibonzo huyu

anatuonyesha hali ngumu ya maisha ya wananchi. Gado anapitisha ujumbe kuwa serikali ya Rais imewabebesha wananchi mzigo mzito ambao ni vigumu kwao kuubeba. Hivyo, taswira ya mkokoteni wenye magurudumu ya miraba minne unaokwea mlima uliojaa mawe imetumika kama metonimia ya kutashtiti hali ngumu ya maisha inayowakumba wananchi wa Kenya. Kwa msingi ya nadharia ya semiotiki, mhimili wa kiishara na kirejelezi, katika muktadha wa nchi ya Kenya, aghalabu mikokoteni huvutwa na punda. Hivyo, ishara ya mkokoteni inatujengea picha ya punda anayevuta mkokoteni. Kutokana na hayo, tunaweza kusema kuwa msanii anapotuonyesha picha ya wananchi wakivuta mkokoteni analinganisha wananchi na punda anayevuta mkokoteni. Kwa kawaida punda hufanyishwa kazi ngumu na huwa hatunzwi kama wanyama wengine wanaofugwa nyumbani, yeye hupata tu chakula pekee. Basi, kutokana na Kibonzo $K_6$UO, tunapata ujumbe kuwa Rais na Naibu Rais ni viongozi wanaowatumia wananchi vibaya, kwa kuwatwika mizigo mizito ya ushuru mkubwa na hawafanyi lolote kutunza wananchi waliowachagua. Usawiri huu ulitumia metonimia ya mkokoteni, na punda kutashtiti Rais na Naibu Rais kwa kuwanyanyasa na kuwahujumu wananchi waliowachagua.

### 4.3.6 Analojia

Mwetulundila na Kangira (2012) wanaelezea analojia kama mlinganisho au mfananisho wa vitu viwili ambavyo havifanani lakini vina sifa au hulka zinazolandana. Msanii wa vibonzo vilivyoteuliwa ametumia analojia katika Kibonzo 5, $K_2$UWW anapolinganisha uhusiano kati ya madaktari wa nchi ya Kenya na serikali ya Rais na ndoa ya unyanyasaji ambapo bibi ananyanyaswa na kudhalilishwa na mumewe kwa kupigwa. Matukio yaliyosawiriwa katika kibonzo hiki yanalinganisha hali ya madaktari wa nchi ya Kenya na ndoa yenye manyanyaso. Hivyo mtafiti alithibitisha kuwa msanii alitumia ulinganisho huo kutashtiti hali ya serikali kuwakandamiza na kuwanyima madaktari wa nchi ya Kenya haki zao.

Waaidha, dhana ya analojia inajitokeza katika Kibonzo 7, $K_3$UWM ambapo msanii anatuonyesha taswira ya Rais akiwa kwenye mkutano wa kudhibiti hasira. Gado amelinganisha matukio katika kibonzo hiki na mikutano ya watu ambao wameshindwa kudhibiti kiwango chao cha ulevi. Mikutano hii, huwa njia moja ya kukabiliana na ugonjwa wa ulevi wa kupindukia. Msanii ametumia maneno "*RAGEAHOLICIS ANONYMOUS Kenyan Chapter 12 steps of ANGER MANAGEMENT*" kutoa

ulinganisho na mikutano ya *Acoholics Anonymous the 12 steps*. ("The Twelve Steps | Alcoholics Anonymous", 2022) ambayo huwa ya watu ambao wameshindwa kudhibiti kiwango chao cha ulevi. Kutokana na ulinganisho huo, msanii anapitisha ujumbe kuwa Rais anaugua ugonjwa wa kuwa na hasira nyingi kupindukia na jambo ambalo lingemsaidia ni kujiunga na mikutano ya kudhibiti hasira zake. Kutokana na hayo, mtafiti alidadavua kuwa msanii alitumia mbinu ya analojia kutashtiti Rais, aliyekuwa mwakilishi wa wanawake wa Kaunti ya Nairobi, aliyekuwa gavana wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi na aliyekuwa seneta wa kwanza wa Kaunti ya Nairobi kwa kushindwa kudhibiti hasira zao.




***Kibonzo 14: K$_3$UF Majini yametoka kwenye chupa #Unyakuzi wa Ardhi. (www.gadocartoons.com).***

Katika kibonzo 14, K$_3$UF ambapo Gado anatuonyesha taswira ya Rais akiwa amefungua chupa iliyoandikwa;

*Land Grabbing*

*Nyakuzi Wa Ardhi Ya Umma*

Ndani ya chupa ile kunatokea mvuke wa kijani kibichi ulio na sura za viongozi mbalimbali wa nchi ya Kenya. Isitoshe, msanii anakipa kibonzo hiki anwani ya "*The Genies are out of the Bottle".* Uchambuzi wa kibonzo hiki ulidhihirisha kuwa Gado alilinganisha matukio katika kibonzo K$_3$UF na hadithi maarafu ya "*Alladin and the magic lamp*" ambapo kijana Alladin alikumbana na taa iliyokuwa na mazingaombwe. Katika hadithi ile, Alladin alipogusa taa, kulitokea jini la rangi ya samawati lililoahidi

kumpa chochote alichotaka. Hivyo, msanii alilinganisha Rais na Alladin na tofauti kati ya jini wa Alladin na jini wa Rais wa Kenya ni kuwa, jini la Alladin alimtajirisha na kumpa chochote alichotaka ilhali jini anayeonekama kutoka kwenye chupa cha Rais analeta masaibu kwa kuwa wanyakuzi wa ardhi za umma ni baba yake pamoja na watu anaowajua na ni wandani wake. Hivyo, msanii alinuia kutujuza kuwa waliohusika na sakata ya unyakuzi wa ardhi ya umma ni watu ambao walijulikana na Rais. Kando na hayo, ingelikuwa vigumu kwa Rais kupambana nao kwa kuwa hata yeye mwenye alikuwa amefaidika kutokana na ardhi za kunyakuliwa.

### 4.3.7 Matumizi ya Anwani, Vipovu vya Sauti na Kutaja


Kwa kawaida wanavibonzo hutumia anwani, vipovu vya sauti na kutaja katika vibonzo wanavyochora kwa minajili ya kudokeza ama kuweka wazi masuala ambayo wanasawiri kupitia michoro yao. Kwa kiwango kikubwa, wanavibonzo wanapotumia anwani, vipovu vya sauti na mbinu ya kutaja huwa hawatoi maelezo ya moja kwa moja ila huwa wanatumia mambo haya matatu yaliyotajwa awali kudokeza tu na kazi ya anayekitazama kibonzo kile ni kudadavua na kuelewa ujumbe ambao mchora kibonzo anajaribu kupitisha.

Katika uchunguzi wake, mtafiti aligundua kuwa mwanakibonzo Gado si tofauti na wanavibonzo wengine. Kutokana na sampuli iliyoteuliwa, mtafiti aligundua kuwa kwa kiasi kikubwa Gado alitumia anwani, vipovu vya sauti na kutaja, aidha kudokeza yanayotokea katika vibonzo vyake ama kama njia ya kuibua tashtiti kupitia mbinu zinginezo za lugha kama vile kejeli na kinaya. Kwa mfano, msanii ametumia anwani katika vibonzo vyake kama njia ya kudokeza tu yanayojitokeza katika vibonzo vyake. Mathalan, katika Kibonzo 2, $K_1$UKS Gado ametumia anwani "*NASA and their Campaign*" kudokeza yanayoonekana kwenye kibonzo kile. Taswira ya watu wanaonekana kukwea mlingoti ulioandikwa "*FLAG BEARER*" na mtego ulioandikwa NASA wenye kuku mwenye kutoa harufu ya kuvutia inaweza kumkanganya mtu ambaye hana uelewa kuhusiana na matukio ya kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2017, lakini anwani ile ya *NASA and their Campaign* inamsaidia mtu yeyote kuelewa kinachosawiriwa katika kibonzo kile.

Vilevile katika kibonzo 16 $K_5$UO, msanii ametumia anwani za *"POPULAR VOTE*" na "*ELECTORAL COLLEGE*" kudokezea hadhira yake kuhusu mambo ambayo hayakuwa wazi katika kibonzo kile. Kando na hayo, Gado ametumia anwani ile kuchochea

anayetazama kibonzo kile kufanya uchunguzi zaidi, kwani kwa kawaida dhana za "*Popular Vote*" and "*Electoral College*" ni mambo ambayo hayafanyiki nchini Kenya. Hivyo, msomaji akikumbana na anwani kama ile itamchochea kutaka kujua maana ya dhana zile mintarafu ya yanayosawiriwa katika kibonzo kile.

Isitoshe, kuna wakati wanavibonzo hutumia vipovu vya sauti kujaribu kufafanua yasiyojitokeza moja kwa moja katika michoro yao. Mtafiti aligundua kuwa kuna wakati msanii alitumia vipovu vya sauti kudokezea masuala aliyotaka kusawiri na kuna wakati alitumia mbinu hii pamoja na anwani kuhakikisha kuwa ujumbe wake umeeleweka zaidi kwa hadhira yake. Kwa mfano, katika Kibonzo $K_1$UO Gado ametumia anwani *Jubilee Will Bring Milk and Honey* kudokezea yanayojitokeza katika kibonzo kile. Fauka ya hayo, Gado ametumia vipovu vya sauti *Forget water…Jubilee will Bring Milk na Honey* na *Kumbukeni Kuwa Kura Yako Ni Haki Yako* kudokezea kutowajibika kwa Rais na Naibu Rais. Kando na hayo, anwani ile, pamoja na vipovu vya sauti katika kibonzo kile, zililenga kuibua kinaya kwani inatakikana Rais aelewe mahitaji na matakwa ya watawaliwa wake na ayatimize, ilhali msanii anatuonyesha taswira ya Rais anayepuuza matakwa ya wananchi.




***Kibonzo 9: $K_1$UP Msitu Mmoja, Tumbili wale wale. Kutoka*** (***[www.gadocartoons.com](http://www.gadocartoons.com)).***

Katika Kibonzo $K_1$UP msanii Gado ametumia vipovu vya sauti;

*Yes, My Sister and The Dp's Relatives Have a Right to Government Tenders Like Any Other Kenyan.*

*Ndio, Dadangu Na Jamaa Za Naibu Wangu Wanahaki Ya Kupata Zabuni Za Serikali Kama Mkenya Yeyote Yule*


*na*

*My Brother and My Deputy's Son Have a Right Like Any Other Kenyan To Be Nominated for Any Position*

*Ndugu Yangu Pamoja Na Mtoto Wa Kiume Wa Naibu Wangu Wanahaki Ya Kuteuliwa Katika Nyadhifa Zozote Zile Kama Wakenya Wengine*

Kudokezea suala la upendeleo kwa upande wa Rais na Naibu Rais na vinara wa NASA RO na KM. Isitoshe, msanii alitumia semi hizi zilizokuwa kwenye vipovu vya sauti kukejeli viongozi hawa kwa kutumia nyadhifa zao kujinufaisha wao wenyewe na jamaa zao. Msanii alitumia maneno yaliyo kwenye vipovu vya sauti kuibua kejeli kama mkakati wa kutashtiti Rais na Naibu Rais na viongozi wa muungano wa NASA RO na KM.

Pamoja na hayo, mchora kibonzo anaweza kutumia mbinu ya kutaja wakati anapotaka kuondoa utata katika vibonzo vyake. Kwa mfano, katika Kibonzo $K_2$UKS, msanii anatuonyesha taswira ya punda aliyeandikwa NASA akiwa amebeba viongozi wa muungano wa NASA na mwanaume aliyeandikwa Oloo akiwa ameshikilia mkia wake.




***Kibonzo 4: K2UKS, Oloo ajiunga na NASA. Kutoka (http://gadocartoons.com/oloo-joins-nasa/).***

Gado ametumia mbinu ya kutaja ambapo ametambulisha vitu au watu waliosawiriwa kwa minajili ya kuondoa utata wowote unaoweza kutokea wakati wa kuchambua na kuelewa kibonzo kile. Ikiwa msanii alituchorea mtu aliyeshikilia mkia wa punda bila kutaja jina la aliyeshikilia punda, ingekuwa vigumu kwa mtafiti kuelewa ujumbe uliokuwa ukipitishwa na msanii. Vilevile, Gado anapotumia mbinu ya kutaja pamoja na kusawiri punda aliyebeba viongozi wa muungano wa NASA, alitaka kusisitizia usemi uliokuwa ukienezwa nchini wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa 2017, kuwa mashindano ya kiti cha urais yalikuwa baina wa wanyama wawili, punda na farasi. Watu walichukulia kuwa chama cha Rais cha Jubilee kilikuwa farasi ilhali, muungano wa NASA ndio uliokuwa punda.

## Hiring and Buying Degrees




***Kibonzo 10: K3UKS, Kukodisha na kununua shahada. Kutoka (<u>www.gadocartoons.com</u>).***


Vilevile mbinu ya kutaja inajitokeza katika Kibonzo K3UKS ambapo watu waliosawiriwa katika kibonzo hiki wametambulishwa. Katika kibonzo kile kuna BABA YAO (BY) ambaye alikuwa mgombeaji wa kiti cha ugavana katika Kaunti ya Kiambu na naibu wake Dr. Nyoro (DN) na Igathe (PI) aliyekuwa naibu wa MS katika kinyang'anyiro cha kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi. Kutokana na maelezo haya tunaona kuwa msanii alitaja watu aliokuwa anasawiri kwa minajili ya kuondoa utata na kudokeza kamili alikuwa anasawiri nini katika vibonzo vyake.

Kutokana na mifano na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa msanii ametumia anwani, vipovu vya sauti na kutaja kama mbinu ya kudokeza yaliyokuwa yakijitokeza katika vibonzo alivyochora. Pili, kama njia ya kulenga palipo na kuondoa utata katika

vibonzo vyake hasa alipotumia mbinu ya kutaja. Kando na hayo, Gado ametumia vipovu vya sauti kuibua kinaya na kejeli katika mambo anayosawiri. hivyo, msanii anapotumia anwani, vipovu vya sauti na kutaja anataja mambo kwa uwazi bila kuficha lolote na kutokana na suala hilo, tunaona uhuru na ukali mwingi unaotokana na uhamiaji wa vibonzo kutoka magazetini hadi kwenye mtandao.

### 4.3.8 Matumizi ya Alama

Wakati mwingine wanavibonzo hutumia alama kuwakilisha mambo ambayo hawataki kusema wazi wazi. Hali hii inajitokeza katika Kibonzo $K_3$UWM ambapo msanii anatuonyesha usemi wa Rais akiwa kwenye mkutano wa kudhibiti hasira na Gado ametumia alama za reli, nyota, mviringo na heshtegi kuwakilisha maneno ya matusi.




***Kibonzo 7: $K_3$UWM Mkutano wa Kusaidia Kudhibiti Hasira. Kutoka (www.gadocartoons.com).***

Msanii alitumia matukio katika Kibonzo $K_3$UWM kuelezea matukio yaliyotokea kwenye mkutano wa ziara ya Rais katika Kaunti ya Turkana. Rais alikuwa ameenda kuzindua mradi wa uchimbaji mafuta katika eneo la Tulow. Gavana Nanok alipotoa hotuba yake, alimrai Rais kuhakikisha kuwa asilimia kubwa ya faida inayotokana na uchimbaji wa mafuta katika eneo lile ibaki kwenye Kaunti na asimilia iliyobaki ipashwe kwenye serikali ya kitaifa.

Rais alikerwa na matamshi ya Gavana Nanok na akatamka maneno haya;

"*Mtu akisimama hapa aseme ati Uhuru ako na haja na mafuta ya wengine. Ashindwe shetani mshenzi...si mimi napitisha sheria. Kazi yangu ni kupitisha kidole halafu mjinga anakuja hapa kusema... Wa kufikiria mimi ni mtu wa kutishwa watafute mwingine. Mimi shida yangu sio uongozi. Mi shida yangu ni kufanya kazi ambayo itabadilisha maisha ya wananchi. Kwa hivyo wakufikiria mimi ni mtu ya kutishishwa watafute mwengine. Kura ni kura na tutakuja kuomba kama wengine... mtupatie mkose kutupatia kwani mnafikiri dunia itaisha."* (Muchiri, 2017).

Hivyo katika kibonzo kile, Gado alitumia alama za nyota, heshtegi, na mviringo kuficha matusi yaliyotamkwa na Rais. Usawiri wa Rais kama mtu mwenye hasira na anayeweza tamka maneno ya matusi hadharani ulilenga kumkejeli Rais kwa tabia hii na pia kumtashtiti.

Licha ya hayo, alama za heshtegi, mzunguko, na nyota zimetumika katika Kibonzo $K_1$UWW kuashiria utukano katika usemi ya Naibu Rais. Msanii anatuonyesha taswira ya Naibu Rais anayekerwa na wagonjwa wanaokufa hospitalini kutokana na mgomo wa madaktari. Badala ya Naibu Rais kuona matatizo yanayowakumba wananchi katika hospitali za umma, msanii anatusawiria Naibu Rais anayekerwa na kura wanazopoteza kutokana na kufa kwa wapigaji kura. Katika kibonzo hiki, Gado alitumia msururu wa alama kuwakilisha neno la utukano kwa minajli ya kuonyesha hali ya kutojali na ufedhuli wa Naibu Rais.

Zaidi ya hayo, matumizi ya msururu wa alama unajitokeza katika Kibonzo $K_1$UP katika usemi wa Rais na RO wanaonekana wakiwafokea raia na kusema;

*Yes, My Sister and The Dp's Relatives Have a Right to Government Tenders Like Any Other Kenyan.*

*Ndio, Dadangu Na Jamaa Za Naibu Wangu Wanahaki Ya Kupata Zabuni Za Serikali Kama Mkenya Yeyote Yule*

Baada ya maneno haya kuna msururu wa alama. Pamoja na hayo, RO anasawiriwa akisema;

*My Brother and My Deputy's Son Have a Right Like Any Other Kenyan to Be Nominated for Any Position.*

*Ndugu Yangu Pamoja Na Mtoto Wa Kiume Wa Naibu Wangu Wanahaki Ya Kuteuliwa Katika Nyadhifa Zozote Zile Kama Wakenya Wengine*

Baada ya maneno haya kuna msururu wa alama. Katika kibonzo hiki, msanii ametumia msururu wa alama kuwakilisha utukano. Kwa kawaida, wanavibonzo hawawezi chapisha matusi au maneno ya utukano katika vibonzo vyao na hivyo wao hutumia msururu wa alama kama njia ya kujidhibiti na kuficha yasiyoweza kutajwa hadharani. Katika kibonzo hiki, Gado alitumia alama kudhihirisha ufedhuli wa Rais na Naibu Rais pamoja na kinara wa muungano wa NASA na naibu wake KM.

Kutokana na maelezo haya, mtafiti aligundua kuwa Gado alitumia msururu wa alama katika vibonzo vyake kama njia ya kujidhibiti kutokana na kuchapisha maneno ya utukano. Ingawaje, Gado alitumia msururu wa alama kuficha utukano, alisawiri viongozi wa ngazi ya juu kama vile Rais na Naibu Rais, pamoja na vinara wa muungano wa NASA RO na KM, kama watu wafedhuli na watu wasiokuwa na maadili. Si jambo la kawaida kwa watu, kutoa cheche za matusi hadharani na watu wenye tabia ile, wanachukuliwa kuwa hawana maadili. Hivyo, msanii alipotumia msururu wa alama kuficha matusi, alilenga kukejeli tabia za viongozi hawa na hatimaye kuwatashtiti akiwa na nia ya kuwafanya wabadilike.

### 4.3.9 Matumizi ya Rangi mbalimbali

Rangi ni mojawapo wa viambajengo muhimu vya mawasiliano ya ishara. Matumizi ya rangi hutumika kama mbinu ya mawasiliano na huwa na maana matlaba kuliko tu matumizi yake katika mazingira yetu. Kwa miaka mingi, rangi mbalimbali zimetumika katika nyanja mbalimbali ikiwemo taaluma ya uchoraji ramani za nchi (Brewer, 1994). Kando na hayo, madaktari na hospitali hutumia rangi kuainisha na kutambulishwa maradhi mbalimbali au hata matukio mbalimbali katika hospitali. Kwa mfano, katika muktadha wa hospitali wanapotumia "*Code Blue*" wanamaanisha kuwa kuna tukio la dharura linalohitaji matibabu ya haraka kama vile; mshtuko wa moyo au mgonjwa anapoacha kupumua. Vilevile, mtoto anapozaliwa na ngozi ya samawati, inachukuliwa kuwa anaweza kuwa na matatizo ya moyo. Kutokana na maelezo haya, tumeona kuwa rangi mbalimbali zimetumika katika nyanja mbalimbali kumaanisha mambo tofauti tofauti.

Kwa kiwango kikubwa, asilimia kubwa ya vibonzo vya msanii katika tovuti yake ni vyeusi na vyeupe. Aidha, mtafiti aligundua kuwa kutokana na vibonzo ishirini

alivyoteua kimaksudi kwa minajili ya utafiti huu ni vitatu tu vilikuwa vimechorwa kwa rangi zinginezo. Hivyo, mtafiti alisaili kuwa kuna mambo muhimu ambayo Gado alitaka kupitisha kwa hadhira yake alipotumia rangi mbalimbali katika vibonzo hivyo vitatu. Kwa kawaida, wachora vibonzo wanapotumia rangi katika michoro yao huwa wanalenga kuhuisha wanayosawiri na kunata akili za watazamaji.

Kwa mfano, katika Kibonzo $K_3$UF msanii anatuonyesha taswira ya Rais akifungua chupa iliyoandikwa "*Land Grabbing*" na mle ndani ya chupa kunaonekana mvuke au gesi ya rangi ya kijani kibichi iliyokuwa na sura za baadhi wa viongozi wa nchi ya Kenya kama vile aliyekuwa Rais wa kwanza, wa pili na watatu wa nchi ya Kenya, Naibu Rais, watu wanaochukuliwa kuwa ni wakoloni kutokana na mwonekano wao wa uso, kiongozi wa zamani wa mkoa, na kasisi. Sura za waliotoka katika chupa zinadhihirisha hisia za kukwerwa na kukasirika. Kwenye upande wa kulia wa kibonzo hiki, Rais anaonekana ni kana kwamba ameshtuka. Matukio katika kibonzo hiki yanatuchochea kujiuliza maswali kama vile, mbona Gado akaamua kutumia mvuke wa kijani kibichi kuelezea suala la unyakuzi wa ardhi na washukiwa wake? Katika kemia, gesi inayotoa rangi ya kijani kibichi ni gesi ya klorini.

Kwa kawaida gesi hii ina harufu mbaya na inachukuliwa kuwa yenye sumu na ina mmenyuko wa hali ya juu. Hivyo, Gado ametumia ishara ya gesi ya kijani kibichi kudhihirisha kuwa waliotajwa kwenye kesi za unyakuzi wa ardhi ni watu mashuhuri waliostahili kulinda sheria na mali ya umma. Kwa hivyo, wanapotajwa kwenye kesi za unyakuzi wa ardhi ni swala ambalo lingeleta mmenyuko mkubwa na kumfanya Rais ashindwe kuchukua hatua kwani mmoja wa waliotajwa ni baba yake na wandani wake wa karibu. Hivyo, msanii alitumia rangi ya kijani kibichi kuashiria mmenyuko ambao unalinganishwa na gesi ya klorini.

Isitoshe, katika kibonzo hiki, Rais amevalia tai ya rangi nyekundu na taji la ufalme la rangi nyekundu. Rais alipochukua hatamu ya kuwa Rais wa nchi ya Kenya, mara nyingi alivalia tai nyekundu kudhihirisha mamlaka na kuwa yeye ndiye aliyekuwa kwenye upeo wa uongozi wa nchi ya Kenya. Hivyo msanii anatumia tai ya rangi nyekundu kuashiria mamlaka na uongozi. Kando na hayo, tunaposawiriwa Rais akiwa na taji la rangi nyekundu, kwa kawaida nchi ambazo zinatamalakiwa na wafalme, wafalme huvalia taji la rangi nyekundu kuashiria ufalme na mamlaka. Kinaya ni kuwa Kenya ni nchi ya kidemokrasia na viongozi huchaguliwa kupitia mchakato wa kidemokrasia wa

upigaji kura wa siri. Kwa hivyo, Gado anapomsawiri Rais akiwa na taji la ufalme huenda anadokeza kuwa Rais anatumia uhusiano wake na baba yake aliyekuwa Rais wa kwanza wa nchi ya Kenya kufanya lolote alitakalo kana kwamba Jamhuri ya Kenya ni himaya yake binafsi. Katika Kibonzo hiki, Gado anasawiri tukio la taji la Rais kutoka kichwani anapofungua chupa ile ya unyakuzi wa ardhi, kumaanisha kuwa anajaribu kujitenga na matendo ya baba yake ya unyakuzi wa ardhi.




***Kibonzo 8: K₁UWM, Kusambaratika kwa Benki ya Maadili. Kutoka (http://gadocartoons.com/morals-bank-collapse/).***

Msanii katika Kibonzo $K_1$UWM anatusawiria benki kuu ya nchi ya Kenya na mameneja walioteuliwa kusimamia shughuli za benki ile. Katika Kibonzo hiki, mameneja wa benki kuu wanaonekana wakiwa wamevalia suti za rangi mbalimbali kama vile; samawati, manjano, kijani kibichi na baadhi yao wana tai za rangi nyekundu. Isitoshe, kwenye upande wa kushoto wa meneja aliyeshika kijisanduku kilichoandikwa "*Central Bank*" kuna jengo lenye maandishi "*Moral Bank*" limeporomoka na kwenye mabaki ya jengo lile kuna gunia la pesa, mafuvu na mifupa ya watu, kuna mguu unaoonekana ukining'inia, mkono wa binadamu, gurudumu la gari, bomba la maji taka na chembechembe za damu zilizotapakaa kwenye eneo la jengo. Matukio katika kibonzo hiki yanamchochea mtafiti kujiuliza mbona msanii aliamua kutumia rangi mbalimbali kusawiri yaliyokuwa yakijitokeza katika kibonzo hiki? Pili, mbona msanii alisawiri mameneja wa benki wakiwa wamevalia suti za rangi mbalimbali.

Wanasaikolojia Tavaragi na Sushma (2016), wanadai kuwa matumizi ya rangi katika michoro, mazingira au hata mavazi yetu yanaweza kuibua maana matilaba katika akili za watazamaji. Wanaeleza kuwa matumizi ya rangi kuwakilisha jambo lililo fiche hutokana na kushirikishwa kwa rangi fulani na utamaduni, historia, dini, siasa au hata lugha ya jamii fulani. Kwa mfano, rangi nyekundu katika jamii nyingi hutumika kusimamia damu au shauku. Nchini China bendera ya wanaujamaa ilikuwa nyekundu. Kando na haya, katika jamii zingine, rangi nyekundu zilitumika kuwakilisha mamlaka. Kwa mfano, katika kanisa katoliki nchini Roma Makadinali walivalia kofia za rangi nyekundu. Isitoshe, wafalme wa himaya mbalimbali walivalia taji zilizokuwa za rangi nyekundu na hata sasa, katika sherehe mbambali waheshimiwa hutandikiwa zulia nyekundu katika hafla zao kuashiria mamlaka.

Isitoshe Tavaragi na Sushma (2016) wanaeleza kuwa rangi ya manjano inahusishwa na miale ya jua na historia ya nchi ya Meksiko, miale ya manjano ya jua iliwakilisha hekima kuu. Vilevile, Yu (2014) anaeleza kuwa rangi za kijani kibichi na samawati zinatumika kuwakilisha bahari na utulivu wake. Waidha, rangi ya samawati hutumika kuelezea mbingu na huchukuliwa kama rangi tulivu. Aghalabu, rangi hii hutumika katika sare nyingi za wafanyikazi au hata wanafunzi. Nchini Kenya polisi huvalia sare za samawati. Hivyo, rangi ya samawati hutumika kuashiria utendakazi na usadikifu. Kutokana na uelewa huu mtafiti aligundua kuwa msanii aliwasawiri mameneja wa benki wakiwa wamevalia suti za sawamati kudhihirisha kuwa ni watu wakuaminika, watendakazi na wasadikifu katika utendakazi wao. Vilevile, mmoja wa mameneja wale amevalia suti ya kijani kibichi ambayo wataalam wa saikolojia ya rangi Tavaragi na Sushma walieleza kuwa ni rangi ya uhai wa mimea.

Hivyo, rangi ya kijani kibichi ilitumika kuashiria mwamko mpya, mwanzo mpya na kukua. Kwenye upande wa kulia wa kibonzo kile, kuna meneja mmoja aliyesawiriwa akiwa amevalia suti ya rangi ya zambarau, ambayo hupatikana baada ya kuchanganya rangi nyekundu na samawati. Tangu enzi za kale, rangi ya zambarua ilitumika na wafalme pamoja na mamalkia kuashiria ufalme, kuaminika na utajiri (Yu 2014). Hivyo, msanii anapomsawiri meneja mmoja akiwa amevalia suti ya rangi ya zambarau alikuwa anamaanisha kuwa ni mtu wa kuaminika na ni tajiri hivyo hana haja ya kupora pesa za benki kuu ya nchi. Kinaya ni kuwa mameneja wa benki kuu amesawiriwa kama nguruwe, fisi na tai ambao wana sifa za ulafi na kunyapanyapa. Katika kibonzo

$K_1$UWM msanii ametumia rangi kuibua dhana ya kinaya na hatimaye kutashtiti uteuzi wa mameneja wa benki kuu ya Kenya kwa kuwa wezi.

### 4.3.10 Mwingiliano Matini

Wamitila (2003), anafafanua mwingiliano matini kama dhana inayotumiwa kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani. Kwa kifupi hapa ni pale sifa za kazi fulani zinajitokeza katika kazi nyingi. Mfano maarufu wa mwingiliano matini ni kuwepo kwa sifa zinazolandana kati ya *Utendi wa Fumo Liongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani* iliyoandikwa na Kitheka wa Mberia. Ingawaje kazi hizi mbili za kisanaa ziko kwenye tanzu tofauti za fasihi, kuna mfanano mkubwa kati ya msuko, maudhui na wahusika wa Utendi wa Fumo Liyongo na Kifo Kisimani. Kazi hizi mbili zilihusu vijana barobaro waliokuwa na ari ya kukomboa jamii zao kutoka kwa uongozi wa kufinyiliwa. Kutokana na uelewa huu, mtafiti alikumbana na mifano ifuatayo ya mwingiliano matini katika vibonzo vya Gado.





K***ibonzo 14: $K_3$UF Majini yametoka kwenye chupa #Unyakuzi wa Ardhi. (www.gadocartoons.com).***

Msanii Gado ametumia mwingiliano matini katika Kibonzo $K_3$UF ambapo tunaonyeshwa taswira ya Rais akifungua chupa yenye maandishi; *Land Grabbing* ndani ya chupa tunaona gesi ya kijani kibichi iliyo na nyuso za viongozi mbalimbali ikitoka mle ndani. Kwenye upande wa juu wa kibonzo kile kuna anwani iliyoandikwa "*The Genies are out of the Bottle"*. Matukio katika kibonzo hiki yanalingana na matukio katika hadithi ya watoto ya *"Alladin and the Magic Lamp"*. Hadithi hii ilitokana na

mkusanyiko wa hadithi za *"Arabian Nights"* iliyohusu hadithi na hekaya za maliwazo na mazingombwe zilizopokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine katika nchi za Uarabuni.

Hadithi ya "*Alladin and the Magic Lamp*" ilitafsiriwa na Antoine Galland (1740) and kumekuwa na toleo nyingi na tafsiri mbalimbali za hadithi hii. Kwa minajili ya utafiti huu, mtafiti alijikita katika tafsiri ya Vohra (2018). Hadithi yenyewe inahusu mhusika Alladin, aliyezaliwa katika familia ya umaskini. Baada ya baba yake Alladin kuaga dunia, mchawi mmoja wa eneo lao alitembelea familia ya Alladin na kuwadanganya kuwa yeye ni mjomba wake Alladin na kuwa walikuwa wamekubaliana na baba yake Alladin kuwa ile siku angeaga dunia alipaswa achukue jukumu la kusaidia Alladin na mama yake. Mchawi yule aliwaeleza kuwa alijua mahali ambapo Alladin angepata utajiri ambao ungewasaidia na hivyo wakafunga safari kwenda kutafuta utajiri huo. Walifika jangwani na wakaingia kwenye pango. Mchawi aliyekuwa anajifanya mjomba wake Alladin alifanya mazingaombwe yake na kukatokea ngazi ambayo ingemsaidia Alladin kuingia mle pangoni.


Alladin alikuwa achukue chupa mle pangoni kisha amletee mjomba wake. Alladin alipata chupa ile na akaanza safari ya kupanda ngazi ndiposa atoke pangoni. Kulitokea mtetemeko wa ardhi na kuta za pango lile zikaanza kuporomoka. Mjomba wa Alladin akamhimiza Alladin amtupie chupa ile ya mazingaombwe na kisha atamtoa mle pangoni, lakini Alladin aliingiwa na wasiwasi na kukataa kutupa chupa ile. Hatimaye, Alladin aliporomokewa na pango lile na akawa amekwama mle ndani kwa siku mbili. Siku ya pili, akipapasa chupa ile huku akitamani kama angeweza kupata njia ya kutoka mle pangoni na ghafla kukatokea jini kutoka kwa chupa ile. Jini lile liliahidi kumtimizia Alladin ahadi zake na baadaye Alladin alitumia nguvu za jini lile kutoka pangoni na hatimaye kumuoa binti ya mfalme. Ingawaje msanii ametumia hadithi ya "*Alladin and the Magic Lamp*" kuelezea suala la unyakuzi wa ardhi nchini Kenya, kinaya ni kuwa jini lililotoka kwenye chupa ya Rais halikumletea baraka na mazuri kwa kuwa waliotuhumiwa kwa madai ya unyakuzi wa ardhi nchini Kenya ni wandani na watu wa karibu na Rais. Hivyo, msanii alitumia mbinu ya mwingiliano matini kuibua dhana ya kinaya na hatimaye kumtashtiti Rais na viongozi mbalimbali.




***Kibonzo 15: $K_4$UO kinyang'anyiro cha ugavana katika Kaunti ya Nairobi. Kutoka (http://gadocartoons.com/nairobi-gubernotorious-race/).***

Kando na hayo, mbinu ya mwingiliano matini inajitokeza katika Kibonzo $K_4$UO pale ambapo msanii amemsawiri mmoja wa wagombeaji wa kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi akiwa na pua ndefu. Kwa kawaida, inachukuliwa kuwa mtu mwongo anasemekana kuwa ana pua refu ama husawiriwa akiwa na pua lilio refu kuliko kawaida. Wazo hili lilitokana na riwaya ya watoto; "*Adventures of Pinocchio*" iliyochapishwa nchini Italia na Carlo Collodi katika mwaka wa 2005. Hadithi hii ya Pinocchio ilihusu mwanamme mmoja maskini aliyetaka kijichongea kikaragosi cha mbao ili aweze kupata mtaji wake kutokana na kikaragosi kile.

Inasemekana kuwa ubao aliotumiwa kuchongea kikaragosi kile haukuwa wa kawaida na ulikuwa wa kimaajabu. Baada ya kikaragosi kile kuchongwa kilitamani kuwa mvulana halisi aliye hai. Hatimaye, ndoto ya kikaragosi kile ilitimia na akawa hai. Lakini kwa kuwa kilikuwa kimeundwa kwa ubao wa kimaajabu kila kiliponena uongo pua lake lilirefuka. Hatimaye, kutokana na hadithi ile ya Pinocchio, watu walianza kuhusisha mtu mwongo na pua refu. Hivyo, msanii alitumia hadithi ya Pinocchio kuelezea kuwa mgombeaji mmoja wa kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi alikuwa ni mtu mwongo




***Kibonzo 16: K5UO Kura za Walio wengi dhidi ya Kura za walioteuliwa. Kutoka (<u>www.gadocartoon.com</u>).***

Vilevile, msanii alitumia mwingiliano matini kuibua tashtiti kama ilivyodhihirika katika Kibonzo K5UO. Katika kibonzo hiki, msanii anatusawiria kinara wa muungano wa NASA RO akiwa amevalia gauni la zambarau la kifalme lilioshikiliwa na watu wanaonekana wakimfuata na wengine wanamcheka. Upande wa chini wa kibonzo kuna picha ya Rais akiwa amevalia gauni la kifalme la rangi nyekundu na limeshikiliwa na wanajeshi. Jambo la kushangaza ni kuwa viongozi hawa wawili wamesawiriwa wakiwa uchi na hasa sehemu zao za mbele zimesawiriwa zikiwa uchi.

Mtafiti alilinganisha usawiri huu na hadithi ya watoto "The Emperor's New Clothes" iliyoandikwa na Hans Christian Andersen kutoka Denmaki. Hadithi ile ilihusu mfalme mkuu aliyependa kuvalia nguo za dhamana na zilizopendeza. Ilisemekana kuwa alikuwa na nguo ya kila wakati wa siku. Siku moja kukaja wezi wawili katika himaya yake na wakamweleza mfalme mkuu kuwa walikuwa na uwezo wa kumtengenezea nguo ambayo ni wajinga tu hawangeweza kuiona. Mfalme Mkuu alifurahishwa na wazo la nguo ile na akaagiza atengenezewe nguo ile kwa minajili ya kutambua watu werevu katika himaya yake. Wezi wale waliwahadaa watu wote katika himaya ile kuwa wametengeneza nguo nzuri na wakajifanya kumvalisha mfalme nguo ile, ingawaje hakukuwa na nguo. Kwa kuwa watu walihofia kutambulika kama wajinga hakuna aliyethubuti kumweleza mfalme mkuu kuwa alikuwa uchi isipokuwa kijana mmoja mchanga aliye pasa sauti na kusema;

> *But the King is Naked*
> *Lakini Mfalme ako Uchi*.

Hadithi hii ya Hans Christian ililenga kusuta watu waliopenda kusifu viongozi hata wakati wanapoona viongozi wanafanya mambo yasiyostahili. Matukio katika hadithi ya “The Emperor’s New Clothes” yanalingana na matukio yaliyosawiriwa na msanii katika Kibonzo K5UO. Katika nchi ya Kenya, wafuasi wa RO husemekana kuwa watafuata kiongozi wao hadi kwenye mwisho wa jabali bila kumkosoa au kwenda kinyume na mawazo yake. Kwa upande wa pili, wanajeshi wanaonekana kumfuata Rais aliye uchi kumaanisha kuwa, wanajeshi hawa watatekeleza amri za Rais bila kumkosoa au kuona ubaya wa matendo yake. Hivyo, msanii alitumia mbinu ya mwingilianomatini kutashtiti hali ya wananchi kuwafuata viongozi wao bila kufikiria wala kuhakiki matendo yao.

### 4.3.11 Hitimisho

Katika sehemu hii, mtafiti alichambua vibonzo alivyoteua kwa minajili ya kupata mikakati ya kitashtiti iliyotumiwa na msanii Gado. Kutoka na ufafanuzi uliotolewa, msanii ameweza kuthibitisha kuwa tashtiti hutegemea mbinu za kisanaa kama vile; kejeli, kinaya, analojia, metonimia, sitiara, matumizi ya rangi na ukaragosi, si kuibua tashtiti tu lakini kupitisha ujumbe fulani unaolenga kuchochea na kuwazindua watazamaji. Lengo kuu la tashtiti si kukebehi wahusika wanaotashtitiwa lakini pia hujaribu kuchochea na kuzindua hadhira kutokana na maovu yanayotendeka miongoni mwao ili kuleta mabadiliko.

# SURA YA TANO

# MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alishughulikia mahitimisho ya utafiti kwa jumla, matokeo ya utafiti ambayo yalipangwa kulingana na madhumuni ya utafiti na mapendekezo kwa tafiti zijazo. Sehemu hizi tatu ziliangaziwa mintarafu ya uchambuzi wa vibonzo ishirini vilivyopakuliwa kutoka kwenye tovuti ya Gado.

## 5.2 Mahitimisho ya Tasnifu

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa mikakati ya kitashtiti katika vibonzo vya Gado vilivyochapishwa katika tovuti yake ya www.gadocartoons.com. Mada ya utafiti huu ililenga kuweka wazi pengo la kiusomi ambalo mtafiti alinuia kuziba. Kwa kawaida vibonzo vinavyochapishwa katika vyombo vya habari kama vile magazeti au hata televisheni huwa vimepitiwa na wahariri na aghalabu huwa vimedhibitiwa ili visikiuke sheria zilizowekwa na vyumba mbalimbali vya habari. Hata hivyo, hali hii huwa tofauti kwa upande wa mtandao na hasa wakati ambapo msanii anatumia tovuti yake binafsi kuchapisha vibonzo vyake. Hivyo, mtafiti alilenga kuthibitisha kuwa vibonzo vinavyochapishwa kwenye mtandao huwa na uhuru wa kusawiri matukio kama yalivyo ama jinsi msanii anavyotaka na huenda vikawa na ukali mwingi. Mtafiti alichambua vibonzo ishirini alivyoteua kimaksudi kwa minajili ya kutambua mbinu za kitashtiti zilizotumiwa na Gado ili kuvifanya kuwa vya kitashtiti na hatimaye kuvifanya viwe na ukali katika usawiri wake.

Mapitio ya maandishi yaligawanywa katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza yalimsaidia mtafiti katika kutambulisha maudhui yanayojitokeza katika vibonzo vya kisiasa. Katika sehemu hii mtafiti aligundua kuwa maudhui yanayojitokeza katika kazi yoyote ile ya kisiasa hutokana na mazingira ya kisiasa ya nchi fulani na kipindi cha kisiasa kinachosheheniwa na kazi ile. Hata hivyo, maudhui tawala katika vibonzo vya kisiasa hulenga kuweka wazi maovu na uozo unaotendeka katika nchi fulani katika kipindi kile.

Kama ilivyoelezwa awali katika sehemu hii ya mapitio ya maandishi vibonzo vya kisiasa huwa vimefungamana na maoni ya anayevichora na msanii aliyebobea ni yule anayeweza kuoanisha sanaa anayoifanya na maoni au mawazo yake kwa kiwango kikubwa. Zaidi ya hayo, vibonzo vya kisiasa aghalabu huwa vyenye hisia hasi, ubeuzi

na vyenye kuhakiki. Kulingana na maandishi yaliyopitiwa katika sehemu hii, maudhui yaliyosheheni vibonzo vya kisiasa ni kama vile; ufisadi, ulaghai, upendeleo, ukosefu wa usalama, na wizi.

Sehemu ya pili ya mapitio ya maandishi ilimsaidia mtafiti katika kutambua mikakati inayoendeleza maudhui ya kitashtiti na inayoibua tashtiti katika kazi yoyote ya kisanaa. Kutokana na mapitio ya tafiti zingine, mtafiti aligundua kuwa tashtiti hutegemea fani zingine za lugha ili iweze kujitokeza. Kwa mfano, kutokana na utafiti wa Eko (2007), mtafiti aligundua kuwa visasili vinaweza kutumika kuibua tashtiti au kuendeleza maudhui ya kitashtiti. Kando na hayo, mtafiti aligundua kuwa hata vihisishi vinaweza kutumiwa kuibua tashtiti pamoja na fani za lugha kama vile, kinaya, kejeli, sitiara, mwingiliano matini, metonimia, na hata analojia. Fauka ya hayo, ishara za kuonekana kama vile; matumizi ya rangi, alama kama vile nyota, alama za reli pia zinawezatumiwa kuibua tashtiti katika vibonzo vya kisiasa.

Kwa minajili ya kupata data ya utafiti huu, mtafiti alidurusu tovuti ya gadocartoons.com na kupakua vibonzo sitini vilivyokuwa vimechapishwa katika mwaka wa 2017. Kutokana na kundi jumla la vibonzo sitini, mtafiti aliteua kimaksudi vibonzo ishirini ambavyo alichambua mintarafu ya nadharia iliyokuwa ikiongoza utafiti huu pamoja na madhumuni ya utafiti wenye. Baadaye alivipanga vibonzo vile kulingana na maudhui yaliyojitokeza na akavitafsiri, na kuvikodi kama alivyoeleza katika sura ya nne. Hatua ya kuchanganua maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa ilifanywa kwa kuchambua yaliyomo katika vibonzo vyenyewe na kisha maelezo yakatolewa kulingana na vibonzo vilivyopangwa.

Baada ya kutambua na kuchanganua maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa, mtafiti aliangalia, matumizi ya lugha na ishara zilizokuwa katika vibonzo vile kwa minajili ya kuchanganua mikakati ya kitashtiti iliyoendeleza maudhui yaliyotambuliwa. Baada ya hatua hiyo, mtafiti aliwasilisha matokeo ya uchanganuzi wake kwa njia ya maelezo chini ya mada ya mikakati ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa. Kwa jumla, utafiti huu ulithibitisha kuwa vibonzo vinavyochapishwa kwenye mtandao huwa na uhuru mwingi wa usawiri wa mambo unaoleta ukali mwingi ikilinganishwa na vibonzo vinavyochapishwa kwenye magazeti. Kando na hayo, mtafiti aligundua kuwa msanii Gado alitumia mikakati kama vile, matumizi ya kinaya, kejeli, sitiara, analojia, mwingiliano matini, matumizi ya rangi, alama na vipovu vya

sauti, kuendeleza maudhui ya kitashtiti kama vile ufisadi, ulaghai, upendeleo na hata unafiki.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Baada ya kuchambua na kuchanganua vibonzo vya kisiasa vilivyoteuliwa, mtafiti aligundua kuwa maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa yalikuwa ya kitashtiti na yalikuwa kama vile; uongozi, unyanyasaji wa wafanyikazi, ulaghai katika siasa, ufisadi, ukosefu wa maadili, upendeleo na unafiki. Maudhui haya yalinuia kufichua uozo uliokuwa ukitendeka nchini Kenya kupitia serikali ya wakati huo. Kama ilivyoelezwa awali, maudhui husheheni yale yanayotokea katika jamii fulani na katika kipindi fulani. Hivyo, maudhui yaliyojitokeza katika uchunguzi huu yalilenga kuweka wazi yaliyokuwa yanatokea katika mwaka wa 2017 nchini Kenya.

Kando na hayo, utafiti huu uligundua kuwa msanii alitumia mitindo mbalimbali ya lugha na ishara kama mbinu za kitashtiti kwa minajili ya kuvifanya vibonzo vyenyewe kuwa vya kitashtiti. Kama ilivyotajwa katika mapitio ya maandishi kuwa tashtiti hutegemea fani na mbinu mbalimbali za lugha pamoja na ishara ili iweze kujitokeza na kufanya kazi yake ya kushambulia wahusika kwa minajili ya kuchochea mabadiliko au kuzindua hadhira ya kazi ile ya kitashtiti. Kutokana na matokeo ya uchunguzi huu, mtafiti aligundua kuwa msanii alitumia fani kama vile; kejeli, kinaya sitiara, metonimia, analojia na mwingiliano matini kuibua tashtiti katika vibonzo vyake.

#### 5.3.1 Uchanganuzi wa Maudhui ya Kitashtiti

Katika sehemu hii, mtafiti alitambua na kuchanganua maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa. Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti alikumbana na maudhui yaliyohusu uongozi wa nchi ya Kenya chini ya Rais na Naibu Rais na yaliyokuwa yakiendelea katika mwaka wa 2017, ambapo nchi ya Kenya ilikuwa kwenye harakati ya kujiandaa kwa uchaguzi mkuu. Katika uchambuzi wa maudhui, mtafiti aligundua kuwa msanii aliwasawiri Rais na Naibu Rais kama watu wasiowajali wananchi kama ilivyothibitika katika Kibonzo K1UO ambapo msanii anawasawiri viongozi hawa wakipuuza matakwa ya wananchi na kuwapa ahadi za uongo ambazo hawawezi kutimiza. Kupitia usawiri huu, mtafiti aligundua kuwa Gado alikuwa anawatashtiti na kuwakejeli Rais na Naibu Rais kwa uongozi wao mbaya. Zaidi ya hayo, mtafiti alitusawiria Rais na Naibu Rais kama viongozi wanaowanyanyasa wafanyikazi wao kama ilivyothibitika katika Kibonzo K2UWW. Katika Kibonzo hiki, msanii alimsawiri

Rais akimchapa daktari aliyesawiriwa kama mwanamke. Kutokana na usawiri huu, Gado alikuwa anatufichulia picha ya kiongozi asiyejali mwananchi wa kawaida pamoja na wafanyikazi wake. Hali ya kuwasawiri madaktari kama mwanamke aliye kuwa katika ndoa ya manyanyaso, ililenga kuonyesha jinsi uhusiano kati ya madaktari na serikali ya Rais na Naibu Rais ulivyokuwa. Pia, kibonzo kile kilikuwa na ukali mwingi katika usawiri wake, kwa kutusawiri Rais kama kiongozi anayewanyanyasa wanyonge na mwenye kukiuka maadili.

Zaidi ya hayo, vibonzo vilivyoteuliwa pia vilisawiri maudhui ya ufisadi kama ilivyothibitishwa katika vibonzo K1UF, K2UF K3UF NA K4UF ambapo msanii amedokeza kuwa uongozi chini ya mfumo wa ugatuzi umekuwa na ufisadi mwingi, wafanyikazi wa serikali ni wafisadi na marais waliokuwepo hapo awali waliokuwa ni wafisadi na hasa wezi wa ardhi za umma. Isitoshe katika K4UF, msanii amewasawiri Rais na Naibu Rais wakibeba kasha la pesa kumaanisha kuwa viongozi hawa wawili wamekuwa wakipora mali ya wananchi. Kwa mujibu wa vibonzo hivi, msanii alikuwa akiweka wazi na kwa njia ya moja kwa moja kuwa Rais na Naibu Rais pamoja na viongozi waliokuwa kwenye serikali ya mwaka wa 2017 na hapo awali ni wafisadi. Usawiri huu wa viongozi hawa ulinuia kuwatashtiti ili kuzua mabadiliko katika mawazo ya wananchi kuhusiana na viongozi wanaowachagua na pia kuwa kukejeli viongozi waliosawiriwa ili waweze kubadilika.

Katika uchambuzi wa maudhui ya kitashtiti, mtafiti aligundua kuwa msanii alisawiri viongozi waliokuwepo katika mwaka wa 2017 kama walaghai kama ilivyothihirika katika vibonzo K1UKS, K3UKS, wasiokuwa na maadili kama ilivyotambulika katika vibonzo K2UWW na K3UWW na wenye mapendeleo (K1UP). Msanii aliibua maudhui haya kwa njia ya moja kwa moja bila kuficha chochote na kwa njia iliyodhibitisha ukali ili kuibua tashtiti katika vibonzo vyake. Kama ilivyoelezwa awali tashtiti ni taalamu ambayo huchochea mabadiliko katika mfumo wa kijamii na kisiasa kwa njia ya kimzaha. Hivyo, msanii alipowaangazia Rais na Naibu Rais wakienda haja ndogo kwenye kaburi au alipowasawiri Rais na Ro wakiwa uchi alikuwa anajaribu kuhakiki siasa za nchi ya Kenya kwa njia ya mzaha akiwa na lengo la kufichua upumbavu, unafiki na masuala ya kipuzi miongoni mwa viongozi, serikali au taasisi za kiserikali. Hivyo, tunaweza kusema kuwa msanii aliangazia mambo kwa njia iliyo wazi kwa kiasi cha kumsawiri Rais na Naibu Rais kama wezi, RO na Rais wakiwa uchi, na Naibu Rais

kama mnafiki. Kwa kifupi, mtafiti alitumia mtandao wake kufichua uozo uliokuwepo katika serikali ya mwaka wa 2017, pamoja na taasisi za kiserikali. Kutokana na uchambuzi wa maudhui yaliyojitokeza, mtafiti aligundua kuwa Gado aliweza kusawiri mambo yaliyotendeka nchini Kenya kwa njia ya wazi, bila kuficha chochote na kwa kiasi kikubwa usawiri wake uliokuwa na uhuru mwingi wa kujieleza ikilinganishwa na vibonzo vinavyochorwa kwenye magazeti.

### 5.3.2 Uhakiki wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Gado

Kama ilivyoelezwa awali, tashtiti haiwezi kufaulu kivyake na aghalabu hutegemea na hutumia mbinu zingine za lugha ili iweze kutambulika. Kwa mujibu wa Knight (2004), tashtiti husawiri "ushambulizi wa ainasafu" ambapo mara nyingi huwa inafaulu kwa kujifanya kuwa kitu kingine. Stinson (2019) anatilia mkazo mawazo ya Knight kwa kudai kuwa ni vigumu kufafanua tashtiti kwa uhakika na kwa kikamilifu, kwa kuwa kumekuwa na vuta nikuvute kuhusiana na ufafanuzi wa tashtiti. Hata hivyo, wataalamu wengi wamekubaliana kuwa tashtiti ni mtindo wala sio utanzu wa fasihi. Katika hali hii, tashtiti huchukuliwa kuwa kimelea. Kutokana na maelezo haya, mtafiti aligundua kuwa tashtiti hutumia mbinu za lugha pamoja na ishara tofuati ili iwezi kujitokeza. Kwa mfano; msanii alitumia mbinu ya ukaragosi kwa minajili ya kuibua tashtiti na pia kudokezea hadhira yake kuhusu anachozungumzia ama anayesawiriwa. Katika uchunguzi huu, mtafiti alitumia neno ukaragosi kumaanisha mbinu yenyewe ya usawiri wa sifa bainifu za mtu fulani zilizopigwa chuku.

Waaidha, msanii alitumia mbinu za lugha kama vile; kejeli, sitiara, kinaya, analojia, mwilingiliano matini kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vyake. Kama ilivyokuwa imeelezwa awali, kazi ya tashtiti ni ushambulizi wa wahusika, unaolenga kuleta mabadiliko katika tabia. Hivyo, msanii Gado alikejeli na kukehebi tabia za viongozi waliosawiri katika vibonzo vilivyoteuliwa kwa minajili ya kuleta mabadiliko na kuweka wazi maovu waliokuwa wakitenda Licha ya hayo, uchambuzi na uhakiki wa vibonzo vilivyoteuliwa ulithibitisha kuwa matumizi ya rangi, msururu wa alama kama vile heshtegi, nyota na mviringo, mentonimia, zinaweza kutumika kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vya kisiasa.

Hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa msanii Gado alisawiri viongozi wa nchi ya Kenya kama wafisadi, wanafiki, wenye kukosa maadili na wenye mapendeleo. Sababu kuu ya Gado kuwasawiriwa kwa njia hii ilikuwa ni kuwatashtiti

na kuzindua hadhira yake kuhusiana na maovu yaliyokuwa yakiendelea nchini Kenya katika kipindi kile. Pamoja na hayo, msanii alifaulu kwa kutumia mbinu mbalimbali za lugha na ishara mbalimbali kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vyake. Isitoshe, mtafiti aligundua kuwa usawiri wa Gado uliosheheni uhuru mwingi wa kujieleza na hakuogopa kuweka wazi maoni yake kuhusiana na kiongozi fulani au suala fulani. Hivyo, sanaa ya Gado ilionyesha ukali na uhuru mwingi katika uangaziaji wa masuala mbalimbali, hali ambayo ni tofauti na vibonzo vinavyochorwa kwenye magazeti ambayo huwa yanafuata sheria fulani za usawiri. Hivyo, utafiti huu ulidhihirisha kuwa uhamiaji wa vibonzo vya kisiasa kutoka magazetini hadi kwenye mitandao ya kibinafsi, ulipelekea kuongezeka kwa makali na uhuru katika usawiri wake. Isitoshe, uhuru na ukali huu ulijitokeza zaidi kutokana na utumizi wa mikakati ya kitashtiti kama vile; ukaragosi, kinaya, kejeli, sitiara, analojia, metonimia, mwingiliano matini, matumizi ya rangi na matumizi ya anwani, vipovu vya sauti na kutaja.

## 5.4 Mapendekezo

Mapendekezo yaliyotolewa katika utafiti huu, yalilenga kuwasaidia watafiti wengine wanaonuia kubobea katika uchunguzi wa masuala ya vibonzo vya kisiasa na tashtiti. Isitoshe, mapendekezo haya yanaweza kutumiwa na wataalam wa mawasiliano ya kisiasa, ambao kazi yao kuu ni kutunza na kukuza. Kwanza kabisa, mtafiti anapendekeza kuwa uchunguzi kuhusu jinsi vibonzo vya kisiasa huunda maoni ya wananchi kuhusiana na wanasiasa ufanywe. Pili, mtafiti anapendekeza uchunguzi zaidi ufanywe kuhusu uhuru unaotokana na uchapishaji wa matini katika mitandao na ikiwa kuna haja ya kuwepo na kanuni za kuongoza uchapishaji wa matini. Hatimaye, mtafiti anapendekeza kuwa watafiti wa baadaye, wanaweza kuchunguza ikiwa hali ya kutashtiti viongozi na taasisi za uongozi huleta mabadiliko yoyote yanayotarajiwa na anayetoa tashtiti zile.

## MAREJELEO


Adejuwon, A., and S. Alimi. 2011. "*Cartoons as Illustration: Political Process in Nigeria*." The Journal of Pan African Studies 4 (3): 57–76.

Afp. (2020, June 28). Dead voters and other ways to steal a Kenyan election. *Nation*., from https://nation.africa/kenya/news/dead-voters-and-other-ways-to-steal-a-kenyan-election-432276

Akande, O. (2002). *A Semiotic Analysis of Political Cartoons: A case study of Nigeria.*, University of Oklahoma, Oklahoma.

Al-Momani, K., Badarneh, M. A., & Migdadi, F. (2017). A semiotic analysis of political cartoons in Jordan in light of the Arab Spring. *HUMOR*, *30*(1). https://doi.org/10.1515/humor-2016-0033

Andersen H. C. (2020). *The emperor's new clothes*. SAGA Egmont. http://brossard.pretnumerique.ca/isbn/9788726418088.

Baloyi, L., & Rabothata, M. M.-. (2014). Toward sustainable development through nurturing diversity: Proceedings from the 21st International Congress of the International Association for Cross-Cultural Psychology. In *The African Conception of Death: A Cultural Implication* (pp. 232–242). Retrieved from https://scholarworks.gvsu.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1018&context=iaccp_papers.

Barasa la Kiswahili la Zanzibar. (2010). *Kamusi La kiswahili fasaha*. Oxford University Press.

BBC. (2013, May 14). *Kenya's Nairobi City hit by pig protest over mps pay*. BBC News. https://www.bbc.com/news/world-africa-22522846

Biedermann, H. (1994). *Dictionary of symbolism: Cultural icons and the meanings behind them*. Meridan Book.

Brewer, C. A. (1994). Color use guidelines for mapping. *Visualization in modern cartography*, *1994*(123-148), 7

Chandler, D. (2002) *Semiotics for Beginners.* Aberystwyth: Aberystwyth University.

Chonka, P. (2016). *Cartoons in conflict: Amin Arts and transnational geopolitical imagination in the Somali-language public sphere*. Critical African Studies, *9*(3), 350-376. https://doi.org/10.1080/21681392.2016.1228074

Collodi C. & Innocenti R. (2005). *The adventures of pinocchio* (1st ed.). Creative Editions.

Conners, L. J. (2005). Visual Representations of the 2004 Presidential Campaign: political cartoons and Popular Culture References. *American Behavioral Scientist, 49* 49(3), 487-497.

Das, A. K. (2019). Caricatures as a Medium of Communication [Reviewof *Caricatures as a Medium of Communication*]. *Interdisciplinary Journal of Contemporary Research*, *vol 6*(1), 7–13. Research Gate. https://www.researchgate.net/publication/333972139_Caricatures_as_A_Medium_of_Communication

Declercq, D. (2018). A definition of satire (and why a definition matters). *The Journal of Aesthetics and Art Criticism*, *76*(3), 319–330. https://doi.org/10.1111/jaac.12563

Dörner, A., & Porzelt, B. (2016). Politisches Gelächter. Rahmen, Rahmungen und Rollen bei Auftritten politischer Akteure in satirischen Interviews des deutschen Fernsehens. *M&K Medien & Kommunikationswissenschaft*, *64*(3), 339-358.

DeSousa, M. A., & Medhurst, M. J. (1982). Political cartoons and American culture: Significant symbols of campaign 1980*. *Studies in Visual Communication*, *8*(1), 84–98. https://doi.org/10.1111/j.2326-8492.1982.tb00061.x.

Dugalich, N. (2018). Political cartoon as a genre of political discourse. *RUDN Journal of Language Studies Semiotics and Semantics*, *9*(1), 158–172. https://doi.org/10.22363/2313-2299-2018-9-1-158-172

Eko, L. (2007). It's a political jungle out there. *International Communication Gazette*, *69*(3), 219–238. https://doi.org/10.1177/1748048507076577.

Eko, L. (2015). The art of satirical deterritorialization: Shifting cartoons from real space to cyberspace in Sub-Saharan africa. *International Communication Gazette*, *77*(3), 248–266. https://doi.org/10.1177/1748048514568759

El Refaie, E. (2009a). Metaphor in political cartoons: Exploring audience responses, in C. Forceville and E. Urios-Aparisi (Eds.), *Multimodal Metaphor*, Berlin: Mouton de Gruyter.

El Refaie, E. (2009). Multiliteracies: How readers interpret political cartoons. *Visual Communication*, *8*(2), 181–205. https://doi.org/10.1177/1470357209102113

Eko, L (2010) The Art of Criticism: How African Cartoons Discursively Constructed

African Media Realities in the Post-Cold War Era, Critical African Studies, 2:4, 65-91,

Friedrich Ebert Stiftung. (2000). *Mtalaa wa elimu ya uongozi wa vyama vya wafanyikazi Tanzania* (pp. 5-10).

Gathara, P. (2019, July 2). *The death of the political cartoon*. Censorship | Al Jazeera. https://www.aljazeera.com/opinions/2019/7/2/the-death-of-the-political-cartoon

Gray, J., Jones, J. P., & Thompson, E. (2009). *Satire TV: politics and comedy in the post-network era*. Nyu Press.

Grynberg, R., & Singogo, F. (2021). An Anatomy of Grand Fraud: The Goldenberg Scandal and the IMF/World Bank. *Public Policy and Administration Research, 10*(2), 17–32. https://doi.org/10.1007/978-3-030-65995-0_9

Hamukwaya, L., &Kangira, J. (2017). *Satire as a Tool for Socio-political Commentary: A Case of the Ramblers' selected Articles in the Namibia Newspaper 2015*. International Journal of English Language, Literature in Humanities, vol V(Vi), 339-402. doi: 316656186

Hess, S., S. Northrop. 2011. *American Political Cartoons: The Evolution of National Identity, 1754-2010*. New Brunswick: Transaction Publishers.

*Highet, G. (2015). Anatomy of Satire. United States: Princeton University Press*

Holsteyn, J. (2017). Rude by Nature? The impact of political cartoons on perceived images of politicians. In *Political Incivility in Parliament, Party Competition and Political Competition* (pp. 1-23). Nottingham: ECPR Joint Sessions of Workshops.

Kessler, M. (2022). Multimodality. *ELT Journal*, *76*(4), 551–554. https://doi.org/10.1093/elt/ccac028

Kimani, H. (2006). Uwiano wa Picha na Matini katika mabango ya Matangazo ya Ukimwi: Mtazamo wa Kisemiotiki (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Knight, C. A. (2004). *The Literature of Satire*. Cambridge: Cambridge University Press.

Kondowe, W., Fishani Ngwira, F., & Madula, P. (2014). *Linguistic Analysis of Malawi Political Newspaper Cartoonson President Joyce Banda: Towards Grice's Conversational Implicature*. International Journal of Humanities and Social Science, *4*(7), 40-51. Retrieved 24 August 2020.

Kothari, C. R. (2004), *Research Methodology: Methods and Techniques,* second revised edition, New Delhi: New Age International (P) Ltd, Publishers

Kress, G. (2004) Reading images: Multimodality, representation and new media *. Information Design Journal, 12* (2): 110-110.

Kress, G., Jewitt, C. Ogborn, J. & Tsatsarelis, C. (2001). *Multimodal teaching and learning. The rhetorics of the science classroom* London: Continuum.

Kress, G., & van Leeuwen, T. (2001). Multimodal discourse: The modes and the media of contemporary communications. NY: Oxford University Press

KTN HOME. (2016). *RUTO TO WAIGURU: "….don't give us catwalks…you presided over theft…"*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=Ei0gl4qPiqI

LeBoeuf, M. (2007). *The Power of Ridicule: An Analysis of Satire*. Senior Honors Projects. http://digitalcommons.uri.edu/srhonorsprog/63http://digitalcommons.uri.edu/srhonors prog/63

Longhorn Publishers. (2011). *Kamusi ya karne ya 21*.

Macharia, D. Incongruity-Resolution Mechanisms and Context in Unintentional Humour: A Linguistic Landscape Analysis of Translation Errors on Public Notices in Kenya (Ph. D). Laikipia University.

Magigi, W. (2012). *Methodology Tool for Researching and Scientific Writing in Emerging Economies*. Dar es Salaam. Thrust Publication Limited

Maina, R. (2012). *Mbinu za Mawasiliano Katika Matangazo ya Runinga Nchini Kenya* (Masters). Kenyatta University.

Marikio Muchiri. (2017, March 9). *Shock as Uhuru calls politician 'Shetani Mshenzi' in public [video]*. Kenyans.co.ke. from http://www.Kenyans.co.ke/news/president-Uhuru-Kenyatta-bitter-exchange-words-turkana-governor-josphat-nanok-17370

Massamba David, P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Tuki.

Medhurst, M. J., & DeSousa, M. A. (1982). The editorial cartoon as visual rhetoric: Re-thinking boss tweed. Journal of Visual Verbal Language, *2*, 43-52. 96

Meyer, J.C. (2000). Humor as a double-edged sword: Four functions of humor in communication. *Communication Theory 10*(3): 310–31.

Mdee, J. & Massamba, D., 2006. *TUKI English-Swahili dictionary*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.

Massamba David, P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Tuki.

Michira, M. (2013, September 6). *Kidero slaps Shebesh, then quickly forgets*. The Standard; Standard Digital. https://www.standardmedia.co.ke/article/2000092952/governor-evans-kidero-slaps-rachel-shebesh-then-quickly-forgets#google_vignette

Miricho M. (2021). *Ukiushi wa Kanuni Katika Hadithi Teule za Watoto za John Kobia na Wadi Wamitila.* (Tansifu ya Uzamili).

Muchiri, M. (2017, March 9). *President Uhuru Kenyatta in Bitter Exchange of Words with Turkana Governor Josphat Nanok*. Kenyans.co.ke. Retrieved from www.Kenyans.co.ke

Mulanda, O., & Khasandi-Telewa, V. (2014). *In the Cartoonist's Mind: Exploring Political Comic Strips in Kenyan Daily Newspapers.* The Journal of Pan African Studies, *6*(9), 30-41. Retrieved 24 August 2020.

Najjar, O. (2007). *Cartoons as a Site for the Construction of Palestinian Refugee Identity* Journal of Communication Inquiry, 31(3), 255(1)

Nauta, D. Jr. (1972). *The Meaning of Information*. The Haque: Mouton:

Newsome, B. (2015). *An introduction to research, analysis, and writing: Practical skills for social science students*. Sage Publications.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkumbo, D. (2019) *Uchanganuzi wa Matangazo ya Ngono Salama Katika Mtandao wa Durex Facebook Page Kenya*. thesis.

Onakpa, M. (2014). Cartoons, cartoonists and effective communication in the Nigeria Print Media. *African Research Review*, *8*(1), 32. https://doi.org/10.4314/afrrev.v8i1.3.

Otumwa, D. (2019). Mitindo na Maudhui katika Uchanganuzi wa Vibonzo kwenye Gazeti la Taifa Leo (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Oz, S. (2014). *The Construction of "the Turk" and Entextualization of Historical Stereotypes in Political Cartoons in French* (Master). Simon Fraser University.

Peifer, J. T., & Lee, T. (2019). Satire and Journalism. Satire and Journalism. https://doi.org/10.1093/acrefore/9780190228613.013.871

*Presidential election process*. USAGov. (n.d) https://www.usa.gov/election#item-36072

Rabe, L. (2018). Four South African "sunrises", four cartoons, four eras and the cyclical nature of history. *Historia*, *63*(1), 178-200 . https://dx.doi.org/10.17159/2309-8392/2018/v63n1a9

Resani, M. (2014) *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*, Dar: Karljamer Print Technology.

Shaikh, N., Tariq, R. and Saqlain, D. (2016). *Cartoon war... a Political dilema! A semitoic analysis of Political Cartoons*. Journal of Media Studies, [online] 31(1), pp.74-90.http://www.researchgate.net/publication/316407081

Sani, I., Abdullah, M.H., Ali, A.M & Abdullah, F.S. (2012). *The role of humour in the construction of Satire in Nigerian political cartoons*. Online journal of communication and media technologies,2(3) (148-153).

Saussure, F. (1966) *Course in General Linguistics* [translated by Wade Baskin]. New York: Mc Graw-Hill Book Company.

Selden, R. (1985) *An Introduction to Literary Criticism. New York: Harvester Wheatsheaf.*

Simpson, P. (2003). *On the discourse of satire: towards a stylistic model of satirical humour*

Singh, K. (2007) Quantitative Social Research Methods. SAGE, New Delhi. https://doi.org/10.4135/9789351507741

Stainbrook, E.J. (2003). Reading comics: A theoretical analysis of textuality and discourse in the comics' medium, doctoral dissertation. Indiana County: Indiana University of Pennsylvania.

Stinson, E. (2019). Satire. *Oxford Research Encyclopedia of Literature*. https://doi.org/10.1093/acrefore/9780190201098.013.1091

Tavaragi, D. M. S., & Mrs. Sushma. C, (2016). Colors and its significance. *International Journal of Indian Psychology*, *3*(2), 116–129. https://doi.org/10.25215/0302.126

*The Twelve Steps | Alcoholics Anonymous*. Aa.org. (2021). https://www.aa.org/the-twelve-steps.

Trommel, W. (2020). Good Governance as Reflexive Governance: In Praise of Good Colleagueship. *Public Integrity*, *22*(3), 227–235. https://doi.org/10.1080/10999922.2020.1723356

Townsend, K., McDonald, P., & Esders, L. (2008). How political, satirical cartoons illustrated Australia's Work Choices debate. *Australian Review of Public Affairs, 9*(1), 1-26.

Tsakona, V. (2009). Language and image interaction in cartoons: Towards a multimodal theory of humor. J. Pragmat., 41(6):11711188.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha,* Dar-es-Salaam: TUKI.

Vatz, R.E. (1973). *The myth of the rhetorical situation*. Retrieved October 01, 2019 fromhttp://www.jstor.org/discover/10.2307/40236848?uid=35369&uid=3739920 &uid =21

Ventola, E., Charles, C., & Kaltenbacher, M. (2004). *Perspectives on multimodality*. J. Benjamins Pub. Co.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Waller, A. (2021). The Electoral College Explained. *The New York Times*. https://www.nytimes.com/article/the-electoral-college.html

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wanjiru, K., 2018. The History and Development of Kenyan Comics. *Awaaz Voices*, https://www.awaazmagazine.com/volume-14-issue-3/cover-story/item/941-the-history-and-development-of-Kenyan-comics

*What the Sikh Turban Means*. We are the Sikhs. (2017). http://www.wearesikhs.org/turban.

Yu, H.-C. (2014). A Cross-Cultural Analysis of Symbolic Meanings of Color. *Chang Gung Journal of Humanities and Social Sciences*, *7*(1), 49–74.

Ziv, A. (1988). *Humor's role in married life. Humor*: The International Journal of Humor research, 1 (3),223–229.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Barua ya Chuo

LAIKIPIA UNIVERSITY

P.O. Box 1100-20300,
NYAHURURU,
KENYA

TEL: +254-(0) 20 2671779, 20-2671771;
Cell: +254 0729285902, 0729281902
bpgs@laikipia.ac.ke; www.laikipia.ac.ke

**OFFICE OF THE DIRECTOR**
**GRADUATE SCHOOL**

**Ref: MK22/2505/2017/9**

27th January 2021

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: MBURU KERRYANN WANJIKU - MK22/2505/2017**

The above named student is a Postgraduate student at Laikipia University undertaking a Master of Arts degree in Kiswahili na Mawasiliano in the School of Humanities and Development Studies.

Her research proposal entitled **"TASHTITI KATIKA VIBONZO VYA KISIASA: UCHUNGUZI WA *GADO* KATIKA MTANDAO"** was **examined and approved** by the Board of Graduate School.

She is hereby authorized to conduct her research.

Any assistance accorded to her is highly appreciated.

Thank you.

**S. Muchendu**
**For DIRECTOR**

*Vision: A University for Valued Transformation of Society*
*Mission: To serve students and society through research, education, scholarship, training, innovation, outreach and consultancy*

Laikipia University is Certified to ISO 9001:2015 and ISO/IEC 27001:2013

## Kiambatisho II: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **180512**

Date of Issue: **17/March/2021**

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Ms.. Kerryann wanjiku Mburu of Laikipia University, has been licensed to conduct research in Laikipia, Nairobi on the topic: TASHTITI KATIKA VIBONZO VYA KISIASA: UCHUNGUZI WA GADO KATIKA MTANDAO for the period ending : 17/March/2022.**

License No: **NACOSTI/P/21/9228**

**180512**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commission for Science, Technology and Innovation -